

19 JUNI, 2024

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 19 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sasa ninamwita Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, aulize swali lake.

Na. 629

**Matengenezo ya Barabara za Wilaya ya Missenyi**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, lini Bajeti ya Barabara za Wilaya ya Missenyi zenye Mtandao wa Kilometa 921 itaongezwa ili barabara hizo zitengenezwe kwa ubora?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa taarifa kuwa, Serikali imeshaongeza bajeti ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za Wilaya ya Missenyi kutoka shilingi milioni 723.85 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 2.42 mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya kutengeneza barabara kwa nchi nzima kadri ya upatikanaji wa fedha ikiwemo kuongeza bajeti kwa Wilaya ya Missenyi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ninaipongeza Serikali. Ni kweli awali Wilaya ya Missenyi ilikuwa inapata bajeti ya shilingi milioni 700 na leo tunapata shilingi bilioni 2.4. Pamoja na hayo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na bajeti hiyo kuongezeka lakini bado mtandao wa barabara ambao unatekelezwa kila mwaka ni kilometa 145 ambao ni sawa na 15% ya mtandao mzima ndani ya Wilaya ya Missenyi wa kilometa 921. Je, sasa Serikali haioni kwamba hiyo asilimia ni ndogo sana, ni muda muafaka wa kutuongezea bajeti ili angalau kiwango cha asilimia ya utekelezaji wa bajeti kila mwaka iweze kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Wilaya ya Missenyi ni Wilaya ambayo inapata mvua katika kipindi cha mwaka 75% na iko katika Uwanda wa Chini ambao unakusanya maji mengi kutoka maeneo mbalimbali na hivyo barabara ndani ya Wilaya ya Missenyi kuhitaji kuinuliwa na hiyo inahitaji gharama kubwa sana. Je, hiyo siyo sababu Serikali ione haja ya kuongeza bajeti ndani ya Wilaya ya Missenyi ili barabara zitengenezwe na kuweza kupitika kwa kipindi cha mwaka mzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifanya kazi kubwa sana ya kuwasemea wananchi wake na katika muktadha huu kuwasemea katika kuhakikisha wanapata miundombinu iliyo bora ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti kila mwaka. Kama nilivyosema mwaka 2020/2021 kulikuwa na bajeti ya shilingi milioni 700 lakini tunavyozungumza mwaka huu 2023/2024 tuna bajeti ya shilingi bilioni 2.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kuna ongezeko pia la urefu wa barabara ambazo zimejengwa katika kipindi hicho kutokea kipindi cha mwaka 2020/2021 ambapo kulikuwa na kilometa 35.5 tu za barabara hizi za lami. Tunavyozungumza mwaka huu, 2023/2024 tumefikia kilometa 146. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kuhakikisha inatenga fedha kila mwaka kuboresha miundombinu ya barabara katika Wilaya ya Missenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli Wilaya ya Missenyi inatuamisha maji. Miundombinu mingi inatuamisha maji na ni kutokana na jioografia ya Wilaya hii. Kutokea kipindi cha mwaka 2021/2022, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kuinua vipande tofauti tofauti vya barabara na hasa vile ambavyo ni korofi ili kuondoa maji kutuama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021/2022, kipande cha kilometa 2.4, Barabara ya Mabuye – Itara kilinyanyuliwa kwa jumla ya shilingi milioni 298. Mwaka 2022/2023 kilometa 3.2 zilinyanyuliwa katika kipande cha Barabara cha Mabuye – Itara kwa jumla ya shilingi milioni 205, lakini mwaka 2023/2024, kuna kipande cha kilometa nane cha Byeju – Nkerenge ambacho kimetumia shilingi milioni 170 kimenyanyuliwa lakini kwa wakati huu bado Serikali inaendelea kunyanyua kipande cha *Kagera Sugar – Bubare,*

19 JUNI, 2024

barabara hiyo, cha kilometa 8.5 kwa jumla ya shilingi milioni 160. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba inaondoa changamoto hizi za kutuama maji kwenye barabara katika wilaya yako Mheshimiwa Mbunge. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Danielson Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Changamoto ya ufinyu wa bajeti kwenye ujenzi wa barabara kule Missenyi inafanana sana na hali ilivyo kule Arumeru Mashariki ambako tuna mtandao wa barabara wa kilometa 800. Pia, hali ya kijiografia ni ngumu kiasi kwamba fedha ambazo zinapatikana inakuwa ni shida, hazitoshelezi kujenga zile barabara. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza hiyo bajeti ili iweze kufanya barabara zitengenezeke? Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba miundombinu ya Barabara, lakini jiografia ya eneo la Arumeru Mashariki ni ya milimani. Kumekuwa na changamoto pia katika miundombinu na Mheshimiwa Mbunge tumekuwa tukizungumza naye mara kwa mara kuhusiana na barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inajenga barabara hizi za wilaya ziwe katika hali ambayo inapitika mwaka mzima. Nikuhakikishie, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba inajenga na kuhudumia barabara zilizoko katika Jimbo lako la Arumeru Mashariki. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

19 JUNI, 2024

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Weekend hii nimekuwa jimboni na nikapita katika daraja moja ambalo lilijengwa na *TARURA* na bahati mbaya nikaona limekatika sana katika Kijiji cha Nyamihuu. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutuongezea bajeti ili sasa turekebishe madaraja yote yaliyokatika katika Jimbo la Kalenga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba, kutokana na mvua nyingi ambazo zimekuwa zikinyesha nchini, miundombinu ya barabara imepata athari. Mheshimiwa Mbunge amezungumza kuhusiana na suala la daraja hili la Nyamihuu katika Jimbo lake la Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba, kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha Serikali inarudisha mawasiliano kwenye maeneo yote ambayo mawasiliano yamekatika na inafanya hivyo kwa udharura. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu, mimi na yeye tutazungumza tuone kama daraja hili lipo katika kiwango hicho na linahitaji udharura, basi kuna kila haja ya Serikali kuweka nguvu kuhakikisha inaenda kurekebisha daraja hilo na miundombinu mingine ambayo inakata mawasiliano kwa sababu, lengo la Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ambayo mawasiliano yamekatika Serikali inarudisha mawasiliano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Labda Mheshimiwa Naibu Waziri, madaraja ni mengi na ni sehemu nyingi. Madaraja ya maeneo mengi hasa Mikoa ya Kusini yamekatika tangu mwezi Februari na Machi, mengine mpaka leo hayajarekebishwa. Kwa sababu Serikali wapo hapa, ninadhani waongeze jitihada kwenye eneo hili ili tuweze kukamilisha haya madaraja kwa wakati. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Tunaenda swali linalofuata. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 630

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Kibondo Mjini kwa  
Kiwango cha Lami**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Kibondo Mjini yenye urefu wa Kilometa sita kwa kiwango cha lami kama ilivyotolewa na Rais wa Awamu ya Tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara za lami Kibondo Mjini ambazo zitachochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi. Kati ya mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024, jumla ya kilometa 5.85 za barabara za lami zimejengwa na kukamilika katika Mji wa Kibondo. Ujenzi wa kilometa 2.5 kwa tabaka la lami unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mpango wa bajeti wa mwaka 2024/2025, zitajengwa barabara za lami kilometa 1.37. Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) itaendelea kuihudumia na kuiboresha miundombinu ya barabara za Kibondo Mjini kadri fedha zinavyopatikana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, hata hivyo ninayo maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; Jimbo la Muhambwe lina mtandao wa barabara wa kilometa 636 na kati ya hizo 636, ni hizo kilometa tano tu za Kibondo Mjini ndiyo ambazo zina lami na

19 JUNI, 2024

lami hiyo tuliitekeleza kwa pesa za kutoka kwenye Bodi ya Mfuko wa Maendeleo ambazo kwa bajeti hii ya 2024/2025, pesa hizo tumeondolewa hazitakuwepo. Je, Serikali haioni sasa iko sababu ya kuturudishia hizi shilingi milioni 800 kutoka kwenye Bodi ya Mfuko wa Maendeleo ya Barabara ili tuweze kuendeleza kujenga barabara za lami Kibondo Mjini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mvua zilizoendelea hapo awali hapa nchini nazo zimeathiri sana barabara za Jimbo la Muhambwe hususan Barabara ya Lukaya – Kigina ambayo haipitiki kabisa na Kata ya Rugongwe ndiyo kata inayoongoza kwa mazao. Pia, barabara ya Kibondo kwenda Murungu, daraja la Nyavyumbu limekatika kabisa. Je, ni lini Serikali itatuletea pesa za dharura ili tuweze kutengeneza hizi barabara zilizokatika angalau wananchi waweze kupita mahali hapo ili kupunguza athari? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Florence Samizi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatetea wananchi wake wa jimboni kwake. Mheshimiwa Mbunge, ninaomba nikuhakikishie kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuboresha miundombinu ya barabara katika jimbo lako. Ndiyo maana katika mwaka wa bajeti 2023/2024, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara katika jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara, jumla ya kilometa 110, lakini ujenzi wa makalavati 32. Kwa hiyo, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ya barabara katika Wilaya ya Kibondo na nikuhakikishie, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha inaboresha miundombinu ya barabara hizi.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mbunge amezungumza kuhusiana na fedha za dharura na kukatika kwa mawasiliano katika Barabara ya Lukaya – Kigina. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeshatoa jumla ya shilingi milioni 105 kwa ajili ya kufanya jitihada za kidharura katika jimbo lako hili. Fedha hizo zinaenda kujenga *box culverts* lakini inaenda kufanya matengenezo katika maeneo yale ambayo yamepata athari kubwa ya mawasiliano, athari kubwa ya mvua, lakini pia kurejesha mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 11 kwa ajili ya kuendelea kufanya matengenezo katika sehemu korofi za barabara hiyo. Mheshimiwa Mbunge, kwa ujumla wake, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu katika barabara zetu hizi za wilaya. Serikali itaendelea kuhakikisha inatafuta, inatenga na kuleta fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara hizi ikiwemo katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya kutoka Mkuyuni – Igelegele – Mahina – Mandu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais toka mwaka 2021. Nimekuwa nikiuliza barabara hii kila leo na leo ni mara ya sita. Mara ya mwisho Mheshimiwa Naibu Waziri alituahidi mvua zitakapokamilika barabara hii itatangazwa na kuanza kujengwa kwa sababu kila hatua imeshakamilika. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kuhakikisha barabara hii inaanza kujengwa mara moja na kuwapunguzia adha wananchi wa maeneo karibia kata sita za barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri.



19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiulizia sana hii barabara hapa Bungeni lakini hata huko mtaani tukikutana bado huwa anaulizia mustakabali wa ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ahadi za Viongozi Wakuu (ahadi ya Mheshimiwa Rais) aliyotoa mwaka 2021 ni kipaumbele katika utekelezaji wa mipango ya Serikali na tayari fedha zimeshatengwa kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hii. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kawaambie wananchi wako tunakuja kujenga barabara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona. Ninataka kujua ni mpango gani sasa wa Serikali kuweka lami katika Barabara inayotoka Singida Mjini – Kinyeto – Merya – Sagara kwa kiwango cha lami ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Marehemu Hayati Dkt. Magufuli, lakini pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi pia alipopita Katibu Mkuu Dkt. Nchimbi, wananchi walimlilia barabara hii iwekwe lami. Sasa, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hii kwa wananchi ambao barabara hii ni ya muhimu sana kiuchumi kwa wananchi wale? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara hii ya Singida Mjini kuelekea Sagara na hasa katika kuchochea maendeleo na kuchochea uchumi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema hapo awali, ahadi za Viongozi Wakuu ni kipaumbele

19 JUNI, 2024

namba moja katika kutekeleza au katika mipango ya utekelezaji wa shughuli za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafuatilia barabara hii ili fedha ziweze kuja kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Amsabi Mrimi.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mvua nyingi zilizonyesha katika Jimbo la Serengeti, Barabara za Bwitengi – Miseke na Mugumu – Machochwe zimeharibika sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya marekebisho ya haraka? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua madhara makubwa ambayo yametokea kwenye barabara zetu hizi za wilaya ambayo yamesababishwa na mvua. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua na tayari inafanya jitihada kuhakikisha kwamba inarudisha mawasiliano maeneo ambayo mawasiliano yamekatika, lakini inaboresha na kufanya ukarabati wa barabara kwenye maeneo yale ambayo yameharibika na barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuhakikisha kwamba barabara hizi, mtandao huu wa barabara za wilaya unakuwa ni mtandao wa barabara ambazo zinapitika mwaka mzima. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali ipo kazini na tutafanya jitihada zote ili kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu ya barabara hizi za wilaya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Wabunge. Tunaendelea na

19 JUNI, 2024

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 631

### **Ujenzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria – Muleba**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Kata sita za Wilaya ya Muleba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Kata Sita za Muleba, Magata, Kurutanga, Gwanseli, Bureza, Kikuku na Kagoma, Wilayani Muleba Mkoani Kagera. Kwa sasa, Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji safi na salama katika kata hizo, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Miradi ya Maji minne ya Ilemela, Karutanga, Butembo na Kagoma inayohudumia wananchi 22,279 waishio katika Vijiji nane vya Ilemela, Gwanseli, Bureza, Butembo, Makarwa, Kikuku, Kagoma na sehemu ya Kijiji cha Nsisha. Aidha, upanuzi wa Skimu za Maji za Karutanga na Butembo kwenda Kijiji cha Magata na Kitongoji cha Umdangara Muleba Mjini unaendelea ambapo unatarajia kukamilika mwezi Septemba, 2024 na kunufaisha wananchi 2,780.

**MWENYEKITI:** Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria

19 JUNI, 2024

ulianza kama siyo mwaka 2009 mpaka leo haujaanza kutekelezwa na mwaka jana Serikali ilitenga shilingi milioni 850 kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huu hatua kwa hatua. Je, ni kitu gani kimefanyika mpaka leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Muleba Magharibi ambayo ina tatizo kubwa la maji inapata maji na wananchi wake wanatokana na adha ya ukosefu wa maji? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali inatambua ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge alichokiongelea kwamba mradi huu ulianza mwaka 2009 na kweli kabisa katika bajeti iliyopita shilingi milioni 850 ilitengwa. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia kwa faida ya wananchi wake wa Muleba Kusini nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali inatenga fedha, lakini pia inaendana na upatikanaji wa fedha. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa mradi huu, Serikali imejizatiti kwa sababu inatambua umuhimu mkubwa sana kwa ajili ya wananchi wa Muleba Kusini kupata maji ya kutoka Ziwa Victoria. Ni jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiliongelea, kama Tabora wanapata maji ya Ziwa Victoria lakini wao wapo karibu pale na kweli Serikali imelitambua hilo na inaliangalia kwa kina vizuri kabisa na tunaendelea kutafuta fedha ili zikishapatikana tu mradi huu uanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna miradi mikubwa, miradi ya kati na miradi ya muda mfupi, tumeanza na maeneo mengine kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi, tumeanza na zile kata zingine ambazo tunaenda kutoa huduma kwa watu wapatao 2,780, lakini pia tunachukua maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwa eneo la Muleba Magharibi ili kuhakikisha kwamba tunaliingiza katika utaratibu wa utekelezaji wa miradi yetu ya

19 JUNI, 2024

muda mfupi ili wananchi wa Muleba Magharibi na wao wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaanza kusambaza maji yanayotoka Kisarawe II katika Kata ya Mbagala Kuu, Kijichi, Toangoma, Kiburugwa na Mbagala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuwasemea vizuri sana wananchi wa Mbagala. Vilevile tunampongeza sana kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa katika kuibua changamoto ambazo zinahusiana na Sekta ya Maji ndani ya jimbo lake na sisi Serikali tunaendelea kuzichukua na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie katika bajeti yetu ambayo tumeipitisha mwezi uliopita tunaamini kabisa kwamba pindi dirisha la utekelezaji wa bajeti hiyo litakapofunguliwa na tutaanza, siyo kwa upande wa Mbagala peke yake, ni upande wote wa Dar es Salaam ambao umekuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. Kwa hiyo, upande wa Mbagala tutapata fursa hiyo ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza miradi hiyo ya kusambaza maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge swali alilouliza Mheshimiwa Chaurembo na namna ambayo ameuliza ndivyo ambavyo Mheshimiwa Spika anatarajia Wabunge tuulize hivyo, maswali yawe ya moja kwa moja na Waheshimiwa Mawaziri majibu yawe ya moja kwa moja ili kutoa fursa kwa Wabunge wengi kuuliza maswali yanayowahusu wananchi.

Tunaenda swali linalofuata, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

19 JUNI, 2024

Na. 632

### **Kutoa Huduma ya Maji Bure Vijijini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa huduma ya maji bure vijijini kama ilivyo kwenye baadhi ya huduma za Elimu na Afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya Mwaka 2019, Kifungu cha 43(1)(a), Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ina jukumu la kupanga, kusanifu na kujenga miradi ya maji vijijini. Aidha, baada ya miradi hiyo kukamilika, skimu za maji hukabidhiwa kwa Vyombo vya Utoaji wa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) ambavyo vimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 32 na 33 cha sheria tajwa kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo (*Operation & Maintenance*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia CBWSOs, jamii inahusishwa katika kupanga bei za utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi kwa kuzingatia teknolojia ya skimu inayotumika pamoja na hali ya uchumi ya jamii ya eneo husika. Vilevile, makundi maalum ya watumiaji wa maji katika jamii inayoweza kumudu gharama za uchangiaji na huduma hizo isiyoweza kumudu gharama za uchangiaji wa huduma hiyo kuwekewa utaratibu na kuyapatia huduma ya maji bure bila kuathiri shughuli za uendeshaji na matengenezo ya skimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na sheria iliyopo ambayo inataka wananchi

19 JUNI, 2024

kushirikishwa katika kupanga bei, hali halisi ni tofauti, maeneo mengi wananchi hawashirikishwi. Mfano, Wilaya ya Lushoto, Lukozi na Kata ya Lukozi, Kata ya Shume na Manolo, bei zilipelekwa kubwa ikamlazimu Mkuu wa Wilaya kwenda kushusha bei za maji kwa wananchi, nini hatua ya Serikali kudhibiti hali hii? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa gharama hizi zinasababishwa na wananchi kugharamia mafundi wa *local fundi* wanaokwenda kukarabati miradi hiyo. Je, Serikali haioni imefika muda muafaka kuwaajiri na kuwalipa mishahara *local fundi* na kuondoa mzigo huo kwa wananchi? Nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za huduma ya maji zinapangwa kutokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza; uzalishaji, eneo ilipo skimu husika, aina ya utoaji wa huduma, lakini vilevile na aina ya jamii inayozunguka eneo husika, lakini kwa mujibu wa sheria na *EWURA* anaingia katika upangaji wa bei ya maji. Kwa kuzingatia *factor* hizo zote, Serikali imekuwa ikiingilia kati pale ambapo tunaona kwamba kuna changamoto na ndiyo maana Mkuu wa Wilaya ni sehemu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo Waziri wetu wa Maji Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, katika bajeti yetu tumepanga kuwepo na fedha za *monitoring and evaluation* kwa ajili ya wakuu wa wilaya pale ambapo kunakuwa na changamoto ya utekelezaji wa mradi au uendeshaji wa miradi, Mkuu wa Wilaya aweze kufika eneo husika na kutoa maelekezo ya Serikali, hilo tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linatokana na uzembe wa uendeshaji wa wataalam ambao wamekabidhiwa jukumu la kuendesha na hayo yote tumekuwa tukiyafuatilia na kuchukua hatua stahiki. Sote tutakubaliana, sheria kuwepo ni jambo moja, utekelezaji wa sheria ni jambo lingine, kwa hiyo,

19 JUNI, 2024

tumejitahidi sana kuhakikisha watu wetu wanaendelea kusimamia na kuhakikisha sheria haivunjwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu ajira kwa mafundi, ni kweli kabisa changamoto hii tumeanza kuiona baada ya kugundua kwamba kuna CBWSOs wameshindwa kujiendesha na wale *local fundi* wanashindwa kuwalipa, inasababisha hata ile miundombinu yetu kuendelea kuchakaa na kuharibika. Kwa sasa tayari tumeshaanza kukusanya maoni, namna bora zaidi ya kwenda kuendesha CBWSOs bila kuleta mzigo mkubwa kwa wananchi ambao wanatarajia kutumia huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, katika kufanya tathmini yetu na yeye tutamfikia kwa ajili ya kuomba maoni yake ili tuweze kuboresha zaidi na hatimaye gharama kwa wananchi iwe *reasonable*, lakini uendesaji wa miradi yetu na miundombinu isiweze kuharibika kwa kukosa fedha ambazo zingesaidia sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaanza kuweka mita za maji ambazo unalipia kabla ya matumizi kama ilivyo kwenye LUKU ili kuepusha malalamiko ya wananchi ya kubambikiwa bili za maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Bupe, kwa kuendelea kuwa mdau mkubwa sana katika sekta yetu ya maji na kwa kuendelea kuwa msemaji wa akina mama kutoka katika mkoa wake. Haya kwanza ni maelekezo ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi tumeshayachukua na tayari tumeshaanza kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais. Vilevile naomba niseme kitu kimoja kwamba jambo ambalo sisi tunaenda kulifanya, tunaenda kwenye *smart prepaid water meter* ambayo ni tofauti kidogo na LUKU. (Makofi)



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaponunua LUKU unamtumia mtu *token* anaingiza, sisi tunataka kwamba mtu akiwa Dar es Salaam maji yake yameisha Dodoma ana uwezo wa kununua maji yake ndani ya sekunde 20 tayari kule *valve* inakuwa imeshaachia imeshasoma na kuanza kutoa maji, hakuna haja ya kupitia njia nyingi nyingi kuhakikisha kwamba unatuma kwa mtu halafu anaingiza LUKU, hapana, sisi tunaenda kwenye *smart prepaid water meter* kuhakikisha kwamba itapunguza changamoto kwa wananchi kubambikiwa kama ambavyo Mheshimiwa amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine itasaidia upotevu wa maji ambayo imekuwa ni changamoto kubwa sana, Serikali kuzalisha maji kwa gharama kubwa, lakini mengine yanapotea bila ya kuwa na sababu. Tatu, itasaidia kwa wananchi wenyewe kujua matumizi halisi ya familia zao na kuji-*regulate* wao wenyewe kuhakikisha kwamba hatuendi kwenye upotevu wa maji ambayo yalikuwa yanapotea bila ya kuwa na sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imeshajipanga tayari na tayari hivi tunavyoongea Mheshimiwa Waziri yupo China na ameenda kutembelea viwanda ambavyo vinazalisha *smart prepaid water meter* na atakaporejea tunaamini kwamba tutakuwa na jibu na muarobaini wa tatizo ambalo limekuwa likitusumbua katika Sekta ya Maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 633

**Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo na Wilaya – Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

19 JUNI, 2024

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Uvinza pamoja na Mahakama za Mwanzo Kalya na Buhingu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Serikali majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Uvinza ni miongoni mwa Mahakama 18 za Wilaya zilizojengwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ujenzi wa Mahakama hii ulikamilika na kuanza kutoa huduma za kimahakama tangu mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama, Mahakama ya Mwanzo ya Buhingu imepangwa kujengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kadri fedha zitakapopatikana Mahakama ya Mwanzo Kalya itajengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, maswali ya nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwanza naomba nikiri kwamba Mahakama ya Wilaya ya Uvinza imeshajengwa na hili swali ni la siku nyingi sana na limekuja tena mara ya pili. Niliacha kulizuia lisiulizwe kwa sababu ya hizi mahakama mbili; sasa ninafahamu kwamba mwaka wa fedha 2023/2024, Mahakama ya Buhingu ilitengewa fedha kwa ajili ya kujengwa, lakini ujenzi ule haukufanyika. Swali la kwanza; je, ni lini fedha hizi zitakuja kwa ajili ya kujenga hiyo Mahakama ya Mwanzo ya Buhingu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; zipo Mahakama ya Nguruka, Uvinza na Ilagala, Mahakama hizi zimechakaa sana, je, ni lini zitapelekewa fedha kwa ajili ya ukarabati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba ni kweli ilipangwa bajeti katika mwaka wa fedha uliopita, lakini hadi mwaka unamalizika fedha hiyo haikuweza kutoka. Hivi sasa nimpe uhakikisho Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Kusini, kwamba Mahakama hii ya Buhingu taratibu sasa hivi zilizofikiwa ni kwenye hatua ya manunuzi kwa maana ya fedha zipo, mara taratibu zitakapokamilika ujenzi wa Mahakama hii utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Uvinza na Ilagala ambazo ni za muda mrefu, tunakiri kuwepo kwa Mahakama ambazo zinahitaji ukarabati au kujengwa upya kulingana na kiwango cha uharibifu au uchakavu na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kadri hali ya fedha itakavyoruhusu Mahakama zote hizo zitakarabatiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Shinyanga ina halmashauri mbili, Halmashauri ya Shinyanga ipo mbali na mjini na Mahakama ipo mjini pale manispaa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Mahakama yenye hadhi ya wilaya katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wazo la Mheshimiwa Mbunge, linapokelewa lakini katika mpango wa Mahakama ambao ni sehemu ya Serikali Kuu ni Mhimili unaozingatia sehemu ya Serikali Kuu tunapenda kujenga Mahakama hizi Makao Makuu ya Wilaya ambapo kuna DC kama unavyofahamu usimamizi wa nidhamu na maadili ya Mahakimu wa ngazi ya wilaya husimamiwa na waheshimiwa ma-DC. Kwa hiyo, tunapendelea zaidi kwenye ngazi ya wilaya tuwe na Mahakama moja ya ngazi ya wilaya. Kwa hiyo, ninafahamu changamoto aliyonayo, lakini kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu hizi huduma zitapelekwa karibu na wananchi.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya kupunguza adha kule Shinyanga kuna Mahakama za mwanzo ambazo zinajengwa. Katika Mkoa wa Shinyanga tunajenga, Kishapu kama wilaya kutakuwa na Mahakama ya Wilaya mwaka huu, lakini zipo Mahakama nyingine mbili za mwanzo zinajengwa kama juhudi za Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kupeleka huduma za haki karibu zaidi na wananchi maeneo ya Malunga na maeneo ya Majengo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 634

### **Barabara ya Makofia – Maneromango Kutengewa Fedha**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za Ujenzi wa Barabara ya Makofia - Mlandizi - Mzenga hadi Maneromango kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Makofia – Mlandizi - Mzenga hadi Maneromango yenye urefu wa kilometa 100 umefanyika na kukamilika. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mlandizi – Ruvu SGR kilometa 23 ikihusisha kilometa 15 za Barabara ya Makofia – Mlandizi – Mzenga - Maneromango kipande cha kutoka Mlandizi hadi *Ruvu Junction* na *Roundabout* ya Makutano ya Mlandizi. Kwa sasa taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Mlandizi – *Ruvu SGR* kilometa

19 JUNI, 2024

23 zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2024. Kwa sehemu iliyobaki Serikali inaendelea kutafuata fedha za kuendelea na ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, ni mara ya kwanza kwa Barabara hii ya Makofia – Mlandizi – Maneromango kupata jibu la matumaini kwamba, awamu hii ya sita imeanza kutekeleza ujenzi wake kwa kipande cha kilomita 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ninataka niulize kwa kuwa, katika barabara hii vipo vijiji kwa mfano, Kijiji cha Matimbwa na Yombo, wananchi walifanyiwa tathmini, kwa ajili ya kulipwa fidia. Je, Serikali haioni haja sasa ya wananchi walio kando ya barabara hii, wakiwemo wa Vijiji vya Matimbwa na Yombo, kulipwa fidia wakati Serikali ikitafuta fedha za ujenzi wa kipande kilichobaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kwa kuwa, wakati wanawasilisha bajeti ya Wizara ya Ujenzi walitupa matumaini Wakazi wa Bagamoyo juu ya ujenzi wa Daraja la Mpigi Chini na kwamba, watamsimamia mkandarasi, ili aendelee na kazi. Je, Serikali ipo tayari kutimiza ile ahadi yao ya kupandisha hadhi kipande cha Barabara ya Mingoyi – Kiembeni inayunganishwa na Daraja hili la Mpigi Chini ili kuwarahisishia Wakazi wa Bagamoyo na Kinondoni, kwa ajili ya mawasiliano? Naomba kuwasilisha na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua jitihada za Serikali. Namhakikishia kwamba, suala hili tunalifanya haraka sana kwa sababu ni barabara ambayo inaenda kuunganisha Mji wa Mlandizi pamoja na Kituo cha SGR na tayari tupo kwenye hatua za mwisho kabisa za manunuzi.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ya vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, tayari tulishawasilisha jedwali ambalo limehahakikiwa na lipo Hazina likisubiri tu fedha itoke tuweze kuwalipa wananchi hawa ambao watapisha ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Daraja la Mpigi Chini; ni kweli kwamba, daraja hili lilishapata mkandarasi. Mimi binafsi nimeenda, lakini pia, Waziri ameenda pale na kutoa maelekezo ni nini mkandarasi aweze kufanya. Katika mito ambayo ilipanuka sana ni pamoja na eneo hili ambalo mkandarasi alikuwa analijenga kwa hiyo, kuna haja ya kufanya mapitio upya ya usanifu uliokuwa umefanyika kwa sababu, daraja hili limeongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupandisha hadhi barabara aliyoitaja; namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, taratibu zipo, tunasubiri maombi kutoka Mkoa ambayo tathmini itafanyika na wataalam wetu mara tutakapopata maombi rasmi ya kupata Mkoa kama taratibu zilivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, kabisa naanza kuipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza ahadi yake ya ujenzi wa kilomita mbili kwenye Mji wetu wa Kharumwa ambapo sasa hivi kilomita moja inaenda kukamilika ndani ya wiki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na ahadi pia, ya kufungwa taa. Je, ni lini Serikali, baada ya kukamilisha hii kilomita moja, itaanza kufunga taa na kuanza ujenzi wa kilomita ile nyingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa ufupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye bajeti, Kharumwa ni Makao Makuu ya Wilaya

19 JUNI, 2024

ya Nyang'hwale na mpango ni kuhakikisha kwamba, miji yote na hasa kwa kuwa, tumejenga lami nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna mpango wa kufunga taa karibu katika Wilaya zote, Makao Makuu ya Wilaya, ukiwepo na Mji wa Kharumwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itamalizia kilomita 35 Barabara ya Uchumi iliyoanzia Ziwani – Madimba – Msimbati kwa kiwango cha lami ambako kuna mitambo na visima vya gesi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, barabara aliyoitaja ndiyo inaenda kwenye visima vyetu vya gesi kilomita 35 na kama atakuwa ameona, bajeti tumepitisha na ipo kwenye mpango kuanza kujenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami katika mwaka unaokuja wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, ujenzi wa Barabara ya Mnivata – Newala hadi Masasi umeshaanza; na Kwa kuwa, ujenzi huu una miradi ya kijamiii ambayo mkandarasi anatakiwa aijenge kama CSR. Je, ni lini miradi hiyo ya kijamii itaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi huu ambao unafadhiliwa na *African Development Bank*, una miradi ambayo tunaita *complementary projects*. Miradi hii inajengwa tutakapokuwa tumekamilisha taratibu zote, ikiwa ni pamoja na usanifu na kuhakikisha kwamba, itasimamiwaje. Kwa kawaida, labda kama kuna changamoto, inatakiwa iende sambamba na ujenzi wa barabara yenyewe, lakini kama kuna changamoto kuanza. Basi naomba nikutane na Mheshimiwa Mbunge, ili tuone kama kuna mkwamo sehemu yoyote, basi tuweze kuikwamua kwa sababu, fedha hiyo ipo. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuata, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo.

Na. 635

### **Ukarabati wa Nyumba za TBA Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanyia ukarabati nyumba chakavu za TBA zilizopo Bagamoyo na kujenga nyingine mpya, ili watumishi na wateja waishi vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ulifanya ukarabati kwa kujenga upya mifumo ya majitaka kwenye nyumba zote 52 za makazi zilizopo Bagamoyo. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi, kupitia TBA, imetenga kiasi cha Shilingi 450,000,000.00 kutoka kwenye Bajeti ya Fedha za Ruzuku ya Serikali, kwa ajili ya ukarabati wa nyumba zilizorejeshwa TBA kutoka TAMISEMI katika Mikoa 20, zikiwemo nyumba zilizopo Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Aidha, Serikali imeandaa Mpango wa Ujenzi wa Nyumba za Makazi kwenye maeneo



19 JUNI, 2024

yaliyorejeshwa kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ikiwemo Bagamoyo na utekelezaji wa mpango huo tayari umeanza katika maeneo mbalimbali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkenge, tafadhali.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, eneo hili lenye nyumba 52 mpaka sasa bado linajaa maji pale mvua zinaponyesha. Swali langu la kwanza; je, ni lini sasa Serikali itafanya maamuzi magumu ya kuwauzia hizi nyumba wananchi wanaoishi pale ili waweze kulipa malipo ya kidogo kidogo ili wazimiliki wao na waweze kuzikarabati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja kutembelea pale katika zile nyumba aone jinsi zilivyochakaa na kuthibitisha kwamba, hizo pesa ambazo ametenga, kwa ajili ukarabati hazitoshi kabisa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutembelea Bagamoyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni wajibu wetu na tukubaliane tu, baada ya kipindi hiki cha Bunge ni lini tuweze kwenda pamoja katika maeneo hayo ili twende tukaangale hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza alilouliza Mheshimiwa Mbunge kuhusu maji kujaa tumelipokea. Nawaagiza Mameneja wa Mkoa wa TBA, Mkoa wa Pwani pamoja na Mtendaji Mkuu waweze kuangalia changamoto ni nini kuhusu kujaa maeneo haya ya nyumba za Serikali kwa maana ya TBA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuuza hizo, nadhani tathmini itafanyika kuona kama Serikali kuna haja ya kuziua ama kuendelea kuzibakiza. Kwa hiyo, namuagiza Mtendaji Mkuu aweze kwenda eneo hilo afanye tathmini na wao wataishauri Serikali kama kuna haja ya kuziua ama ziendeleo kuwa za

19 JUNI, 2024

umma, kwa ajili ya kusaidia watumishi wengine wa umma. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na kasi ya ujenzi wa viwanda kwenye Mji wa Mlandizi na Kwala. Ni nini mpango wa Serikali kuiagiza TPA na NHC kujenga makazi, ili wakazi wafanyakazi wa eneo lile waje kupata huduma bora ya makazi? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kulichukua suala ama wazo la Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha, ambapo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi pamoja na wenzetu wa Ardhi wana NHC tuone namna ambavyo tunaweza kufanya, ili kuweza kujenga majengo ambayo Mheshimiwa Mbunge nadhani atakuwa ni msada mkubwa katika maeneo haya ili kutoa huduma bora kwa watumishi watakaokuwepo katika eneo hilo. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuata ni swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum. Kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Grace Tendega.

Na. 636

### **Ujenzi wa Barabara ya Iguguno hadi Ndunguti – Mkalama**

**MHE. GRACE V. TENDEGA K.n.y. MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Iguguno hadi Nduguti – Mkalama itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Iguguno – Nduguti – Gumanga – Mkalama yenye urefu wa kilometa 89 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami katika Mji wa Nduguti kwa sehemu ya kutoka Nduguti *Roundabout* kuelekea Iguguno (kilometa 7.5), Nduguti *Roundabout* kuelekea Gumanga (kilometa 2.0), Nduguti *Roundabout* kuelekea Nkungu (kilometa 0.5). Taratibu za zabuni ziko hatua za mwisho na mkataba unatarajiwa kusainiwa Mwezi Julai, 2024. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Barabara ya *Iringa Bypass* kilometa 7.3 ni barabara ya mchepuo na tayari mkataba umeshasainiwa. Ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; nini mkakati wa Serikali kufanya marekebisho ya barabara maeneo hatarishi ya Mlima Kitonga ambako mara nyingi kumekuwa kukitokea ajali na hasa kwa usalama wa magari mazito? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Iringa Bypass* kilomita saba tulishaanza. Barabara ile ilikuwa haipo na tunachofanya ni kuifungua na baada ya kuifungua itawekewa lami kilomita hizo saba na hata kwenye bajeti tumeipangia. Tunaendelea na tutahakikisha kwamba, tunaikamilisha.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kurekebisha Barabara ya Kitonga, wakandarasi wapo *site* na kazi inaendelea. Kazi inayofanyika pale ni kupanua kona, lakini pia, tumeanza kuweka mpango wa taa, ili kusaidia kwenye kona kali iwe ni rahisi kwa madereva kuona magari na kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikiendelea. Tutahakikisha kwamba, Mlima wote ule tunaukamilisha kwa kuupanua pamoja na kuweka taa ambazo zinasaidia sana madereva kutokugongana kwa sababu, wanaonana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ni lini itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Lami ya Kibada – Kisarawe II – Mwasonga mpaka Tundwi, Songani katika Halmashauri ya Kigamboni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi alishasaini kilomita zote 41 na tunategemea muda wowote ataanza kufanya kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara ya Pofu – Mandaka – Kilema ni Barabara ya *TARURA*, lakini ilitetekezwa. Kwa hekima ya *TANROADS* kwa kuona umuhimu wa kuunganisha Barabara ya Kawawa – Pakula – Marangu Mtoni wamekuwa wanadunduliza fedha kidogo pale na wamejenga kama kilomita tatu sasa, zimebaki kilomita tano. Je, Serikali ipo tayari kuiwezesha *TANROADS* kukamilisha barabara hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa ufupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hizi mbili TANROADS na TARURA zimekuwa zikifanya kazi kwa pamoja na tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. TANROADS na TARURA, kwa maana ya Mkoa na hata Watendaji Wakuu, waone uwezekano wa kuweza kuona namna ambavyo TANROADS wanasaidia kujenga hii barabara, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mara kadhaa Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge na wananchi wa Kyerwa kwamba, Barabara ya Bugene kwenda mpaka Kaisho, kilomita 50, mkataba umesainiwa na mkandarasi amepatikana, lakini muda wote tunasubiri barabara ianze, haianzi. Tunataka Waziri awaambie Watu wa Kyerwa ni lini ujenzi unaanza na ni kwa muda gani utakamilika? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hizo kilometa 50 tayari mkandarasi alishapatikana na alishasaini mkataba. Sasa hivi yupo kwenye taratibu za kufanya maandalizi ya awali, ili aanze kujenga kwa hiyo, Wanakyerwa wawe na uhakika hiyo barabara Serikali inaenda kujenga kilomita 50. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaenda swali linalofuata. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 637

### **Ujenzi wa Barabara ya Kiranjeranje hadi Ruangwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

19 JUNI, 2024

Je, ni lini ujenzi wa Barabara ya Kiranjeranje – Nanjilinji – Ruangwa kwa kiwango cha lami utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kiranjeranje – Nanjilinji – Namichiga – Ruangwa yenye urefu wa kilometa 120 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Ruangwa Mjini hadi Namichiga (kilometa 20) yanaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa *RISE* ambapo mkataba wa ujenzi unategemewa kusainiwa mwezi Agosti, 2024. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kassinga.

**MHE. ALLY M. KASSINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali yanayoleta matarajio kwamba, barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami huku Serikali ikitafuta fedha, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara hii ya kilometa 120 Kiranjeranje mpaka Ruangwa, Jimboni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, inapitiwa na mito mitatu na Madaraja matatu ya Kigombo, Nakiu pamoja na Mto Mbwemkuru. Mito hii imeharibika na kwa hivyo, hakuna mawasiliano kati ya Kilwa na Ruangwa, jirani zetu. Ni nini mpango wa haraka wa Serikali kurudisha mawasiliano kwa kujenga Daraja la Mto Mbwemkuru ili tuweze kupata mawasiliano hayo pamoja na huduma za kijamii na za kiuchumi ziendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kilometa 17 kutoka Kiranjeranje mpaka Makangaga ni sehemu ambayo ina tija sana ya kiuchumi kwani ndio sehemu ambayo yanapatikana mawe ya gypsum kwa kiwango kikubwa sana hapa nchini. Ujenzi wa barabara hii ni wa kokoto zisizokuwa rafiki kwa magari yanayokwenda kuchukua madini haya ya gypsum. Je, ni nini

19 JUNI, 2024

mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, kilometa 17 hizi tunafanya maandalizi ya awali ya kujenga kwa kiwango cha lami, lakini tunaweka kifusi ambacho ni rafiki kwa wapitaji wa maeneo haya? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge ni kweli tunatambua eneo hilo ni muhimu sana sasa hivi katika biashara ya viwanda na hasa *cement*, ambapo *gypsum* inatoka eneo hilo. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumekusikia na naamini Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* pamoja na *Manager* wa Mkoa wa Lindi, hizi kilomita saba waende wakaone namna ya kufanya kuweka kifusi rafiki wakati Serikali inatafuta fedha ya kujenga eneo hilo aidha, kwa zege ama kwa kiwango cha lami, ili kutokukwamisha biashara kubwa ambayo najua tunatoa *material* ya muhimu sana katika eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, natambua kwamba, hakuna mawasiliano kati ya Kilwa na Ruangwa kwa sababu ya hiyo mito mitatu na ninajua kwamba, mpaka mto ambao wanapakana Mbunge na Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu hawawezi wakawasiliana. Mpango uliopo wa Serikali, moja ni kwamba, tayari tumeshatafuta fedha, kwa ajili ya kujenga Mto wa Mbwenkuru ambao hauwezi ukajengwa kirahisi kutokana na mvua iliyonyesha. Tayari fedha inatafutwa na Serikali kwa sababu, bado maji yapo mengi na hawawezi kuvuka, tunalitambua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha ambayo Serikali inatafuta, kwa ajili ya kurejesha miundombinu ni pamoja na hayo madaraja matatu ambayo Mkoa wa Lindi ndio ulioathirika kuliko Mikoa mingine yote katika Tanzania. Kwa hiyo, macho ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, inatafuta fedha na ninakuhakikishia yapo maelekezo mahususi kwa *TANROADS*, kwa maana ya Wizara, kutoka kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba, madaraja yote kwanza yatakuwa ni kipaumbele kuyajenga yawe ya kudumu ili tuweze kurejesha mawasiliano. Ahsante. (Makofi)

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago - Kizaga kilometa 71 toka umesainiwa una miezi nane, mpaka leo mkandarasi ame-*mobilize* hajalipwa *advance payment* hayupo *site*. Nini majibu ya Serikali kwa wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi na Iramba? Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli mkandarasi yupo *site* na taarifa nilizonazo ni kwamba tayari yupo kwenye hatua za mwisho kukamilisha *camp* (kambi) yeye pamoja na mhandisi mshauri. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bajeti ambayo tumeipitisha na kuanzia Julai tuna uhakika kwamba shughuli sasa zitaanza na mkandarasi atashika kasi kwa ajili ya kuanza kujenga hiyo Barabara ya Singida mpaka Kizaga. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, ni swali la Mheshimiwa Sylvia Fransis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum na kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Deus Sangu.

Na. 638

### **Kuwasaidia Wakulima Walioathirika na Mafuriko**

**MHE. DEUS C. SANGU K.n.y. MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, Serikali inawasaidia vipi wakulima ambao mazao yao yameharibiwa na mafuriko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.



19 JUNI, 2024

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapenda kuwapa pole waathirika wote wa mafuriko yaliyotokana na mvua za *El-Nino* zilizonyesha katika msimu wa mwaka 2023/2024 katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Mikoa ya Manyara, Morogoro, Pwani na Mbeya. Kufuatia athari hizo, Serikali imechukua hatua za haraka na za muda mfupi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kusaidia waathirika kwa kuwapatia msaada wa kibinadamu ikiwa ni pamoja na chakula. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, Serikali ilisambaza jumla ya tani 1,043.34 za mahindi ya chakula katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya awali ilionesha takribani ekari 75,594 za mazao ziliharibiwa katika mikoa iliyoathirika na mafuriko, ili kuwezesha wakulima katika maeneo hayo kuendelea na shughuli za kilimo, Serikali kwa kushirikiana na wadau imetoa msaada wa pembejeo ikijumuisha tani 70 za mbolea, tani 5.6 za mbegu bora za mahindi, maharage, ngano na alizeti. Maandalizi ya kusambaza mbegu za mahindi tani 748.4 na mpunga tani 449 yanaendelea kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya ya Kibiti na Rufiji kwa msimu wa 2024/2025. Serikali itaendelea kufuatilia hali ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na usalama wa chakula katika maeneo yote na kuchukua hatua stahiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika mafuriko haya yaliyotokea hasa Bonde la Ziwa Rukwa kuna skimu za umwagiliaji kama Skimu ya Tumaini Ng'ongo, Skimu ya Melepa, Skimu ya Sakalilo na Ilemba ziliharibiwa na ndiyo tegemeo kubwa kwa wananchi wa maeneo haya ya Bonde la Ziwa Rukwa. Nataka kupata *commitment* ya Serikali wana mpango gani wa kwenda kutengeneza skimu hizi za umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Bonde la Mto Ilemba katika Kata ya Mpuu ni bonde ambalo linategemewa sana na

19 JUNI, 2024

wakulima wa kata hiyo na wameathirika sana na mafuriko hayo na tayari wameshaenda kufanya upembuzi yakinifu. Ni lini Serikali italeta fedha kujenga Skimu katika bonde hilo la Mto Ilembo? Nakushukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba sisi kama Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tunafanya tathmini katika maeneo yote ambayo yameathirika zikiwemo Skimu za Milepa ambapo Mheshimiwa Mbunge anatokea na nimthibitishie tu kwamba tutarekebisha maeneo yote ambayo yameathirika ikiwemo katika jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha katika Bonde la Mto Ilemba ambako tunafanya tathmini, tukishamaliza tathmini tutangaza *tender* na baada ya hii kazi maana yake kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha ujao kazi itakuwa imeanza katika eneo lako. Kwa hiyo nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake kwamba tutaifanya kazi hiyo. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 639

### **Hitaji la Mwekezaji wa Kilimo cha Miwa na Kiwanda cha Sukari Mahenge – Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatafuta mwekezaji kwa ajili ya kilimo cha miwa na Kiwanda cha Sukari katika Kata ya Mahenge Wilayani Kilolo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Sukari Tanzania imefanya upembuzi wa awali ili kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha miwa na uwekezaji wa viwanda vya sukari katika Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa. Matokeo ya upembuzi huo yameonesha kuna jumla ya hekta 11,746 zinafaa kwa uwekezaji huo zikiwemo hekta 8,945 katika Kata ya Nyazwa na hekta 2,801 katika Kata ya Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazoendelea kutekelezwa ni upimaji wa maeneo hayo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na baada ya hapo maeneo hayo yatakuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya nchi iliyopo kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru Serikali kwa majibu mazuri, pamoja na hayo ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia TEMDO wanatengeneza mtambo wa kuchakata sukari ambapo tayari wameshatembelea Kata hiyo ya Mahenge na Nyanzwa na wameonesha nia ya kufunga mtambo huo kwa majaribio. Je, Wizara ya Kilimo ipo tayari kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili mtambo huo ufungwe Mahenge ili kiwanda kile kiweze kuanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa ulimaji wa miwa unaenda sambamba na Bwawa la Bonde la Nyanzwa ambalo usanifu wake umekamilika. Je, Serikali inatoa *commitment* gani kwa bajeti ya mwaka ujao bwawa lile kujengwa ili kilimo cha miwa kiweze kufanyika na kuunga mkono kile kiwanda cha sukari? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ni moja,

19 JUNI, 2024

sisi kama Wizara ya Kilimo tupo tayari kushirikiana na kufanya kazi na Wizara ya Viwanda na biashara ili kuhakikisha kwamba tunaongeza tija kwa wakulima hususani wa eneo la Kata ya Mhenge. Kwa hiyo jambo hilo tupo nalo tayari na tutafanya nao kazi kwa ukaribu. Kuhusu *commitment* ya Serikali kwenye Bwawa la Nyanzwa ambalo tayari usanifu wake umeshakamilika hatua ya sasa inayofuata ni kutangazwa kwa *tender* hiyo na baada ya hapo ni kwamba tutapata mkandarasi na mwisho tutamleta katika eneo husika ili aanze kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu kama Wizara ni kuhakikisha maeneo yote tutakayotangaza *tender* yatafunguliwa na tutahakikisha kwamba miradi hii inaanza kabla ya mwaka wa fedha ujao. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Asha Juma Abdullah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 640

### **Kuhamasisha Kilimo Hai**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje katika kuhamasisha kilimo hai kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chakula, nguo na vipodozi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hai ni mfumo ambao unazingatia usalama wa rasilimali za uzalishaji, hifadhi ya mazingira, afya ya walaji na kuongeza kipato. Hapa nchini, kilimo hai kinatumika katika uzalishaji wa mazao ikiwemo pamba, kahawa, kakao, chai na mazao ya bustani kulingana na mahitaji ya soko.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha kilimo hai kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya masoko mbalimbali Wizara inatekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo Ekolojia Hai wa mwaka 2023 – 2030; kusimamia mikataba ya kilimo hai katika mazao ya pamba, kahawa, kakao, chai na mazao ya bustani; kutoa elimu ya kilimo hai na hifadhi ya mazingira kwa wakulima kupitia mbinu mbalimbali ikiwemo mashamba darasa; na kufanya utafiti wa matumizi sahihi ya viuatilifu kwa lengo la kulinda ekolojia na kuwezesha kilimo endelevu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana hatua ya Serikali kwa kupitisha mkakati wa kilimo hai ekolojia wa mwaka 2023 mpaka 2030 hii ni *component* muhimu sana. Swali la kwanza; je, Serikali katika bajeti hii ya kilimo iliyosheheni fedha imetenga kiasi gani kwa ajili ya kuendeleza mkakati wa kilimo hai ekolojia ambao una mwelekeo wa kuwanufaisha wakulima wetu na kuwatajirisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, vipi lile dawati la kilimo hai kwenye Wizara bado lipo hai? Kwa isivyo bahati aliyekuwa anashughulika na dawati hili Mwenyezi Mungu alimpenda tangu hapo hatujasikia mwingine. Sasa kwa kuwa tunataka shughuli za kilimo hai ziendele, tunataka uhakika huyu mtu ameshakuwa-*replaced*? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetenga bajeti kwa ajili ya kusimamia kilimo hai na ukiangalia pale, tuna kifungu kabisa kime-*state amount* ambayo itatumika kwa ajili ya kusimamia zao hili ambayo siyo chini ya shilingi milioni 200 na

19 JUNI, 2024

katika moja ya mkakati mkubwa tulionao tumeiteua Bihawana kuwa moja ya *centre of excellence* kwa mazao haya ya kilimo hai ekolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawati, dawati lipo hai na tayari tumeshamteua msimamizi tarehe 6 Juni, 2024, tayari mtu ambaye anasimamia dawati la kilimo hai pale Wizarani amepatikana kupitia katika ule mkutano na nimthibitishie tumepata vilevile wawekezaji ambao wapo tayari kutu-support katika uendelezaji wa kilimo hai ekolojia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali la nyongeza kuhusu wakulima wale walioathirika na mafuriko, siyo Rufiji peke yake ambapo wakulima wa mpunga wameathirika na mafuriko. Swali langu, je, Serikali haioni haja ya kuwapatia mbegu na mbolea ya dharura wananchi wote (wakulima) wa maeneo yote yanayolima mpunga ambao wameathirika na mafuriko katika msimu ujao? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika ile tathmini tumeainisha watu wote ambao wameathirika wale ambao wanahitaji msaada kutoka Serikalini. Kwa mfano, katika maeneo ya Kibiti pamoja na Rufiji tayari tumeshadainisha na tunaendelea kuainisha na maeneo mengine yakiwemo katika jimbo lako. Kwa hiyo tutakapomaliza hiyo tathmini yetu maana yake na wenyewe tutawafikia kwa sababu miongoni mwa misaada tunayotoa ni pamoja na mbolea na mbegu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anataja hukuitaja Rukwa kwamba na wao wamefikiwa. Kata zote za pembezoni mwa

19 JUNI, 2024

mwambao wa Ziwa Tanganyika wamepata hiyo athari ya mafuriko. Kwa kuwa hawakuwa kwenye chanzo cha maji isipokuwa ni mabadiliko ya tabianchi. Ni lini na wao watafikiwa wapewe msaada huo? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilipokee swali la Mheshimiwa Mbunge ili tutume timu yetu ikafanye tathmini na kuona ukubwa wa tatizo na watu gani wanahitaji Serikali iweze kuwasaidia kwa sababu haya yapo katika mpango wetu na tunaweza kuyatekeleza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Kia na Kata ya Muungano ambao wanahudumiwa na Mto Johari walipata mafuriko na tunashukuru Serikali ilituletea chakula, lakini chanzo cha mafuriko yale kinasababishwa na kukosekana na ukuta unaozuia maji kwenda kwenye mashamba ya wananchi. Je, Serikali ipo tayari na ni lini itaenda kujenga ukuta ili kuzuia maji yasipande kwenye mashamba ya wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujenga lazima tufanye tathmini na sisi tutatuma timu yetu ya Tume ya Umwagiliaji ili waweze kufika katika hizo kata mbili ulizozitaja za Kia na Muungano na baada ya ile tathmini maana yake tutatafuta fedha ili tujenge tuweze kuwasaidia wananchi katika kipindi kinachofuata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Asia Abdugarimu Halamga, sasa aulize swali lake.

19 JUNI, 2024

Na. 641

## **Vitambulisho vya Taifa kwa Wafungwa na Mahabusu**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuwapa Vitambulisho vya Taifa wafungwa pamoja na mahabusu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdugarim Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kusajili na kutambua watu waliopo katika makundi maalum ikiwemo wafungwa na mahabusu ni kupitia maombi maalum kutoka kwa Wakuu wa Gereza katika wilaya husika. Uratibu wa usajili wa makundi hayo unafanywa na NIDA kupitia Wakuu wa Magereza na Maafisa Usajili wa Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya wafungwa na mahabusu wamekwisha kusajiliwa walipokuwa uraiani kabla ya vifungo vyao, Serikali kupitia NIDA ipo tayari kufanya usajili na utambuzi kwa watu wote waliokidhi vigezo ikiwemo wafungwa na mahabusu kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kuwa tayari kwenda kufanya utambuzi kwa kuwa suala la kupata Kitambulisho cha Taifa ni haki ya kila Mtanzania aliyekidhi vigezo. Je, ni lini sasa zoezi hili litaanza kwa kuwa wafungwa waliokaa kwa muda mrefu magereza wakitoka wanapata adha ya kupata huduma? Ahsante sana.



19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni haki ya msingi kila raia mwenye kigezo kupata Kitambulisho cha Taifa na ndiyo maana jibu la msingi tumesema *NIDA* ipo tayari kuwasajili wafungwa pamoja na mahabusu waliopo magerezani, lakini lini itaanza? Usajili huo utanza katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itawapa wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi Vitambulisho vya Taifa ambao wamepewa namba za *NIDA* tu kwa muda mrefu sasa na hawaelewi hatima ya kupata vitambulisho hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Mwezi Oktoba, 2023 tumetengeneza vitambulisho vya kutosha na niagize Msajili wa Halmashauri ya Arumeru kuhakikisha kwamba anavipeleka vitambulisho hivi kwa wananchi wote waliosajiliwa katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali.

19 JUNI, 2024

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo machache, kwanza tunayo matangazo yanayohusu wageni.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika, Mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Mwalimu Aida Mleli kutoka Shule ya Msingi *Katumba Two* iliyopo Tukuyu, Mkoa wa Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni Ndugu Balozi Kindamba, Mwenyekiti wa CCM Tawi la Amana; Mheshimiwa Ibrahim Mohammed, Mbunge wa Maldives na Ndugu Yesser Hassan, Mkurugenzi Mwendeshaji *Enviro-House*, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Wabunge wa Mkoa wa Iringa ambaye ni Mchungaji Origen Mpwage, Mkuu wa Jimbo la KKKT - Iringa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ambao ni wanafunzi wa *BBT* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ambao ni baba yake mzazi na mtoto wake kutoka Singida Kaskazini, karibu sana baba yetu na mwanetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Aziza Ally, ambao ni wafanyabiashara kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ambao ni vijana wa CCM kutoka Tarime Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, ambao ni Kundi la Wazalendo Huru kutoka Bagamoyo Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, ambao ni Viongozi wa Jukwaa la Wazalendo kutoka Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ambao ni Watendaji Kata wa Kata ya Ifakara Mjini, Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, ambao ni Walimu Wakuu wa Shule ya Msingi na vijana wa kutoka Jimbo la Arumeru Magharibi, Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wageni watatu kutoka *Ilazo Extension* Jijini Dodoma, karibuni sana kama wapo, ndiyo. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu kutoka *Tanzania Voice of Humanity* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 106 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya *St. Antony* ya Mbagala, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 75 na walimu sita kutoka *Libermann Primary School*, Dar es Salaam, karibuni sana kwa mafunzo Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo mengine, tunalo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga ambaye ni

19 JUNI, 2024

Mwenyekiti wa Bunge Bonanza, anaomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa Tamasha la *Grand Bunge Bonanza* litafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 22 Juni, 2024 katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma. Mgeni Rasmi wa tamasha hilo atakuwa Mheshimiwa Daktari Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Tamasha hilo kabambe litakuwa na ushindani mkubwa kati ya timu za Bunge na wadau katika michezo mitano kama ifuatavyo:-

- (i) Mpira wa miguu ni kati ya timu ya Bunge na Mahakama;
- (ii) Mpira wa pete kwa maana ya *netball* ni Bunge dhidi ya Baraza la Wawakilishi;
- (iii) Mchezo wa kuvuta kamba wanaume ni Bunge dhidi ya Hazina na kuvuta kamba wanawake ni Bunge dhidi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi;
- (iv) Mpira wa kikapu wanaume ni Bunge dhidi ya CRDB; na
- (v) Michezo mingine iliyobaki itashirikisha timu za Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge pekee. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, aidha mnakumbushwa kuwa jioni ya siku hiyo kutakuwa na tafrija kubwa itakayokuwa na burudani mbalimbali. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Bunge na wadau wote wanakaribishwa kushiriki kwa wingi katika bonanza hilo litakalodhaminiwa na Benki ya CRDB. *(Makofi)*

Katibu.

19 JUNI, 2024

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango  
wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025  
na  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa  
Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hoja za Serikali. Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na hoja ya Waziri wa Fedha. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Naomba niwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba hii bajeti tuiptishe kwa sababu nina miradi mingi huko Musoma Vijijini inasubiri fedha ikiwemo barabara yangu ya lami inasubiri fedha na mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji na wenyewe unasubiri fedha. Kitu cha pili ni lazima tuiunge mkono Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita sana kwenye uchumi. Uchumi wetu unakua kwa taratibu sana, sasa nitajaribu kueleza nini tufanye ili uchumi wetu uende kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchumi unakua kati ya kiwango cha asilimia 5.1 mpaka 5.5. Kipimo kingine cha ukuaji mdogo wa uchumi wetu ni, sijui Kiswahili chake *HDI (Human Development Index)* hii ndiyo inachukua kila kitu, mambo ya afya, elimu na kila kitu, Tanzania hatujafanya vizuri hapo. *HDI index* yetu ya mwaka 2022 ni 0.532, hii inatufanya tunakuwa nchi ya 167 kati ya nchi 193,

19 JUNI, 2024

ukilinganisha na Seychelles ambayo *HDI* yake ni 0.802, inakuwa ni nchi ya 67 duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu tulijiwekea kwenye mpango wetu wa maendeleo tufikie *GDP per capital* ya dola 3,000 na uchumi unapaswa kukua kwa asilimia nane mpaka 10%, lakini uko chini ya hapo. Ili twende mbele ni lazima tuangalie historia ya ukuaji wa uchumi wetu, nimechukua hapa takwimu kidogo ambazo zinajenga hoja ya kuharakisha ukuaji wa uchumi. Mwaka 1960, tulikuwa Watanganyika milioni 10, thamani ya dola kwa shilingi ilikuwa dola moja ilikuwa shilingi saba. Miaka 20 baadaye 1980, tulikuwa watu milioni 19, dola moja ilikuwa sawa na shilingi nane za Tanzania. Maana yake ni nini? Kwa miaka hiyo 20, Watanzania wameongezeka kwa 90%, lakini thamani yetu ya dola ongezeko lake lilikuwa karibu 14%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mwaka 2000, Watanzania tulikuwa milioni 34 na mwaka 2020 miaka 20 baadaye, tulikuwa watu milioni 62 lakini mwaka 2000 dola moja ilikuwa sawasawa na shilingi 800 za Tanzania na mwaka 2020 dola moja ilikuwa sawasawa na shilingi 2,320 za Tanzania. Maana yake ni nini? Ni kwamba, kwa hiyo miaka 20 Watanzania tumeongezeka kwa 82% lakini thamani yetu ya dola imepungua na imekuwa kiwango cha zaidi ya 190%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hali kama hiyo lazima tukubali kwamba uchumi wetu haujaenda kasi na nimechukua mifano, kila siku tunasema tuchukue nchi ambazo tulifanana miaka ya 1950 na 1960. Hapo nachukua India na China siyo nchi nyingi zaidi, kwa leo hii mwaka 2024 nchi tano tajiri kabisa duniani, Nchi ya ya kwanza ni USA, Nchi ya pili ni China. Kwa hiyo, China tuliyokuwa nayo sawa sawa miaka ya 1960, mwaka 2024 tayari imekuwa ya pili kwa ubora na kwa utajiri duniani na Nchi ya tatu ni Ujerumani, Nchi ya nne ni Japan na Nchi ya tano ambayo tulikuwa nao sawa sawa miaka ya 1950 na 1960, leo hii *GDP* ya India ni trilioni 3.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatayarisha dira ya maendeleo ya mwaka 2050, angalia nchi tano tajiri tukifika mwaka 2050. Nchi

19 JUNI, 2024

ya kwanza itakuwa ni China, itakuwa tayari imeitoa Marekani na itakuwa na *GDP* ya trilioni 58. Pili itakuwa ni US, Nchi ya tatu itakuwa India itakuwa na trilioni 22, Nchi ya nne itakuwa Indonesia na Nchi ya tano ni Ujerumani. Kwa hiyo, tunavyotengeneza dira yetu ya maendeleo ni lazima tuwekee hivi vitu maanani kwa nini wenzetu wametoka nyuma na leo hii wanaongoza dunia kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali letu kubwa, ili uchumi ukue kati ya asilimia nane na 10% tunapaswa tufanyaje? Kitu cha kwanza kabisa ni nchi hizo zenye mafanikio ni kwamba elimu yake ni bora kweli kweli. Maana yake ni kwamba, sijui nitaliwekaje kwa Kiingereza, ni *quality education and train at all levels*. Hicho ndiyo kitu cha kwanza kwa nchi zilizofanikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ni lazima ipatikane nishati ya uhakika na ya bei nafuu. Ukweli ni kwamba tulipiga mahesabu tukitaka kuwa nchi ya kipato cha kati, lazima tupate *megawatts* 10,000. Naomba tena hili nilisisitize ndugu zangu, umeme lazima tufike *megawatts* 10,000 kama tunataka kuwa nchi inayoendelea kwa haraka sana. Kwa zaidi ya miaka kumi vyanzo vya umeme ambavyo duniani vimezalishwa kwa wingi cha kwanza ni *solar*, cha pili ni upepo. Kwa hiyo, nadhani *energy mix* yetu tutaiweka vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha tatu ni lazima tuwe na bidhaa bora na nyingi za kupeleka kwenye soko la dunia, walengwa hapa ni wananchi wa dunia hii. Sasa hivi tuko bilioni nane, lakini 2025 ambapo tunatengeneza dira tutakuwa watu karibu bilioni 10. Sasa nini tupeleke sokoni huko na nini kifanye uchumi wetu uende kwa kasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ni kilimo cha umwagiliaji, hapa tutafute mazao au bidhaa ambayo inatumiwa na watu wengi duniani. Kwanza ni mchele ambao unatumiwa karibu na nusu ya dunia na uzalishaji kwa sasa ni tani milioni 524. Je, sisi hapo tunachangia kiasi gani? (Makofi)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ni ngano. Theluthi moja ya watu wa duniani wanatumia ngano kama chakula kikuu, uzalishaji ni tani milioni 785, lazima tuchangie huko. Viazi mviringo sasa hivi kimekuwa chakula cha tatu duniani na wanazalisha tani milioni tatu kwa mwaka na sisi tuzalishe. Baadaye mazao mengine ni mahindi, mihogo, maharage, soya beans, korosho na matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni ufugaji na uvuvi. Lazima tuwekeze huko kweli kweli, yaani hapa tuuze nyama, maziwa na samaki. Kwa mfano, sasa hivi uzalishaji wa maziwa duniani ni tani milioni 930. Je, sisi tunachangia kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha tatu kitakachofanya uchumi wetu ukue kwa kasi ni madini, lakini tusibaki na madini tuliyoazoea kila siku. Tuwasaidie wachimbaji wadogo lakini lazima tutafute uwekezaji mkubwa kabisa hasa kwenye hizi *critical minerals*, madini ambayo ni muhimu kabisa duniani yanayohitajika kwenye nishati, kwenye mambo yanayohusu vifaa vya ulinzi pamoja na mambo ya teknolojia ya sasa, soko hilo sasa hivi la *critical minerals* ni la dola bilioni 320 na litaongezeka mara mbili ikifika mwaka 2080, litaongezeka mara nne ikifika mwaka 2050. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kitakuza uchumi wetu, ni *natural gas* na *helium*. *Natural gas* tunazo zaidi ya TCF 57 trilioni hatujazifanyia kazi. Majadiliano ya LNG kama walivyoongea wengine lazima yaende kasi. Msumbiji waliokuwa nyuma yetu wameanza kuzalisha na kusafirisha LNG na wanaweka *plant* ya pili na *plant* ya tatu ya *total energies* itakayokuwa inasafirisha tani milioni 43 itaanza kazi mwakani. *Helium* ambayo inapatikana huko Rukwa, Lake Eyasi mpaka saizi tunakisia kuwa na kama bilioni 150 *cubic feet*, hatujafanyia chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kitakachotuongezea mapato ni utalii. Tunafanya vizuri lakini tuendeleo. Angalia Morocco mwaka jana walikuwa na wageni milioni 14.5, Egypt walikuwa na wageni milioni 15, sisi tulikuwa na milioni 1.8. Lazima tujiongeze uchumi ukue kwa kasi. (Makofi)



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha mwisho kwa ruhusa yako, dunia ya sasa hivi inapokea fedha kutoka nchi zingine yaani kuna *labour export* na *remittance*. Tutafute hizi Dola zinazopungua lazima vijana wetu wawe na sifa za kufanya kazi popote duniani ili walete fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naangalia hapa, India mwaka jana wameingiza bilioni 125, China bilioni 50, Nigeria bilioni 21, Egypt bilioni 24 na mahesabu ni kwamba kufika mwaka 2030 tutakuwa na upungufu wa wataalam milioni 80 duniani, tulenge hapo

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho la kustawisha uchumi wetu na uchumi kukua ni kuwa na *gold reserve*. Lazima tuwe na dhahabu Benki Kuu.China ambao wanachukua dhahabu yetu, sasa hivi wana tani 2,265, India wanaochukua dhahabu yetu wana tani 822 kwenye benki yao lakini sisi Tanzania bado tuna kilo 418. Naomba tujitahidi uchumi ukue kwa kasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatia Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu na Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, nimesoma hotuba yake anataka kuleta mabadiliko ya sheria ya sukari. Mimi ni mfanyabiashara na ninauza sukari. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na ningependa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi kama nchi hakuna tatizo kubadilisha sheria na ndiyo kazi ya Bunge. Suala la sukari ni suala kubwa sana na limekuwa na kelele nyingi sana karibu kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2019 wakati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo akiwa Tizeba na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara nadhani alikuwa Mwijage, wao walitoa sukari kwenye ma-godown kwa kutumia ma-SMG. Sasa nashauri sana, tunapoona kama suala hili linawakera wananchi na ni

19 JUNI, 2024

tatizo, ni vizuri tukabadilisha sheria ili haya masuala yakakaa vizuri na watu wakaacha kukaa kwenye *tension*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita hapa mimi ni mfanyabiashara wa sukari pia na ninaishi Mwanza. Ninataka kuzungumza tu kuhusiana na suala dogo la *cartel*. Kwa wale wanaotoka Kanda ya Ziwa sukari ilikuwa inauzwa kwa mtu mmoja tu. Ni kweli baadhi ya viwanda wanasema wana ma-*agent* lakini ni ma-*agent* bosheni, hawana sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kanda ya Ziwa (mimi nakaa Mwanza mjini katikati ya mji) watu walianza kwenda kupanga foleni saa 9.00 usiku na huyo aliyetajwa hapa *VH-SHAH* ambaye ndiye alikuwa *agent* mkubwa alikuwa na sukari imejaa kwenye ma-*godown*. Tunaona anashusha meli kila siku kutoka Kagera, lakini ili uuziwe sukari labda mifuko 50 inabidi ununue na *toilet paper* lazima ununue *toilet paper* au ununue biskuti. Sasa hii nchi ya wastaarabu hatuwezi kuwa na *design* hiyo ya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri zibadilishwe Sheria. Tumechoka kuona kila mwaka ukifika mwezi wa Januari, Februari na Machi tunaanza kupiga kelele ya sukari humu ndani haiwezekani. Misamaha inatolewa lakini matatizo ni yale yale, haiwezekani! Ukienda Zambia mpakani sukari inauzwa rahisi, ukienda Mutukula inauzwa rahisi. Sisi kwetu kila mwaka ikifika wa Januari, Februari na Machi kelele inaanza humu ndani Bungeni na wananchi wetu. Ninataka kusema ukweli, mimi natoka Jimbo la Geita Vijijini, wananchi wangu wa Izumacheli walinunua sukari shilingi 11,000 acha kusema 10,000 na ushahidi ninao. Sasa hatuwezi kuwa na nchi ya *design* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza sana Mheshimiwa alete hiyo Sheria hata kesho tubadilishe. Tunachotaka ni nafuu ya maisha ya Watanzania. Hatuwezi kung'ang'ana na sheria ambazo watu wetu wanakandamizwa. Inawezekanaje wewe unang'ang'ana na sheria halafu sheria imetungwa miaka 30? (Makofi)

19 JUNI, 2024

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunadhani tunataka kusaidia nchi hii ni vizuri tukaweka Sheria viwanda vyote vya sukari vitauzia NFRA halafu NFRA ndiyo ianze kusambaza. Leo Watanzania tumefika mahali pa kuweza kuepuka hili tatizo kubwa ambalo tunahangaika nalo la ku-*import* sukari tuamue kwamba tu-*import* sukari, tafsiri yake tunaua viwanda, tukiua viwanda halafu matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukweli tuzungumze ukweli tofauti na hapo maana yake ni kwamba tunarudi miaka 47 mahali tulipotoka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma unaipokea taarifa?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu na niwaombe Waheshimiwa kwa sababu kila mtu ana dakika 10 zake tujipange tu kuchangia tusipigane taarifa, nilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipi bora, kuwa na viwanda sawa kila mtu anataka kiwanda tunataka watu wetu wapate ajira, lakini tuwe na viwanda vya wanyonyaji ambao wanaweza kutengeneza kuipiga shoti Serikali halafu watu wakanunua sukari shilingi 10,000 pembeni hapa tu Mutukula, watu wananunua sukari 2,800 hivi ni viwanda au ni viwandani? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuwa na viwanda na ndiyo maana Bunge tunapitisha misamaha, lakini tunaowapa kufanya kazi ya viwanda na wao wawe waungwana. Haiwezekani tukawa tunasema tuwe na viwanda, kiwanda ambacho kinaweza kutengeneza shoti halafu kikauza kwa bei isiyotakiwa na Serikali imekaa kimya. Hii itakuwa siyo sahihi.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri leta Sheria tutaidadavua humu ndani tupitisha watu wapate nafuu ya sukari tupekane na hili janga a kupigizana kelele na sukari. Hata ukiwauliza watu wa kilimo, ukiwauliza watu mipango, hakuna mtu anayejua sukari inazalishwa kwa gharama gani kwa kilo hakuna hata moja. Waambieni wawape gharama ya kilo moja ya sukari wanatengeneza kwa shilingi ngapi? Hakuna mtu anayejua. Sasa hii ni Serikali, lazima ilinde watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tena wote wanatoka mMoja mmoja wa Singida. Niwaombe kuwasikiliza wafanyabiashara na kutatua matatizo yao ni jambo kubwa ambalo wataacha *legacy* kubwa sana. Nakumbuka mwaka jana tulianza kuwaambia humu suala la Kariakoo wakawa wanapiga chenga akiwa dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu. Kikaumana Mheshimiwa Waziri Mkuu akaenda akaokoa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu kila siku wanawaeleza na wamewaita kwenye Kamati wamewapa mapendekezo wanakwepa kuyatatua. Kuna ugumu gani kwa mfano wamewaeleza wanasema ukifika bandarini unaambiwa ulipe kodi 100 na kuna 100 nyingine ya mfukoni. Wao wako tayari kulipa hiyo 200 lakini iwe bei elekezi ya Serikali. Halafu Kariakoo nilishawaambia siku zote wafanyabiashara wengi ni darasa la saba hawajui mahesabu ya kodi. Kwa hiyo kodi unaenda kutegemea utakayemkuta leo yupo unalipa 50 kesho 100 na za mfukoni 100, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamewaomba na Kamati ya Bajeti wasikilizeni, wapo tayari kulipa lakini walipe kwa bei elekezi. Kama tunafuata viatu kontena ni 200 tulipe yote iingie Serikalini. Sasa haya majadiliano kila siku na Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ile akiwa pale, nilikuwepo, kuna makubaliano waliweka lakini hawataki kutimiza; wawasikilize wafanyabiashara. Leo hii sisi watu wa Tanzania tunafuata bidhaa Uganda, hawaoni aibu? Tunafuata bidhaa Kenya, hawaoni aibu? *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari inatumika ya Dar es Salaam kuchukua mizigo kupeleka Uganda halafu sisi tunaifuata Uganda kuileta Tanzania hii haiwezekani! Tumekosea wapi? Lazima waangalie, tukiiua Kariakoo tutakuja kushikana mashati humu ndani. Kariakoo ndiyo kila kitu kwa Tanzania, kwa hiyo ni vizuri tupalinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine waangalie namna Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kamata kamata Kariakoo ni nyingi mno. Hakuna mgeni anaenda kwenye nchi inayokamata. Ukinunua *t-shirt* una pini, ukinunua haka una pini. Mwisho wake watu wote wa Zambia sasa hivi wanenda Uganda sasa kweli haiwezekani. Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ile alieleza vizuri sana kwamba *operation* walitajwa mpaka mapolisi wakatajwa na nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita hapa *barrier* ukipita huku, kila mtu siku hizi mle ana tai. Sasa kwa kweli niwaombe sana tuiangalie Kariakoo tusije tukaipoteza tutapata hasara kubwa sana. Ni vizuri wawasikilize kama wana mambo yao wawasikilize wasiwanyime muda wa kuwasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusiana na suala la *spirit (ethanol)*. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni mchumi na kaka yangu Profesa tulikuwa tunakaa wote wakati akiwa huku nyuma, ana busara kubwa sana na bado namwamini. Sasa nataka niwaulize; sisi hapa wamesajili viwanda vya pombe hizi kali wamesajili wamevipa *certificate*, wamevipa leseni na vinalipa kodi nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, najua labda wanalenga kuzuia *fake*, lakini walichokilenga ni kuua hii biashara. Haiwezekani Mheshimiwa Dkt. Mwigulu mchumi, dokta mwenzangu pipa moja la *ethanol* kulitoa nje kulileta hapa linagharimu shilingi 600,000, ukilipa na ushuru ilikuwa shilingi 200,000 na gharama zingine inakuwa shilingi 1,000,000. Leo wewe ushuru kabla ya kununua umeweka shilingi 2,000,000. Sasa pipa lililokuwa linauzwa shilingi 1,100,000 likauzwe shilingi 3,500,000 huo

19 JUNI, 2024

uchumi wa *design* gani? Maana yake wanataka watu wafunge viwanda, waliwapa leseni za nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama kila siku anahamasisha watu wafungue viwanda wanawapa leseni, wanawapa vibali wakishakopa hela ya benki wanaingia tena na Sheria mpya; haiwezekani! Nimwambie Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Waziri Profesa Mkumbo tuwe hai. Watoto hawa baada ya kufunga hivi viwanda vya pombe watarudi kwenye ugoro na madawa ya kulevywa hakuna starehe nyingine. Sasa hata konyagi haitatengenezwa, hakuna *K-vant*, hakuna kila kitu. Ni lazima wakae warudi waangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu akatoa ushuru wa shilingi 220,000 akapeleka 2,200,000. Hii ni biashara gani jamani au labda *calculator* zinakuwa zinaenda mbele na nyuma? Ninadhani tuwe makini sana tunapoamua kubadilisha. Hawa watu walishaingia kwenye mfumo wa biashara na walishakopa hela za benki halafu unam-*disturb* tena. Wataua wafanyabiashara halafu kila siku wanahamasisha suala la wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nipo kwenye Kamati ya Nishati. Tulitembelea viwanda vya gesi ya magari. Kwanza tu kutengeneza ule mfumo wa gesi kwenye gari inaenda karibu shilingi 2,000,000 halafu vituo vyenyewe vya ku-*refuel* gasi ni viwili peke yake. Kituo cha Ubungo pale Urafiki mtu anaenda saa 8.00 usiku anapata huduma saa 7.00 mchana. Tulifika pale Kamati watu wanasema sisi hatutaki kuwaona Waheshimiwa Wabunge foleni imeshatuweka hapa mpaka gari za watoto anakwambia nimekuja sasa 7.00 usiku mpaka saa 5.00 asubuhi tunaenda pale, bado anasubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Serikali vituo viwili kingine *Airport*. Tukiwa kwenye hii hali ya kubembeleza watu warudi kwenye hiyo biashara ya kutumia gesi unaongeza tena ushuru jamani? Nilidhani Serikali itatoa *subsidies* kupunguza bei badala yake tena unataka kukusanya shilingi bilioni tisa kwenye gari 3,000; kweli hatuna chanzo kingine? Ni vizuri tusifanye bajeti ya ku-copy

19 JUNI, 2024

na ku-paste, ni vizuri waumize vichwa. Serikali inawalipa pesa waumize vichwa kutafuta vyanzo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirundika kila siku vitu kwa watu inaleta chuki kubwa sana kwenye Serikali. Nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Profesa Mkumbo suala la mashudu na bahati nzuri na mwenzangu jana alizungumza. Mashudu yanaangukia Singida na tunaenda kwenye uchaguzi. Mashudu ya alizeti yapo Singida peke yake, ukiyawekea ushuru hiyo *withholding tax* watu hawatayanunua. Kwa hiyo watu Wanyiramba pale watayalalia kitandani au yataenda wapi? Kwa sababu ng'ombe zinafuata majani sisi hatuna mfumo wa kulisha mashudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekanaje tunakuza kilimo, tumeua pamba, tumekuja kwenye alizeti ndiyo inaanza ku-grow tena wewe unaiwekea makorokoro jamani? Nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunamtakia kazi njema na wewe na Mheshimiwa Profesa Mkumbo, lakini waumize vichwa kutafuta vyanzo vya mapato tusifanye bajeti ya ku-copy na ku-paste. Ni vizuri sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na bahati nzuri siku ile kwa mfano Kariakoo tulikuwa wote uliona mtiti ulivyokuwa sasa wa *term* hii ukiamka sijui nani ataenda kwa sababu tulitoa maelekezo hatujayatekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri watu wanalalamika wamemwomba punguza, sasa unaenda unaambiwa unalipa *service levy* halmashauri halafu ukimaliza *service levy* unakuja hela ya taka, hela ya kwenda kujisaidia na hela ya kupaki. Sasa *service levy* gani tunawachukulia watu hela? Ni vizuri Serikali tuamue kama tunaenda kutafuta vyanzo vipya tuumize kichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kuna jambo la kukumbushana. Wakati Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma anachangia Mheshimiwa Mathayo Manyinyi alimpa taarifa lakini Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma alipotakiwa

19 JUNI, 2024

kupokea au kutopokea taarifa hiyo alionyesha kutoridhika na utaratibu wa kupewa taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe kwamba utaratibu wa kupewa taarifa upo kwenye Kanuni zetu za Kudumu za Bunge Kanuni ya 77. Mheshimiwa Mbunge unapopewa taarifa unayo mambo mawili tu ya kufanya au unapokea taarifa au unakataa kupokea taarifa. Naomba niweke huo msisitizo ili kutonyima haki za Waheshimiwa Wabunge kutoa taarifa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, anayefuatia kuchangia sasa ni Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema yeye ambaye ametupa uzima kwa siku ya leo kuwepo katika Bunge hili. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya kuendelea kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Fedha ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa kuwasilisha bajeti hii ambayo ni bajeti ya matumaini kwa wananchi wa Tanzania. Nianze tu kwa maeneo kadhaa nikianza na eneo la suala la makusanyo ya Serikali. Katika makusanyo ya Serikali tunakusanya fedha ndiyo, lakini bado hatujaweza kufikia katika kiwango kile ambacho kinatakiwa kwa ajili ya kukidhi nakisi ya bajeti ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika ukiangalia hakuna mwaka ambao tumeweza kufika tukaweza kuvuka yale malengo ya bajeti ambayo tumeweka. Kwa hivyo suala hili linahitaji umakini na umahiri wa hali ya juu na kwa jinsi ambavyo namfahamu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na kazi zake na timu yake ni lazima wahakikishe sasa kwamba wanafikia



19 JUNI, 2024

bajeti hiyo waweze kuikusanya kwa kiwango ambacho bajeti inatakiwa kama Bunge ambavyo tunakwenda kupitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukusanya mapato kuna changamoto nyingi ambazo zinaikabili Wizara hii, kwa mfano suala la rushwa. Rushwa katika kukusanya mapato kwa baadhi ya watumishi (siyo wote) wanafanya *bargain* kwamba wewe lipa labda shilingi bilioni 15 ndiyo kodi yako, lakini baada ya hapo yule mfanyabiashara atakapokuwa analalamika, basi inarudi kwamba wanaenda kupatana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupatana wanarudi kwenye makubaliano fulani kwamba sasa wewe lipa shilingi milioni tano lakini unipe shilingi bilioni 10 ije kwangu. Ninayasema haya siyo kwamba ni suala ambalo siyo ukweli kwa sababu siyo baadhi ya watumishi wanaofanya hiyo kazi, lakini wachache ambao hawaitakii Tanzania mema, wachache ambao hawaitakii Wizara hii mema wanafanya hivyo. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ana kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba Wizara yako hiyo katika kukusanya fedha za umma kunakuwepo na uadilifu na uaminifu wa hali ya juu ili mwisho wa siku tupate watumishi ambao wanaweza kuwa waadilifu zaidi japo wengi wanafanya kazi yao vizuri, lakini kuna baadhi ya wachache ambao wanaharibu ile taswira ya TRA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ningepomba kuishauri Wizara hii Sheria ya suala la kujadiliana kwamba ulipe kodi ya kiasi fulani. Ninadhani hii Sheria Mheshimiwa Waziri wangeendelea kuiangalia namna ya kuiboresha zaidi. Suala la kukaa mezani au mtu kukaa kukadiria kodi inasababisha rushwa zaidi. Kwa sababu kama ingekuwa kuna *fixed* kwamba mtu ana biashara fulani Sheria ndiyo inatamka wazi siyo mtu anakisia, ninaamini tungepunguza suala la rushwa na tungekusanya fedha nyingi sana kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kutofikia kiwango hicho ni kwamba hatutaweza kutimiza miradi yetu ya maendeleo...

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## **TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza nakubaliana naye kwamba Sheria yoyote ambayo inatoa hiyari ya afisa yeyote wa Serikali au TRA ku-*negotiate* ile kiasi cha kodi, basi hiyo Sheria itakuwa ina matatizo makubwa kwa sababu inakaribisha rushwa; yaani kama Sheria inapanga kwamba atoe kati ya 10,000 au 30,000. Kama ni *cutting* iseme tu kama ni 30,000, iwe 30,000 basi na kama ni 20,000 iwe 20,000 basi, siyo ku-*negotiate*. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Noah unapokea taarifa ya Mheshimiwa?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na ndiyo madhumuni hasa ya kusema hilo eneo ndilo linalosababisha kutokukusanywa kwa mapato ya Serikali kwa sehemu kubwa. Pia ndiyo inayosababisha hata TRA kushindwa kufikia malengo na Serikali kufikia malengo ya kukusanya fedha ili kwenda kuhudumia miradi ya maji, miradi ya kimkakati kwa maana ya Bwawa la Nyerere na miradi mingine yote ile ambayo inatakiwa Wizara ipeleke fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Sheria hii tunaweza tukaibadilisha naomba sana iletwe hapa Bungeni tuiweke vizuri, wataalam wakae ili basi tuhakikishe kwamba tunakuwa na Sheria ambayo haina ukakasi wa kuendelea kutoa mwanya wa rushwa ili basi wale wala rushwa wasiendelee kuhujumu nchi yetu na kuhujumu hii miradi ambayo tungetegemea kwamba iweze kupelekwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kwa mara pia kila ripoti inayokuja ya CAG kunakuwepo na masuala ya madudu ya udokozi udokozi na ulaji ulaji. Hii inatokana na nini? Inatokana na watumishi pia ambao siyo waadilifu na watumishi ambao hawafikiri kuhusu uzalendo wa nchi hii kwamba wananchi hawana maji, wananchi hawana barabara, mafuriko

19 JUNI, 2024

yametuvamia barabara zimeharibika na mambo mengi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie suala hili kwa sababu tusipofikia mahali pa kuweza kuwasimamia watumishi wakaweza kuhakikisha kwamba wanakusanya mapato kwa ukamilifu na uadilifu mkubwa, kila mwaka Taarifa ya CAG itakuja hapa na tutakuwa kwenye mazingira magumu ya kutokuwa na aibu ya kila mwaka kuna ufisadi, rushwa, mambo ambayo hayafai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Waziri ajitahidi kujitathmini kwenye Wizara yake, Waziri wa Fedha, sijui Waziri wa Maji, kama kuna vitu vyovyote ambavyo vinatokea kwenye Wizara zao wajitahidi na ninaona wanajitahidi kweli, lakini waongeze juhudi na wale watu wote walioko chini yao wahakikishe kwamba wanafanya kazi vizuri kwa uaminifu na uadilifu ili bajeti hii ambayo tunaenda kuipitisha ikapate kuzaa matunda na ikapate kuwa na matumaini makubwa kwa wananchi Watanzania na kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais kufikisha malengo yake ya kuwahudumia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama ambavyo anajitahidi kwenda huku na huko kutafuta fedha na sisi tunakuja kuneemeka huku. Kama suala la makusanyo likisimamiwa vizuri naamini nchi yetu itakwenda mbali na itasonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misamaha ya kodi; nilipokuwa napitia ripoti kuna misamaha mingi ya kodi ambayo inafanyika, lakini hatuangalii sana maslahi makubwa ya Taifa. Niombe kwa wale wahusika, misamaha ya kodi ilenge katika kuhakikisha kwamba ina tija kwa Taifa na inaleta matumaini kwa wananchi. Wasisamehe kodi bila utaratibu kwa sababu tukisamehe kodi bila kuangalia uchumi wa nchi yetu, bila kuangalia Serikali inanufaika na nini, ninaamini hapa tutakuwa tunahujumu Taifa, tutakuwa tunahujumu wananchi wa Tanzania, tutakuwa tunafanya jambo ambalo ni kinyume na nafasi zetu ambazo tumepewa. Naomba sana tuhakikishe kwamba tunaacha kutoa misamaha ya kodi isiyokuwa na utaratibu.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ukosefu wa watumishi *TRA*; watumishi ni wachache *TRA* na kwenye taasisi zingine za fedha ambazo zinakusanya fedha. Suala lingine ambalo linaikumba *TRA*, *TRA* ni miongoni mwa taasisi ambazo zinatajwa katika tafiti mbalimbali, nenda kasome, inaonekana ni miongoni mwa taasisi ambazo zinaongoza kwa rushwa na rushwa yenyewe inatokana na suala la kujaribu kufanya ajira, ajira ya *TRA* ni changamoto sana kwa wananchi wengine wa kawaida kupata. Kwa nini ajira za *TRA* zisirudishwe kwenye utumishi ili utumishi ndio uwe unasimamia kwa sababu matumaini makubwa ya Watanzania yako kwenye Wizara ya Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ili tupate watumishi waadilifu, *TRA* na Benki Kuu ni ajira ambazo haziko wazi, ziwekwe wazi ili wananchi wote Watanzania waombe na waweze kufanikiwa kwa sababu bila kufanya hivyo ina maana kutakuwepo na ubaguzi na hapo ndipo ambapo tunakwenda kukidhi matakwa ya *nepotism* katika kutowapa wananchi wetu usawa katika kupata ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niombe kumaliza kwa kusema, ninajua Wizara ya Fedha na Wizara zote wana kazi kubwa ya kutekeleza bajeti hii, sasa ni jukumu letu sisi wote kuungana kwa pamoja tukiwemo sisi Wabunge na ninyi Waheshimiwa Mawaziri na Makatibu Wakuu na wote wanaohusika katika kutekeleza bajeti hii kuhakikisha kwamba tunakwenda kutekeleza bajeti hii kwa kiwango ambacho kinatakiwa kwa kupeleka fedha, kwa kuwapa makandarasi fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ili kuepuka suala la kutowapa makandarasi fedha ambapo baadaye zinatokea zile *penalty* ambazo inakuwa ni gharama kubwa kuja kuwalipa makandarasi kwa sababu hatukuweza kulipa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Serikali inajitahidi kwa kiwango ambacho imeweza na bado tunaona jitihada zao kubwa wanazozifanya, basi naomba waendeleo kuongeza jitihada na juhudi kubwa katika kuhakikisha kwamba shughuli hizo zinakwenda vizuri na nina imani na wao, tuna imani na Serikali ya

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na tuna imani na wote ambao wamepewa madaraka na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, atafuatia Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Grace Victor Tendega ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya, lakini niwashukuru na Wabunge wenzangu sasa hivi naona wako wazima na wana afya kabisa katika viti vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mawaziri wangu, Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa wanazozifanya katika Wizara zao na leo hii wapo hapa tunawapitishia bajeti zao. Kwa hiyo, kuna masuala ambayo tutaweza kuyachangia na wao wakayachukua wakaweza kuyafanyia kazi, kwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nina suala hili la bandari na mizigo, hasa kwa wajasiriamali. Suala hili tunalizungumzia sana humu katika Bunge hili Tukufu lakini bado lina kadhia yake halijakaa sawa. Leo kama ya nne au ya tano nitasema, kuna jamaa yangu mmoja kapitisha mzigo mdogo tu mpaka kunipigia mimi huku akiniambia kwamba nina mzigo wangu, lakini watu wamenikamata na hasa watu wa TRA pamoja na watu wa Uchukuzi. Kwa maana hiyo Uchukuzi na TRA wanashirikiana na imebidi atoe pesa kwa hali yoyote ile ili ule mzigo upate kupita uingie katika boti uende zake Zanzibar, je, Serikali inalizingatia vipi suala kama hili na tukizingatia sisi ni watu wa muungano? Mwenye mzigo mdogo aachiwe apite akafanye shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kama mzigo mdogo mtu akimwona mjasiriamali kama yule mwanamama, hali yake duni

19 JUNI, 2024

hana kitu, katupa nauli yake kutoka Zanzibar kaja Dar, kaja kutafuta mzigo wake unakwenda zake kule Zanzibar. Matokeo yake leo hii anafanyiwa kadhia kama hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango hili suala walichukue na wakalifanyie kazi na hili suala tusije tukaliona tena katika bandari ile kwa sababu wanatukera sana hasa sisi watu wa Zanzibar na wakati sisi ni watu wa Muungano, tunaomba hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili, nazungumzia kuhusu suala la ndege, suala la utoaji wa tiketi za ndege kupandishwa nauli kila wakati, ukienda leo unakuta pesa nyingine, ukienda siku nyingine unakuta pesa nyingine. Kwa hiyo, hili suala nalo linaumiza, bado hatujawa na mustakabali mzima wa Taifa letu ambapo tukienda kwenye ndege tunakuta shilingi 260,000 ama shilingi 350,000 kila siku tunapandishiwa nauli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili la nauli nalo naomba walifanyie kazi, kwa sababu mataifa ya wenzetu wa nje wao wana punguzo katika ndege zao, je, itakuwa sisi hapa Tanzania, ukizingatia kuwa ndege zetu zipo na hizi tunasema ndege zetu wenyewe. Hebu watufanyie wepesi wa hizi ndege kwa sababu na mabasi nayo wakati mwingine ukizingatia watu wazima hawawezi kuyapanda migongo inawauma, mwili wote hata akifika Dar es Salaam wa maji. Kwa hiyo, watufanyie wepesi katika nauli hizi za ndege. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alifanyie kazi suala hili ili twende sambamba tuweze kupanda ndege kwa murua bila wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, ni kuhusu huu mpango wa unyanyasaji. Juzi tu hapa tulizungumzia mpango huu wa unyanyasaji katika Wizara ya Maendeleo, lakini tunazungumzia lile kumbe sisi tunapiga kelele kule wanatuambia mtakoma. Hapo hapo watoto wetu wananyanyaswa, walimu wanawanyanyasa watoto, kweli ni vizuri? Ustadhi mzima kanyanyasa watoto juzi tu hapa na nikasema hawa watu wahasiwe, jamani sheria iletwe Bungeni haraka kwa Wizara hii ya Mipango, Wizara hii ya Fedha, sheria iletwe hapa Bungeni haraka tuifanyie kazi ili hawa watu wanaowafanyia vitendo viovu

19 JUNI, 2024

wahasiwe. Mimi nasema tena wahasiwe ili hii kadhia wanayowafanyia watoto wetu kwa makusudi kwa kuwabaka na kuwafanyia vitendo vibaya hivi wanavyotaka sio vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mbunge mmoja pale kalia machozi ule unyanyasaji, mtoto kakatwa viungo kisha wamemwacha, wamechukua viungo vyao wameenda zao, kweli vile hii ni haki? Mtu kama yule mnamfunga maisha hatoki mpaka anakufa huko huko. Hili linakuwa sheria ipitishwe hapa vilevile, suala hili linatuuma na lifanyiwe kazi katika hizi Wizara zao. Hii Wizara ya Maendeleo waiongezee kipato ili na wao waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu kipato chao wanachoingiziwa ni kidogo. Kwa hiyo, waongezewe kipato ili waweze kufanya kazi vizuri, watu wazima humu na akili zao hawana adabu wanabakabaka tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza nazungumzia suala la askari jamii katika nchi yetu kila mahali pana askari jamii. Wengine wanakubali kabisa kutumwa na wanatumikia vizuri na ukienda katika kijiji kimojawapo unakikuta kijiji kimetulia na kinafanya kazi vizuri hasa kijiji chetu cha Wilaya ya Kusini, Kijiji cha Kizimkazi, kwetu mimi nilikozaliwa, askari jamii wamepangwa vizuri na wanafanya kazi vizuri, kule hakuna uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hao askari jamii na wao wafanyiwe kazi ili waweze kufanya kazi vizuri wasiwe nyuma, tuwe nao watulinde usiku na mchana ili angalau sisi watu wazima tuweze kulala. Maana wewe unaingia ndani unalala huna raha, hujui nani ataingia ndani ya nyumba yako. Kwa hiyo, hawa askari jamii nao pia kwa Wizara hii ya Mipango na Wizara ya Fedha na wao wafanyiwe kazi ili waweze kufanya kazi vizuri, kama ni kuhusu suala la michezo, wafanye michezo vizuri, kama suala la kwamba mmoja mmoja mle anaweza akatolewa akawa yeye ni askari kabisa kutokana na juhudi zao wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, atafuatia Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Grace Victor Tendega ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Kabla sijaanza nina mambo mawili niyaseme, amemaliza kuongea Mheshimiwa Mbunge aliyechangia na jana yamezungumziwa. Hayo majanga mnayoyasikia yamenipata mimi, Asimwe aliyekatwa miguu tunatoka kata moja, lakini huyo ni Asimwe, kwetu kwenye Kisiwa cha Uchumi Gozba, vijana wamechukuliwa na watu wanaojulikana mmoja wakampiga na wakamtosa kwenye maji. Ninaiomba Serikali na nilifarijika nilipomwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, watendaji walioko Wilayani Muleba na Kagera waongezewe nguvu, hayo Wabunge wanayoyasema, watendaji walioko kule wanahitaji nguvu za ziada na wataalamu wa intelijensia kusudi watu wapate haki yao hapa duniani, siwezi kuzungumza zaidi litaniumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ninapopigana kujenga upya Rutoro nina matatizo mawili, Mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga umeme Rutoro hafanyi kazi, inaniletea shida na tatizo lingine Rutoro, kuna watu wanakiuka tamko la Serikali pale ambapo Mheshimiwa Rais alisema wawe wafugaji na huku wawe wakulima. Sasa kwa wakulima kuna watu wanakiuka maelekezo ya Mheshimiwa Rais, wanapeleka ng'ombe kule. Ninashukuru Mheshimiwa Fatma akiwa Hijja Makkah ameniambia ngoja arudi na maji ya zamzam atawafukuzia mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihutubie Taifa, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri kwa hotuba zao na nitaanza na Waziri wa Mipango, anasema kupanga ni jambo moja na kutekeleza ni jambo lingine. Sisi tumeamua kutekeleza, tumezipitia bajeti za kisekta tumezimaliza, sasa tunakuja kuwapa baraka kusudi tutekeleze. Angalizo langu kwa Serikali, hii dhana ambayo wanataka kuipigania sana, dhana ya *KPI (Key Performance Indicator)* ni suala la kawaida, lipo, lakini inaonekana katika Mpango huu wa 2024/2025 wanataka kuliwekea nguvu zaidi kwamba tuwe tuna vipaumbele, sawa tunavijua, tuwe na



19 JUNI, 2024

nidhamu ya utekelezaji, tumekuwa tukisikia viongozi na sisi tunasema lazima tuwe na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu kabla Waziri hajam-*task* meneja kufanya hivyo lazima ampe mamlaka. Meneja ambaye hana mamlaka akimwajibisha anamwonea, ayajue majukumu yake, lakini ampe rasilimali, atamwambiaje mtu atengeneze mradi aumalize kabla hajampa pesa *on time*, lakini atamwambiaje meneja atekeleze mradi aumalize wakati cheti alichonacho ni *fake*? Kwa hiyo, inaanzia hapo, lazima ajue hizo *KPI* anazitekelezaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachotofautina kitu kingine, lazima wafanye kitu kinaitwa *TQM (Total Quality Management)*. Wasisubiri mwisho wa mwaka kuja kutupa matokeo, waende wana-*monitor* na yule atakayeshindwa apishe kando kusudi wengine waweze kuendelea na kazi. Kinyume cha hapo nakubaliana na dhana hiyo na kimsingi iliasisiwa hapa Tanzania ikaenda kutekelezwa kwenye nchi nyingine tunabaki kusoma kwenye makaratasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze mambo 10 yatakayopewa kipaumbele au msukumo. Waziri wa Mipango anasema na tumeliona kwenye sekta kwamba ni kuendeleza kuwekeza katika kukuza uzalishaji kwa Sekta ya Kilimo na kuendelea kuweka uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Ninachoshauri Sekta ya Kilimo ichukue tafsiri asilia, tafsiri asilia ya kilimo ni *crops, animal husbandry, livestock, pottery, aquaculture, pisciculture na forest*, haya yote yanakwenda pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza na nilizungumza waziwazi kwamba hapa tukipachukua vizuri tunaweza kupata pato kwenye sehemu hizi inayofikia dola bilioni 12 za kuagiza nje bila kusahau kwamba hiki kilimo kwa mapana yake ndiyo kinatuwezesha kuwalisha Watanzania au kupata chakula mwaka mzima na tukaweza ku-*export* nje. Profesa nakuelekeza taratibu, unajua kama unatamani kwenda kusoma *Ph.D*, lazima Profesa amshughulikie taratibu, anaweza akalipiza, lakini tukiyasikiliza vizuri

19 JUNI, 2024

na hizo *KPI* hapa kuna uhakika wa kupata dola bilioni 12 na nilizungumza kwenye bajeti za kisékta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mkazo katika maendeleo vijijini na nimefurahishwa na matamko ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango anasema anakwenda kukazia ujenzi au uhamasishaji wa viwanda vidogo vidogo. Ninawaomba Watanzania wasahau vyerehani, nyie katika viwanda vidogovidogo vyerehani ondoka, kwa sababu watu wengi unyanyapaa wao ni pale vyerehani kwamba ni viwanda, lakini niwaambie viwanda vidogo ni shule, huwezi kutoka hapa hujawahi kumiliki kiwanda ukapata kiwanda cha shilingi bilioni kumi ukakiendesha, haiwezekani ni utamaduni, *it is a culture*. Kwa hiyo, tunapokwenda kujenga viwanda vidogo vijijini maana yake tunajenga utamaduni wa watu wetu miaka ijayo waweze kuwa na utamaduni wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; tunapojenga viwanda vidogo vijijini tunawa-retain wananchi vijijini na kupunguza tabia ya watu kuhamia mijini. Profesa Ndulu alisema kwamba, kijijini ukishaweka umeme, ukaweka barabara za *TARURA* panapendeka, *lovable* na pakishakuwa *lovable* panakuwa *livable*. Vitu vizuri viko vijijini, *TARURA* ameshafika, shule zimeshafika, *VETA* zimefika unakuja mjini kutafuta nini, ugongwe na gari? Kwa hiyo, naomba tuweke viwanda mambo yote yaweze kuishia vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu *NEDF*; Profesa amezungumza suala la kuijenga upya *SIDO* nakubali na niwaambie wakijenga *SIDO* vizuri kama nilivyoiacha wakaanzisha *NEDF* kama nilivyoiacha, mifuko yote itakwisha. Tofauti ya *NEDF* na mifuko mingine ni kwamba *SIDO* wanakupa pesa baada ya kukufundisha, unapohitimu wanakupa kiwanda. Ndio maana wakati ule tulianzisha *industrial area* wilaya zote, Mheshimiwa Mageza akiwa *District Commissioner* anakumbuka nilimpa saa 24 aanzishe *industrial area* akaianzisha. Kwa hiyo, lazima turudi kule wasione tatizo kutazamia, ule mwendo ulikuwa mzuri. (*Makofi*)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tozo kwenye gesi ya magari, tumekosea. Mheshimiwa Waziri, *Omwana wa umukazi Mwigulu*, anisikilize. Kwa nini anaweka pesa kwenye gesi? Kwa nini gesi? Watu wengi hawataki kuzungumza. Sisi kwetu gesi ni kinga, usalama na kwamba, endapo kuna tatizo kwenye ugavi sisi tutabaki salama. *In case of disruption in supplies in the gas, we will be safe here.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa dawa ni kuhimiza Watanzania wawape gesi nyingi, wawape kichocheo, ili kusudi moja, tuwe salama kwenye vyombo vya usafiri. Pili, itakapotokea tatizo tutakuwa hatuna tatizo. Hata hivyo, wanapotafuta pesa mbona wanaziacha zinapita? Malori yote yanayopita hapa yanalipa ushuru au tozo? Kuna magari yanapakia mafuta Zambia yanakwenda kushusha mzigo Mombasa yanaharibu barabara za Bashungwa, kuna mengine yanatoka Rwanda, hawajui kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu haelewi nije nimweleze. namwomba Mheshimiwa Waziri alete wataalam wake nimweleze. Magari ni 400 na kama gesi ni nzuri, niliwaambia Mwaka 2023, ya Serikali ni mangapi? Juzi nimeona *Prado* tena namba A, Prado la namba TZA ndiyo linakuja limewekewa mtungi wa gesi, kwa nini hawakuweka kwenye hizi VXR? Kwa hiyo, namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, hapo tumekosea. Hiyo shilingi 300 waiondoe, watu wote waingie tuwe salama na tatizo la mafuta, tukishakuwa salama tutajiweka taratibu. Nahitaji muda nimwoneshe pesa zilipo. Magari ya nje yanayopita hapa hayatupi mafuta hapa Tanzania na hatuna lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine ni kusaidia kuweka mazingira mazuri ya biashara, iko kwenye mpango. Ngoja niwaambie, kila *export* iwe *formalized*. Kuna watu wanatoka huko watokako wanaleta mitumba hapa, wanaipiga pasi, wanawapa ndugu zetu wakulima, wanawapa mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawaambia tuna *potential export* ya mchele. Waziri wa Kilimo ameonesha mchele umekwenda juu hata kuliko kahawa. Sasa a-*formalize* pia, ili a-*formalize* wawawekee mazingira mazuri wakulima wa mpunga.

19 JUNI, 2024

Wasiwawekee *withholding tax*, wawapetipeti, wawawekee *magodown* kusudi mchele unapoondoka, wao wanaandika *documents* tunapata *revenue* inaingia ndani. Hata hivyo, wakiweka *withholding tax* mchele utahama saa 9.00 usiku na hawatakuwa na la kufanya na kwanza hawatauona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe. Baada ya kuona kahawa inaondoka alikuja kutaka ushauri kwangu, nikamwambia akatafute ng'ombe wa maziwa awape walima kahawa, wanaotaka kuuza kahawa kwake wakalipe deni kwa maziwa, waweke mbolea kwenye mibuni halafu mibuni wamuuzie kwenye kahawa. Karagwe na Bukoba *KDCU* na *KCU* wamekubaliana na Bashe hakuna kahawa itakayovuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natengeneza upande huu, naharibu upande ule. Tanzania kunapendeza, sasa mjomba itabidi alie kwa sababu, kahawa ya Tanzania hataipata. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri asitumie nguvu, atengeneze mazingira mazuri ya biashara, *the easier of doing business, the blueprint*, wakisome kile kitabu. asipende ganda lake, lakini *the content matter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, kuandaa nguvu kazi kwa soko la dunia. Tunaanzisha Mitaala, Katibu Mkuu wangu wa zamani Waziri wa Sayansi na Teknolojia, tumeandaa mitaala, ukiona inakucheleweshwa ibadilishe, inaitwa *radical change*. Siyo lazima mchakato, unajua kuna mchakato na kuna *radical change*. Ukiona unachelewa badilisha. Kama Korea, wanataka nguvu kazi leo waulize wanataka nguvu kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wamebahatika, watoto wetu wanafundishika. Aondoe magari *VETA*, afundishe vijana Wakorea wanataka nini? Apeleke vijana waende Korea. Hatuwezi kusubiri watoto wetu washindwe halafu tuhangaika. Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia, namweleza, nilimwomba karakana nne mojawapo ikiwa ya urembo, siyo biashara tena. Badilisha ya urembo, fundisha taaluma zinazotakiwa Korea na Ulaya, fundisha vijana wetu miaka sita,

19 JUNI, 2024

miaka minne, waende kutumika ulaya. Watarudi nyumbani wakati wa *Eid* au *Christmas* wakiwa wanaendesha magari yenye hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudie tena. Nimepata muda wa suala la magari yanayotoka nje. Tulifanya maamuzi kwa nia njema tukabadilisha *road toll* za kwetu. Waende wakapitie *road toll* na hiyo kuna *dilemma* kwa sababu, wakinywa mafuta mengi hapa utakuwa na *deficit* kwa kuwa, utatumia dola ku-*import*. Hata hivyo, wanaharibu barabara zetu, ni lazima tuwachakate, ili nao tuweze kuona inafanyikaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nilipokuwa ninachangia niliunga mkono bajeti zote bila kuacha hata moja. Sasa ninapokuwa najumuisha nitakuwa kituko nitakaposhindwa kuunga mkono. Sijawahi kusoma bajeti nzuri au hotuba nzuri ya mipango kama ya safari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti tu ya fedha imezungumza yenyewe. Pia, nachukua fursa hii Mheshimiwa Waziri, juzi Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI amenipigia simu ananiambia shule anazonipelekea sasa, tuko tunahangaika na tunakubali hiyo. Hata hivyo, nilimlilia Waziri wa Fedha, lile soko langu walilioniahidi mwaka 2022 na wakamsainisha mkandarasi mpaka leo anasubiri *advance*; Mheshimiwa Waziri atafute *advance* yoyote aniwekee wepesi, yeye nimekwishamwekea wepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Taufiq Salim Turkey ajiandae.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya roho ya nchi yetu na roho ya chama chetu. Kuna shairi linasema:-

19 JUNI, 2024

“Huko barabarani kumeingia shabuka, kuna vituko,  
Ikishawaondoka, wanatia huzuni na masikitiko”

Mheshimiwa Mwenyekiti, shairi hili Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande, atawafafanulia. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nafikiri alipoingia kwenye madaraka wengi walidhani hawezi, lakini waje kumtazama au kumsikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Awamu yake ya Sita amefanya mambo makubwa sana na sote ni mashahidi. Hata hivyo, huwezi kumzungumza Mheshimiwa Dkt. Mama Samia ukawaacha Mawaziri wake, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu. Hawa ndiyo wasaidizi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunapozungumzia barabara Waziri yupo, unapozungumza afya Waziri yupo, unapozungumza Elimu Waziri yupo, na kadhalika, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashangaa sana kumkuta Mbunge anaacha kuzungumza maneno Bungeni au kwenye chama chake anakwenda kuzungumza kwenye mitandao au kwenye vyombo vya habari. Ukimkuta Mbunge kama huyu ana lake jambo. Tena Waheshimiwa Wabunge tusilichukulie jambo hili kwa urahisi, hawa ndio wanaoturejesha nyuma katika maendeleo, hawa ndio wanaoirejesha nyuma Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na hawa ndio wanaomrejesha nyuma Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia miaka mitano tena. Atakapoachia miaka mitano tena, basi na wewe utajipanga, kitaamua Chama Cha Mapinduzi au wananchi kukuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesema barabarani huko kuna shabuka wanafanya vituko, wanawaahidi watu mambo ambayo hayapo kwa sababu, wananchi wanayaona mambo anayoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mengi. Vilevile tunaambiwa siku zote tumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini umshukuru na binadamu mwenzako kwa yale aliyoyafanya.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wa Tanzania sasa hivi sio wajinga, ni waelewa, yanayofanywa wanayaona. Mheshimiwa Dkt. Mama Samia yanapoingia maafa amekuwa ni Rais wa mwanzo anayewakimbilia wananchi. Hajamhamisha mwananchi yeyote kwenye maeneo yake, isipokuwa anamhamisha mwananchi aliyefikwa na maafa au pale alipo yatamfika maafa ndipo anakwenda kumwondosha. Vilevile hamwondoshi kwa mtutu wa bunduki wala kimabavu, anamjengea, anamwekea mazingira mazuri ndipo anakwenda kumweka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanatokea Watanzania wachache, wanaume, ninawashangaa sana. Hata hivyo, mwanaume huyu, Waheshimiwa Wabunge leo nitasema neno kama nitakosea nitaomba radhi, ukimkuta mwanaume anamtukana mwanamke kwenye viriri, huyo alichelewa kufanyiwa jando. Mwanaume huyu alichelewa kufanyiwa jando mpaka akaingia huko mitaani ndipo wakamwambia bora uende ukafanyiwe jando na waliomwambia ni wanawake. Kwa hivyo, leo ndiyo unamkuta kinywa chake kipana kumtukana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, haiwezekani na haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wanawake tunasema Mheshimiwa Dkt. Mama Samia ametufikisha mahali pakubwa sana. Tunajiamini na tunajielewa. Tunafanya kazi zetu kwa maono makubwa kuwa, hatujali kama mimi siwezi, mimi ni mwanamke. Mfano mdogo ni dada yetu Mheshimiwa Jenista anapofanya kazi zake kwa kweli, huyu mama ninampenda sana na ninamfagilia sana. Anaisaidia Serikali ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, lakini pia, anakisaidia Chama Cha Mapinduzi na analisaidia Bunge hili kwa nguvu zake zote. Waheshimiwa Wabunge tunapokaa kuzungumza ni lazima mambo mengine tupongezane, tushukuriane na tujaliane, isiwe kila kitu hatufanyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika. Bajeti zilizopita tulisema hapa, jamani Barabara kutoka Dodoma – Dar es Salaam iko vibaya sana. Hata hivyo, leo Wabunge

19 JUNI, 2024

tunaokwenda Dar es Salaam asilimia kubwa tunaona barabara inavyotengenezwa, imepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Fedha, tunapita pale Chalinze, usiku unakuta taa barabarani zimejipanga. Pia hii barabara ya Dar es Salaam ni kubwa na ni barabara ya biashara. Hebu na sisi tujipange kutia zile taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwantumu alizungumza akasema kuhusu kadhia ya bandarini. Mheshimiwa Waziri wa Fedha pale pana Wizara nyingi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha na Wizara ya Bandari (Wizara ya Uchukuzi), wakae wajaadili. Wanaopita pale ni wananchi wetu na wapigakura wetu, ninadhani wakae watazame vizuri na vilevile wale waliopo pale bandarini wawape elimu. Wakitaka kuzungumza kitu kizuri hata kama hakiwezekani, basi wazungumze na mtu vizuri. Hakiwezekani, lakini zungumza naye vizuri akuelewe kuliko ukiwa unampa maneno ya shombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana suala la pale bandarini limezungumzwa kwa muda mrefu, miaka mingi sana, walikalie kitako, kwa sababu, pale mwananchi anayepita anasema hao ni CCM, huyo ni Dkt. Samia, haiwezekani! Kwa hiyo, haipendezi. Mheshimiwa Waziri, tunakuomba walisimamie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabasi yanayokuja mikoani. Mabasi yanayokuja mikoani yana vituo vyao vidogovidogo vya kupakia abiria kutoka mjini kwenda Magufuli, Mbezi. Watu wengi wa karibukaribu walioko Dar es Salaam watakwenda pale Shekilango na maeneo mengine. Hata hivyo, toka juzi watu pale wamekuwa wanazuiwa wanaambiwa wasiende kuingia, watu wanafukuzwa na wanapata shida sana. Kutoka pale mjini mpaka kuelekea Mbezi ni shilingi 30,000 au shilingi 50,000 kwa taxi. Suala hili linakuwa gumu na wananchi wetu wanapata tabu. Tusijitazame sisi tuwatazame wananchi.



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi viongozi tuwajali zaidi wananchi wetu na ndiyo tunaisaidia Serikali yetu, chama chetu na Rais wetu. Ikiwa wale wananchi wa chini hatuwatazami na hatuwasikilizi matakwa yao ndiyo tunajiharibia sisi wenyewe. Leo utasikia DC ndiyo amezuia. DC hana uwezo wa kuzuia mabasi yasipakie Shekilango kwa sababu, kuna Sheria, sasa aisome ile Sheria. Vilevile ma-DC wamepelekwa kule, ili wakasimamie wananchi wamsaidie Rais na kukisaidia chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ukifanya lazima ujiongeze. Tusiwe tu kwa sababu, tumekuwa kwenye magari makubwa wale wa chini tunawaacha, tunakosea na tunakosea sana. Sisi wanawake tunapowakuta wananchi wetu kama wale roho zinakuwa zinatuumia sana kwa sababu, moja kwa moja anakuwa analengwa mkuu wetu wa nchi wakati lile suala ni la DC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine wazee wetu walikuwa wanasema “mnakuwa mnajitakia”, lakini sio kweli. Hatujitakii, ila ni lazima tujiongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kumzungumzia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Ninampongeza sana, anafanya mambo makubwa sana Zanzibar. Aliyekuja jana na juzi kwa kweli, Zanzibar imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo. Zanzibar kila wiki, kila mwezi ukienda kuna jambo jipya, mambo yamebadilika. Sasa wale wanaotia chokocho Mheshimiwa Dkt. Mwinyi anaendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Zanzibar kuna wazee, nyumba za wazee na Wazee Welezo. Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi wazee wale amewaweka kwenye Nyumba za Serikali Amani kwa Wazee. Hata hivyo, anawalisha, anawavisha na anawahudumia. Vilevile kuna wazee walioko mitaani, amewachukua wazee wale, kila mwezi alikuwa anawalipa shilingi 20,000 na sasa anawalipa shilingi 50,000. Wale wazee anawaenzi, tunasema Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi anafanya mambo makubwa sana.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja lilizungumzwa neno tukaambiwa tunataka *passport*. Sisi Zanzibar suala lile hatukuliunga mkono na wala hatukuliafiki. Sisi Zanzibar tuko na amani na tunapenda wageni kwa sababu, sisi Zanzibar tunapenda kutembea. Sisi Wazanzibari asili yetu ni kutembea na kufanya biashara kila maeneo na kila sehemu. Kwa hiyo, madhali tunatembea kwa watu na sisi tunasema Zanzibar ni njema atakaye na aje. Aje kwa maendeleo, upendo na kuishi na Wazanzibari, hilo kwetu sisi hatuna shida. *Passport* hii sisi bado hatujawa tayari, wala hatukuunga mkono na wala hatukumtuma mtu aje alizungumzie suala lile. Tunalilaani na sisi Wanzanzibari tunalilaani kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tuna tangazo lingine la wageni.

Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika, ambao kwanza ni Mheshimiwa Kemirembe Lwota, aliyekuwa Mbunge na ni Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, karibu sana Mheshimiwa na Ndugu Barnaba Mushi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Manyoni, kama yupo karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine; kwanza ni wageni 60 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni Kamati ya Siasa ya Wilaya na Viongozi wa CCM Kata kutoka Manyoni Mashariki Mkoa wa Singida, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 63 wa Mheshimiwa Mary Francis Masanja, ambao ni Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi lingine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 90 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Feza ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanafunzi. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Tunao wanafunzi 100 na walimu nane kutoka Taasisi ya *PCM Foundation* ya Jijini Dar es Salaam. *PCM Foundation* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanachama 60 wa Jukwaa la Wazalendo Huru kutoka mikoa mbalimbali Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wajasiriamali 10 kutoka Taasisi ya *Women Supporting Women* ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, namkaribisha Mheshimiwa Grace Tendega, atafuatia Mheshimiwa Toufiq Salim Turkey na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Bajeti hii ya Serikali ya mwaka huu 2024/2025, lakini pamoja na Mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IMF* ilibainisha vihatarishi vinavyoweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya ukuaji wa uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Nchi yetu ya Tanzania. Baadhi ya vitu hivyo ilikuwa ni upatikanaji wa mitaji, uhaba wa fedha za kigeni, gharama kubwa za mikopo na ukusanyaji duni wa mapato ya ndani. Hayo yaliainishwa huko lakini pia kuna vitu ambavyo vinaweza kusaidia kuimarika kwa uchumi kama tunavyo ambavyo ni upatikanaji wa dola za Marekani pamoja na kupungua kwa mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia suala la gesi kwenye magari ambalo Waheshimiwa wenzangu wawili watatu wamezungumza. Tumeona siku zote kuna mfanyabiashara mkubwa Dangote yeye alikuja na magari yake na yakawa yanatumia gesi *exclusively* kabisa na yalikuwa na sehemu yake anayotumia. Sisi raia wa kawaida kwa Dar es Salaam ambapo tuna vituo vikubwa ambacho kipo Ubungo tuna kituo kingine kiko TAZARA na kuna kituo kingine kiko *airport*.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tumegundua gesi ya kutumia kwenye magari tumekuwa na kituo mama ambacho ni cha Ubungo kikikorofisha ina maana vile vituo vingine haviwezi kupata kabisa gesi ya kuweka kwenye magari na sasa hivi watu wameanza kuhamasika. Watu wamehamasika kutumia magari wafanyabiashara, wenye magari ya *uber*, madereva wa malori na watu wengine wanajitafutia vipato wameanza ku-*install* vifaa vya kuweza kutumia gesi kwenye magari yao kwa sababu hiyo tunaona kwamba hili ni jambo zuri sana na linafaa kwa nchi yetu kwa nini? Kwa sababu kwanza hatuagizi gesi nje, gesi inapatikana nchini mwetu na kama inapatikana nchini mwetu ina maana kwamba hatutatumia dola kwenda kununua mafuta huko nje. Kwa hiyo ina maana kwamba sisi tutakuwa tumeweza kuhimili huo mfumuko kwa sababu tutakuwa na dola ambazo hazitumiki nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshtushwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyosoma ile hotuba kuongeza shilingi 382 kwa kila kilo ya gesi. Sasa hapo nikaanza kujiuliza unapoongeza mapema namna hii na watu wamehamasika watu wanaanza kutumia gesi na kubadilisha magari yao na kubadilisha ni gharama na ni kuanzia shilingi milioni mbili, milioni tatu na kwa malori milioni kumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mtu anayenunua gari akatumia mafuta haiingii hizo gharama, sasa huyu anayetumia gesi ataingia kwanza hizo gharama za mwanzo za vifaa vya kuwekeza kwenye matumizi haya ya gesi, sasa hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba tunatakiwa tutoe hata *incentives* tuweke ruzuku kwa vifaa vinavyoletwa kwa ajili ya kuweka kwenye magari yale ili wananchi waweze kuweka kwa gharama ndogo ama kama ni ruzuku basi waweke kwanza ili gesi iweze kutumika na inunulike itumike vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi yetu ikitumika hivyo tutakuwa tumeweza kufanya kazi kubwa, kwanza kule tutakuwa tumewanyima kazi kwa sababu kule tunavyopeleka dola tunanunua mafuta wenzetu wanaendelea kuwa na viwanda; vijana wanapata ajira na kadhalika. Sisi huku vijana hawapati

19 JUNI, 2024

ajira kwa sababu gesi yetu hatuitumii vizuri. Pia mteja wa gesi ni TANESCO, lakini tukifanya hivyo Watanzania walio wengi, magari ya Serikali na magari mengine watakwenda kutumia gesi yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutakuwa tumeacha kuagiza mafuta nje lakini sisi wenyewe dola tunaipata kwa shida yaani uuze korosho, uuze tumbaku, uende ukachimbe madini, uende kufanya utalii vitu vyote hivyo vinatufanya tutafute dola. Sasa kama tunatafuta dola halafu tunakwenda kununua mafuta badala ya kutengeneza namna ambayo tutafanya gesi yetu iweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndilo jambo ninalomwomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, anapokuja hapa hebu atueleze kwa nini ameweka hii gharama tena sasa? Badala ya kuacha kwanza angalau watu wahamasike waweze kuwekeza huko ndipo baadaye sasa tukiona kwamba ina manufaa tuone namna nyingine ambayo tunaweza tukafanya. Kwa hiyo, tutapata wateja wengi kama tutatoa ruzuku na tutaweza kuwasaidia wananchi. Vilevile, tutatengeneza ajira kubwa sana hapa nchini kwa sababu tutakuwa tumewafanya vijana wetu wamepata nafasi ya kuweza kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ni suala kushukuru Wizara imeweza kusikia na kuingeza kikokotoo ambacho wananchi walikuwa wanapiga kelele kwa muda mrefu. Japo wameongeza kutoka 33% kwenda kwenye 40% na ile kwenda kwenye 35% lakini mimi hoja yangu iko hapa kuna wale wastaafu ambao walishakuwa wamepata kiinua mgongo chao na wanalipwa kila mwezi hawajawahi kubadilishiwa wanakwenda na kiinua mgongo kilekile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za wenzetu unaona kwamba wanavyopandisha kima cha chini na pensheni inapanda. Kwa hiyo unakuta kwamba yule ambaye amestaafu na yeye ananufaika na kuishi kwa wakati huo kama wanavyoishi wengine lakini mtu anakuwa na kiinua mgongo kile kiko vilevile miaka nenda miaka rudi mtu alistaafu akiwa mwekahazina mkuu na

19 JUNI, 2024

mwingine alikuwa ni mhudumu anakuja yule anapata kiinua mgongo kikubwa na ile pesa ya kila mwezi kubwa kuliko yule na hakuhuishwi kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Wizara iweze kutekeleza na Wizara ya Mipango iweze kuweka kwenye mikakati yake kuhakikisha kwamba hawa waliokwishastaafu wanapohuisha mishahara, wanapohuisha masuala mbalimbali wawe wanawa-consider kwa sababu ni watu waliofanyia kazi nchi hii, wameitumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa na mpaka sasa hivi bado tunawategemea kwa sababu ni wazee ambao bado wanatupa busara zao. Kwa hiyo hawa wananchi walijenga nchi kwa busara kabisa, tunaomba wawafikirie hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka huwa tunapitisha Bajeti za Wizara zote ambazo zinaomba tukishapitisha tunajua kutakuwa na matumizi ambayo tumeyapitisha, lakini cha ajabu kwa mfano kuna Wizara ya Maji, Ujenzi na kadhalika lakini kinachosikitisha wakandarasi mbalimbali ambao wanafanya kazi maeneo tofauti wamekuwa hawalipwi fedha na hilo kwa kweli ni janga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kabisa wakandarasi wa Wizara ya Maji wengi hawajalipwa, kwenye Ujenzi huko TARURA hawajalipwa. Kutowalipa wakati tumetenga bajeti hawafanyi sawa kwa sababu kuna kuwa na malimbikizo ya riba ambayo hayo malimbikizo yanakuja kuathiri sasa kwenye bajeti zetu na hatimaye Watanzania wanakwenda kuwa na hali ngumu ya maisha kwa sababu fedha zinakwenda kutumika kulipa riba wakati tulitenga fedha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hapa atuambie kwa nini tunatenga pesa halafu zile pesa haziendi kulipa hizo *certificate* ambazo zinakuwa ziko *raised* na tulipokuwa tukisema hapa anasema fedha zipo hawajaleta lakini inaonesha kwamba *certificates* nyingi zimekwenda na hawajalipwa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Taarifa ya CAG inasema hivi kwenye matokeo ya ukaguzi wa kiufundi kuhusu

19 JUNI, 2024

usanifu wa usimamizi wa miradi teule ya usambazaji wa maji, jumla ya miradi mikubwa ilikuwa na mikataba ya jumla ya bilioni 110.7 hiyo ni miradi mikubwa na ilikuwa Fedha za Marekani milioni 523.84 na Euro milioni 52.44, ukaguzi ukabaini Wizara haikuwa na mipango kabambe ya kuwezesha utekelezaji. Hiyo Wizara haikuwa na mipango kabambe, sasa hii imepelekea kuwa na gharama kubwa za riba katika utekelezaji wa mikataba yake na imepelekea gharama za miradi kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 337 hadi shilingi trilioni moja ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu ucheleweshaji wa wakandarasi wa usambazaji, kwa mfano nachukulia mfano mmoja tu wa Mradi wa Usambazaji wa Maji wa Arusha unaitwa Orkesumet ambao aliomba kulipwa riba ya jumla ya shilingi milioni 728.6 na dola za Marekani 284,546.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia hizo fedha zingeweza kwenda kutekeleza miradi mingi ya zahanati zetu, vituo vya afya vyetu kwenda kutekeleza miradi ya shule, kwenda kutekeleza miradi ya kuwapa taulo za kike watoto wetu, lakini huyo anaomba hivyo kwenye mradi lakini kule kwenye bajeti tulitenga na hakupata na ali-raise certificate. Kwa hiyo tukiangalia hili, ndiyo maana unaangalia IMF imesema kabisa tunadorora kupata uchumi unaotakiwa kwa sababu ya kutokusanya vizuri mapato ya ndani na kutosimamia fedha ambazo zinatoka hilo ni kosa kubwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri akija atuambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nishukuru Serikali kufanyia marekebisho kipengele cha 18, ukurasa wa 82 cha jedwali la msamaha wa kodi linalojumuisha magari pamoja na vifaa vinavyotumika na Jeshi la Wananchi. Tulizungumza sana hapa, tunashukuru Serikali imefanyia kazi kwenye vifaa vile kwa sababu ni mazao ya kijeshi ni vyema vikafanyiwa hivyo kulikuwa na shida. Nashukuru sana. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Toufiq Turkey karibu, atafuatia Mheshimiwa Suma Ikenda na Mheshimiwa Japhet Hasunga, ajiandae.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. Naomba nitangulize kumshukuru Mwenyezi *Subhanahu Wata'ala* kwa kutujalia uhai na uzima na kufika siku ya leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa juhudi kubwa sana zinazotendeka kupitia Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli dira ya nchi hii inakoelekea na *vision* iliyokuwepo ndani ya nchi yetu ni ya kupatiwa faraja na fahari kubwa sana siyo ndani ya nchi yetu tu bali ndani ya Bara la Afrika na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi hii ya kimkakati na nataka niipongeze Serikali hususani katika Mradi wa SGR pamoja na Nyerere. Kupitia miradi hii Tanzania ndani ya Bara hili la Afrika kupitia *East Africa* tutakuwa kinara. Sasa pamoja Mji wetu huu wa Dodoma leo Mheshimiwa hapa Bibi Mwantumu alikuwa anaongelea kuhusiana na suala la ndege kuja ndani ya *capital city* yetu hii imekuwa ni changamoto kubwa sana. Sasa hivi ndege inafika shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni na nusu kwa sababu ndege zote zinakuwa *full*. Serikali walitazame suala hili la kuongeza ndege ili sasa Mji huu wa Dodoma uweze kunawiri na uweze kweli kuwa *capital city*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akihutubia Bunge letu hapa alituambia katika sababu zinazofanya Deni la Taifa kuongezeka ni kwa sababu sarufi imeshuka thamani. Tujiulize, changamoto hii imeikumba dunia yote, lakini ndani ya Tanzania sababu kuu iliyofanya sarufi yetu kushuka ni kuongezeka kwa *import* lakini pia kuwepo kwa *scarcity* ya dola imesababisha *scarcity* ya dola. Hii *scarcity* inatokana na kitu gani? Tuna *imports* ambazo asilimia kubwa ya *import* zetu ni mafuta na sababu nyingine kwa sababu ya *loan repayment* zetu zinahitaji *forex*. (Makofi)



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, Mheshimiwa mwenzangu aliyenitangulia, Mheshimiwa Tendega aliaongelea suala zuri tu la CNG. Jamani ilipotokea vita Ukraine mafuta kwetu huku yanapanda, vita vinatokea Israel na Lebanon kwetu sisi vinapanda. Tuna rasilimali zetu Tanzania, hatuna ushawishi wala hamasa wala *incentives* ya kuongeza masuala ya CNG. CNG gesi tunayo leo tunaelekea kwenye kuzalisha umeme kupitia *Nyerere Dam Hydro* gesi yetu tutakuwa tunayo kwa wingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna gani tunatazama hili suala la *forex* tukiweza ku-save *forex* tu basi tayari tulishalipa deni kubwa tu la Taifa letu. Kwa nini hatupi kipaumbele suala zima la *forex* tukasema hapa lazima rasilimali ya nchi yetu tuitumie ili sarufi yetu iwe imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anatoka mjasiriamali Kariakoo alikuwa na pesa zake dola 10,000 akaenda zake China akaleta mzigo. Kafika zake Dar es Salaam kalipa kodi anauza bidhaa yake kakopesha kwa wiki mbili, kauza. Mwanzo alikuwa na milioni 25 kawekeza milioni 30 anauza mzigo anasema bwana kapata faida mwenyewe milioni tano, kumi anaenda ku-change ile dola anaambiwa umepata hasara ya milioni mbili, huyo Mtanzania anaelekea wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ifike sehemu jamani lazima tuwe na mkakati madhubuti, tumechukua mikopo ambayo ni mizuri kwa sababu ya Taifa letu tumewekeza katika mpango na maendeleo ya nchi yetu, lakini yako mataifa makubwa tu kama Spain, Marekani na duniani kote wana *restructure* mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumechukua mikopo ambayo tunatakiwa tulipe ndani ya miaka nane hadi 10, kwa nini tusiwarudie tukawaambia mikopo hii tunataka tulipe ndani ya miaka 15? Inawezekana, tukipandisha ule muda *automatically* ile *EMI* ya kila muda inapungua. Kwa hiyo, yale mahitaji ya dola yataapungua yataingia kwenye soko letu ndipo tutaweza kui-save *forex* yetu. Kwa hiyo, naomba sana kupitia Wizara hizi mbili, ya Fedha na Mipango, lazima waje na mkakati maalum wa

19 JUNI, 2024

kuhakikisha kupitia Wizara ya Fedha waje na *restructure* za *loan*. Lazima muda wa kulipa hii *loan* uwe mrefu ili wao wapate pumzi ya kuweza kuhimili kutokulipa dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni lazima tutumie rasilimali zetu. CNG ipo, hamasa ipo, lakini bado Serikali hatujaona kuwapa kipaumbele suala zima la gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tukiwa tunatembea katika ndege hizi na tukienda safari hizi za mikoani, unaenda sehemu unakuta kwa mbali hakuna nyumba, unapita baada ya mwezi unakuta nyumba mbili, tatu, baada ya miezi sita zinaanza nyumba 10, 20 baada ya mwaka unakuta ni kijiji. Huu mpangilio wa ardhi wa nchi yetu inaonekana bado hatujaupa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna tunavyoendelea tutafika mwisho wa dunia tutasimama hapa itakuwa kilio chetu ni maji, barabara na umeme kwa sababu hatuna mpango wa ardhi, kuna umuhimu sana. Sasa hivi ni lazima ifike sehemu nchi nzima tuwe na mpango wa ardhi. Tujue wapi pa kulima, wapi pa kufuga na wapi kwenye maendeleo ya makazi ya watu kuishi. Haiwezekani leo mtu ajiamulie tu aende porini aweke banda lake, kesho amuite jamaa yake, mjomba wake na shangazi yake, waseme sasa hivi hii ni Kata hatuna maji! Nchi haiendeshwi hivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huko Marekani, Uingereza na uende sehemu yoyote iliyoendelea ziko sehemu haziruhusiwi kujengwa nyumba. Ziko sehemu za kujenga makazi na ziko sehemu za kufanyia biashara, lazima kuwe na mpangilio. Kwa hiyo, naiomba Serikali itizame suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujikita sasa katika suala la biashara hususani baina ya Tanzania Visiwani na Tanzania Bara. Wizara ya Fedha kuna changamoto kubwa sana ambayo inafanya Visiwani Zanzibar kutokuwa na *advantage* ya biashara. Leo hii mfanyabiashara anaponunua bidhaa zake Zanzibar

19 JUNI, 2024

anachukua VAT analipa 15%, anapokuja Bara anatakiwa alipe *difference* ya *three percent*, inakuwa *18 percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina hoteli, nataka ni-*claim* vitu ninavyonunua Zanzibar ile asilimia ya *input* ya 15% iweze kunisaidia. Ile haikubali kwenye mifumo yao. Kwa hivyo Sasa mfanyabiashara wa Bara anasema kwa nini ninunue Zanzibar ambapo siwezi ku-*claim* VAT yangu? Kwa sababu mifumo haioani. Kwa hivyo, namwomba Waziri awaelezee Wizara ya Fedha huko kuhakikisha mifumo yao iendane na ZRA kuhakikisha watu wa Bara waweze ku-*claim* VAT yao, hilo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili katika suala zima hata masuala ya bidhaa, hapa Mheshimiwa Mwantumu pia kaliongelea, suala zima la biashara unapoleta bidhaa zako kutoka Visiwani kuja Bara na Bara kwenda Visiwani. Jamani hakuna *easy of doing business* kabisa. Unapofanya biashara baina ya Visiwani na Bara ni kama unaenda zako vitani vile. Unajiwekea makombora yote na kadi zote, leo bwana akija huyu niwe na hiki, niwe na hili na niwe na lile maana inakuwa bugudha hata saa nyingine bora usifanye biashara! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sana kuna umuhimu wa kuwa na kamati maalum ya kupeleka hizo kero, leo kuna kamati maalum za kupeleka kero hapa *East Africa Community*, kama kuna tatizo baina ya Kenya na Tanzania, ipo, baina ya Rwanda sijui na nani, ipo, kwa nini baina ya Zanzibar haipo na wakati ni nchi moja? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nenda TRA hiyo moja, huyu anakwambia hivi, yule vile, huyu lile na huyu lile, haiwezekani! Ifike sehemu lazima kuna sehemu twende. Kuna mambo mengine hayataki hata, kuna tatizo la sheria wala *policy*, kila kitu kipo. Ni mtu tu na tabia yake siku hiyo kakerwa kaamua na yeye akere kila mtu, haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi kuna mifumo ya *digitalisation*, sasa hivi kuna *e-office* na kuna kila kitu, hata tunapozungumza *committee* siyo kama mtu utengeneze jambo

19 JUNI, 2024

lolote kubwa, inatakiwa ile mifumo ioane na kama kuna *complains* zifanyiwe kazi na siku hizi *complains* zinaonekana kwa *graph* tu, ngapi zimechukuliwa na ngapi zimefanyika, hutakiwi ku-*address*. Huko tunakotaka kuelekea hilo ndiyo Taifa, dunia ndiko inakoelekea katika masuala ya *artificial intelligence*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bado hatu *embrace* mifumo wala hatutaki kuitumia, bado tunataka Mungu watu. Maana lazima mtu asimame aseme bwana mimi ndiye kibambe, haiwezekani! Leo tuiachie mifumo ifanye kazi, watu wafanye kazi tuende katika *easy of doing business* tuwajibike. Ndiyo maana katika Sekta ya Elimu nikasema sana, jamani kuna umuhimu sana vizazi vyetu sisi tukiwemo na wajao, kuna umuhimu wa *artificial intelligence*. Kazi zitakazokuja baadaye siyo kazi za Mungu mtu, siyo kazi ya kuonekana wewe, ni kazi za maarifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu vijana wetu wawe tayari katika hilo Taifa linalokuja baadaye. Uchumi unaokuja, nilizungumza mara nyingi hapa, tulipoanza dunia hii tuliambiwa *landlords* ndiyo walikuwa wenye pesa, wakaja *industrialists*, wakaja watu wenye mifumo (ma-ICT), Sasa hivi tunapoelekea ni *artificial intelligence*, roboti. Taifa letu limejiwekeza wapi? Katika *research and development*, bado tuko nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kupitia Bunge lako hili Tukufu Serikali ijielekeze katika suala zima la *artificial intelligence* na *research and development*, kwani Mabara yote yanayoendelea duniani sasa hivi na yaliyotajwa yatakayoendelea duniani yamejiwekeza katika *digitalisation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba niunge mkono hoja, ahsanteni sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Turkey kuna mahali ulitamka sarufi, nadhani ulimaanisha sarafu naomba ufanye marekebishio ili *Hansard* ikae vizuri.

**MHE. TOUFIQ S. TURKY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sarafu (*currency*), ahsante sana. (Makofi)

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mchango kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na afya njema na imempendeza muda huu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mwigulu amekuwa akifanya kazi kubwa na nzuri sana ambapo mambo yote kwenye upande wa Wizara ya Fedha yanakwenda vizuri pamoja na Kaka yangu Naibu Waziri Mheshimiwa Chande wanafanya vizuri sana, nikisema wanafanya vizuri ni pamoja na Wizara yote ya Fedha wanafanya kazi nzuri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wanafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu, nikiwa ni mwakilishi wa wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya, nampongeza Kaka yangu Profesa Kitila Mkumbo anafanya kazi nzuri sana. Hotuba yake niliisikiliza vizuri sana imesheheni mambo mazuri ya mipango mingi ambayo Serikali inafanya, nampongeza sana pamoja na Naibu Waziri wake kwa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana nimekuwa nikimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo Mwenyezi Mungu anaendelea kumpatia macho ya rohoni kwa wateuzi wake wote anaowapa nafasi za kusimamia Serikali yake na kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa nikiomba sana Barabara ya njia nne ya Mkoa wa Mbeya na barabara hiyo iko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, barabara hiyo ya kutokea Igawa mpaka Tunduma. Kwa mapenzi mema na makubwa sana ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu

19 JUNI, 2024

Hassan alisikia maombi ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya, alisimama akaeleza kwamba wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa kuanzia naomba tuanze na kilomita 29 ambazo zinaanzia Nsalaga mpaka Ifisi, kwa kuliona hili barabara hiyo ambapo Mheshimiwa Rais alisema ianzie, barabara hiyo inapita katikati ya Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapenzi mema hayo ya Mheshimiwa Rais ninachoelewa mimi na wananchi wa Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa Rais atakachokisema hayo ni maagizo na hayo ni maelekezo kinachosubiriwa ni utekelezaji. Wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanampenda sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na wana mapenzi mema sana naye, lakini sasa sijui ni kwa nini, sijui ni watendaji, sijui ni watumishi, wanataka kumchonganisha Mheshimiwa Rais na wananchi wa Mkoa wa Mbeya, wananchi wa Mkoa wa Mbeya wamemkubali sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba barabara ile imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 138, mpaka sasa zimetolewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 17 ndizo alizopewa mkandarasi, ambapo barabara hiyo mkataba wake ni wa miaka miwili. 14% ndiyo fedha iliyotolewa bado 86. Kati ya hiyo miezi, miezi 16 ndiyo 14% bado miezi nane. Nina wasiwasi na wananchi wa Mkoa wa Mbeya, tuna wasiwasi kwamba je, ndani ya hii miezi nane mkataba unavyoonesha hiyo barabara itakuwa tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kaka yangu hapo Profesa Mkumbo nakuomba mipango yako unayoipanga kuhusu maendeleo ya Taifa hili la Tanzania, naomba sana uelekeze pale Mkoani Mbeya, kwa sababu tunakokwenda sasa tunaelewa kabisa pale barabara zinapotakiwa zipite barabara nne tunaelewa kabisa kwamba pale ndipo Jiji lilipo na Jiji hilo linaeleweka ni Jimbo la nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, maeneo yale yote tunayoyaongelea, Mbeya ni lango la biashara. Nchi ya Zambia, Malawi na Congo wanategemea sana pale, lakini ukiangalia magari makubwa yote yanayopita kwenda nchi zote

19 JUNI, 2024

jirani na Tanzania magari yale yanapita pale. Ninaiomba sana Wizara ya Fedha tuelekeze kibubu chote cha fedha kwenye barabara zile njia nne za Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata shida sana wakati tukiwaeleza wananchi na kuwaaminisha, barabara ya njia nne iko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambapo tumeambiwa kwamba kufikia 2025 barabara itakuwa imekamilika. Sasa je, kwa mambo kama haya yanavyoendelea kwa fedha zinavyotolewa kidogo kidogo, je, hii barabara itakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapenzi makubwa ambayo tunaheshimu kiti na viti alivyonavyo Mheshimiwa Dkt. Tulia, tunaheshimu sana nafasi alizonazo kuwa yeye ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge ya Dunia, lakini sasa pale usoni kwake barabara ile inasuasua sana. Naomba sana barabara ile Serikali iitizame kwa umakini sana ili kuhakikisha inakwenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwenye Wizara ya Ujenzi majibu niliyopata hapa wananchi wa Mkoa wa Mbeya wakasikia kwamba barabara ile ya Mkoa wa Mbeya kilichokuwa kikiichelewesha ni miundombinu kwa maana kwamba kuhamisha mabomba ya maji, sijui mambo ya umeme na nini. Sasa hivi ile imefanyika na imekuwa tayari, sasa mkandarasi anachoomba ni kuelekezwa fedha za kutosha ili aendelee kufanya kazi aweze kukamilisha barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanyakyusa tabia yao kubwa ni huruma na upendo, ndiyo maana wakipita mahala akasikia kuna msiba anakatisha anaanza kulia kwenye ule msiba, akilia saa nzima anaanza kuuliza aliyekufa hapa ni nani, wakimwambia aliyekufa ni nani anaanza upya msiba mzito. Sasa ule ni msiba wa mtu hata hamfahamu. Sasa wananchi wa Mkoa wa Mbeya wana msiba wao wenyewe, wanalia juu ya barabara, kwa sababu ni tatizo kubwa sana. Unategemea wanalia kiasi gani kwa sababu msiba ule ni wa kwao wenyewe wanalia ndani ya nyumba yao wenyewe. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili mlichukulie kwa uzito sana, lakini najua Wizara yote ya Afya, Wizara ya Mipango pamoja na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yote kwa ujumla inaitazama kwa jicho la huruma na upendo barabara hiyo. Kwa hiyo, tunategemea sana kwamba barabara ile ikamilike kwa wakati kama mkataba unavyoonesha, kwa sababu ya kusema ratiba zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya uendeshaji wa ile barabara zimekamilika, sasa ninachotegemea kwamba pale patakwenda kushambuliwa kama mpira wa kona ili kuhakikisha barabara ile inakwenda kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia sehemu moja kwenye Wizara ya Habari, kwenye Wizara hii Wilayani Kyela kuna Kata nane ambazo baadhi ya maeneo ukifika kwenye zile Kata unaambiwa tu karibu nchini Malawi, yote hiyo ni kwa sababu ya minara ya kule inaonekana kwamba ni hafifu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke utaratibu wa kujenga minara kule na Kata zenyewe nazitaja hapa. Kata zenyewe ni Kata ya Matema, Kajunjumele, Ngana, Njisi, Ibanda, Ngonga, Ikimba na Katumba Songwe. Kwa maana hiyo wananchi wanaoishi maeneo yale hawaweki vocha kupitia huku kwetu Tanzania, ina maana vocha wananunua za kule. Mapato inapata nchi nyingine wakati wao ni Watanzania na mapato hayo yanatakiwa yaingie kwenye Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iliangalie hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda samahani, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, taarifa.

## **TAARIFA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, anachokisema ni sahihi kabisa. Siyo tu kwamba wananunua



19 JUNI, 2024

vocha za Malawi, pia wanasikiliza Redio Malawi kwa sababu tayari kila kitu kinakuwa nje. Kwa hiyo, tunaomba waliangalie kwa umakini. Anachokisema nakiunga mkono na nakisisitiza zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda, unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Sophia Mwakagenda?

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. Nakushukuru sana Mheshimiwa Sophia kwa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, kwa hiyo nchi yetu ya Tanzania wananchi wale ambao wanaishi kwenye hizo Kata kule Wilayani Kyela wanakwama kabisa kusikiliza wakati fulani hata taarifa ya habari ya Taifa lao la Tanzania kwa maana muda wote wanasikiliza Redio Malawi, nitashukuru sana kwenye hili kama wamelifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni pale ambapo wakandarasi wa Taifa hili la Tanzania wanafanya kazi kwa kujitoa sana wanapokuwa wamekabidhiwa mikataba katika kazi zao maana mikataba inawaamuru wafanye kazi kwa wakati, lakini wakimaliza kufanya kazi kwa wakati hawalipwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi wengi sana, wazabuni na *suppliers* wa Taifa hili la Tanzania wakipewa *order* ama wakapewa kazi ya kufanya, siyo kwamba wanapewa *advance* kwanza Serikali, wao wanachukua jukumu, wengine wana mitaji, lakini katika mitaji hiyo wanatakiwa wazungushe, lakini walio wengi wanakwenda kukopa fedha benki ili waendeshe kazi hizo wakitegemea kulipwa, matokeo yake hawalipwi kwa wakati na hatimaye wanakwenda kuuziwa dhamana zao na watu hao hao wanakwenda kupata *stroke* kwa ajili ya mshtuko na wengine wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu kwa sababu alikuwa ameweka dhamana nyumba anayoishi lakini inakwenda kupigwa mnada, anaanza kwenda kupanga, matokeo yake anapigwa *stroke* na wengine wanapoteza maisha. (*Makofi*)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hilo hilo hapo, kinachoonekana ni kwamba mkandarasi huyu ama mzabuni ama *supplier* kama hajafanya kwa wakati, Serikali inampiga *penalty* aanze kuilipa Serikali, lakini mkandarasi huyu ama *supplier* na mzabuni wao wakicheleweshewa fedha zao hakuna chochote ambacho wanapewa kwamba ni nyongeza zaidi ama kwamba wataifanyia sasa kwenye ule mpango kwamba na sisi sasa hivi tuanze kulipwa fidia ya kucheleweshewa fedha zetu. Kama ali-*supply* vifaa miaka mitano iliyopita au miaka 10 matokeo yake anakwama, anaanguka mtaji na anapata shida sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba sana kaka yangu, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu na kaka yangu Mheshimiwa Prof. Kitila, wanapokuja hapa kuhitimisha watuambie sana wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuhusu ile barabara wana mpango gani na barabara ya Mbeya Jiji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka majibu hayo yatukolee sana, yasiwe ya juu juu tu. Yawe ya uhakika kwamba barabara ile ya njia nne ambayo tunaiongelea kila siku, mambo hayaendi kama inavyotakiwa. Kila wakati barabara ile imeleta shida, ni kwamba haina hata *service road*, tunapita sehemu moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Waziri Prof. Kitila wanapokuja hapa ku-*wind-up* watuambie wananchi wa Mkoa wa Mbeya kitakachoendelea juu ya barabara ile ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya tunayopiga kelele kila siku ukizingatia nimepata ajali juzi, wiki mbili zilizopita wamekufa watu wengi sana kwenye ile barabara. Magari matatu yamegongana kwa sababu ya ufinyu wa barabara...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wamekufa na wengine wamebaki walemavu.

19 JUNI, 2024

Tafadhali sana, nakushukuru sana kwa nafasi. Naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa ajili ya *Hansard*, nafikiri Mheshimiwa Suma Ikenda alipotamka Wizara ya Afya alimaanisha Wizara ya Fedha.

Nadhani ndivyo hivyo, Mheshimiwa Suma?

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ulimi uliteleza, ninaongelea Wizara ya Ujenzi, lakini tunaongelea hapa Wizara ya Fedha ambayo ndiyo imeshika kihenge chote cha nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Jambo la kwanza, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio na kazi kubwa ambazo anazifanya katika nchi yetu. Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa mnazoendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawapongeza Mawaziri wawili; Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Uwekezaji, kwa hotuba nzuri ambazo wameziwasilisha humu Bungeni. Pia, nawapongeza watumishi wa Wizara hizi mbili na taasisi zote zilizoko chini ya hizi Wizara. Zaidi ya hapo tunaipongeza Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuchambua bajeti hii na mipango hii, mmeifanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua na katika kuchagua lazima uangalie unachagua nini na kwa wakati gani?

19 JUNI, 2024

Katika kipindi tulichonacho, tunayo matatizo ya msingi ambayo mipango yetu lazima iende kujibu hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo yanayotusibu katika nchi hii ni pamoja na ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Tatizo la ajira ni kubwa na tatizo hili lazima mipango hii tuonyeshe tunavyoenda kulitatua na tuwe na mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili tulilionalo ni umaskini mkubwa ambao wananchi wanao katika nchi ambayo ni tajiri sana. Tatizo la tatu ni uchumi mdogo tulionao katika rasilimali nyingi zilizopo katika nchi yetu. Tatizo la nne ni tija ndogo katika maeneo mbalimbali, na la tano ni ujinga na teknolojia duni tunazotumia katika uzalishaji na mambo mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa bajeti yetu na mipango yetu lazima ijielekeze katika kujibu hoja hizi. Tukitatusa hizi ndiyo tutaweza kujenga nchi yetu, tutaweza kuwasaidia wananchi wetu na nchi itapiga hatua kubwa. Sasa, ukipitia bajeti ya leo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inatuonyesha sura ifuatayo:-)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mapato ya ndani ya TRA ni shilingi trilioni 29.4, mapato yasiyo ya kikodi ni shilingi trilioni 3.8, mapato ya halmashauri ni shilingi trilioni 1.3. Jumla ya mapato yote ya ndani ni shilingi trilioni 34.5, sawa na 70% ya bajeti nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaashiria nini? Maana yake ukichukua bajeti yetu yote ya shilingi trilioni 49, shilingi trilioni 34 tu ndiyo tuna uwezo wa kuzikusanya na kuzizalisha wenyewe. Kwa hiyo, fedha nyingine lazima zitoke kwenye misaada na mikopo. Sasa bajeti inatuambia mikopo na misaada ni shilingi trilioni 14.7 ambapo mikopo ya ndani ni shilingi trilioni 6.5 na mikopo ya nje ni shilingi trilioni 8.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ya nchi yetu ni shilingi trilioni 11.1. Hii maana yake ni nini? Kama bajeti ya

19 JUNI, 2024

maendeleo ya nchi yetu ni shilingi trilioni 11 na bajeti ya mikopo na misaada ni shilingi trilioni 14 na mapato ni shilingi trilioni 34, maana yake katika bajeti hii mapato yetu ya ndani hayatoshelezi na hayawezi kwenda kutumika kuwekeza katika miradi mbalimbali tunayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake bajeti ya kwetu sasa hivi ya maendeleo lazima ni bajeti tegemezi. Maana yake tukikosa hiyo misaada, tusipokuwa na mikopo, maana yake hatutaweza kutekeleza mradi hata mmoja wa maendeleo. Sasa hii maana yake nini? Ni kwamba kwa wale wanaosema hatutakiwi kukopa, maana yake tusimamishe miradi yote ya maendeleo, na hii nchi hatuwezi kufanya hivyo. Sana sana, sasa hivi lazima tukope tukawekeze kwenye miradi hii ya maendeleo, lakini tuwe na muda kwamba ikifika kipindi fulani sasa tujitegemee. Kwa hiyo, lazima sasa tuache kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kujitawala ni kujitegemea na ili tufike kujitegemea ni lazima tukope, tuwekeze, na tuzalishe. Tukizalisha sasa, tuanze kujitegemea. Kwa hiyo, nadhani kwa msingi wa bajeti hii, lazima tuendeleo kupata misaada na mikopo, lakini tuelekeze kwenye sekta za uzalishaji zitakazoweza kujenga uchumi imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hii bajeti, mchango wa taasisi za umma yaani mashirika ya umma na taasisi mbalimbali, zinachangia shilingi trilioni tatu tu. Nimeangalia, wameweka ile ruzuku au gawio tunalolipata. Sasa, bajeti zao zile wanazozalisha, fedha zote wanazozalisha mashirika ya umma na taasisi za umma hazipo kwenye hii Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *model* inayotumika katika kupanga hizi bajeti, sasa Waheshimiwa Mawaziri wangu wawili wapendwa, mwangalie ile *model* ili tuweze ku-*capture* mapato yote yanayozalishwa na taasisi za umma yaingie kwenye Bajeti Kuu, ije hapa na Bunge liwe na mamlaka ya kuidhinisha hizo bajeti. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi bajeti za mashirika ya umma haziidhinishwi na hazipitishwi na Bunge hili. Hii ni kinyume kidogo. Kwa hiyo, nafikiri umefika wakati tuangalie ile *model* ili bajeti ya TANESCO, Bandari, TTCL, mashirika mbalimbali zije hapa Bungeni iwe ni sehemu ya Bajeti Kuu na mapato yataweza kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sisi kule Mbozi tunahitaji maendeleo na tunahitaji vitu vingi kwa sababu ni mkoa wa wakulima na ni wilaya ya wakulima. Kuna vihenge vilianza kujengwa vikaishia katikati havijakamilika. Vile vihenge ni muhimu sana kwa kuhifadhi chakula. Tunaomba Serikali mvimalizie vile vihenge vianze kufanya kazi kwa sababu vilikuwa vimefika 85%. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Barabara ya Londoni – Iganduka – Msia – Isalala, Barabara ya Ihanda – Ipunga – Chindi, Barabara ya Chimbuya – Ludewa, Barabara ya kutoka Mahenje – Kimondo – Hasanga na barabara nyingine ni muhimu sana zikapewa fedha ili kusudi ziweze kuchangia katika mendeleo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iweze Kwenda, tunahitaji *import substitution* na tunahitaji tuweze kutatua changamoto tulizonazo. Nini tukifanye? Kitu cha kwanza, tuwekeze fedha nyingi katika sekta za uzalishaji na ninawapongeza mmeweka fedha nyingi kwenye sekta za uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kilimo kilivyopewa fedha nyingi, tunaona uvuvi ilivyopewa fedha nyingi, mifugo ilivyopewa fedha nyingi. Kikubwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu peleka hizo fedha zikazalishe zaidi, zisimamiwe vizuri na ziongeze uzalishaji kwenye nchi hii. Hapo nchi tutaweza kupiga hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuanza kutafuta mazao ambayo tutayazalisha hapa na bidhaa ambazo zinachukua fedha zetu za kigeni kwa wingi ambazo tunaagiza nje. Kwa mfano, mafuta ya kula yanatumia shilingi bilioni nyingi sana za hela za Tanzania kwenda kuagiza nje. Nchi yetu tulipofika

19 JUNI, 2024

hatuhitaji kuagiza mafuta kutoka nje. Tunahitaji mafuta ya kula, tuzalishe hapa alizeti kwa wingi, tuchakate na kuhakikisha kwamba tunapata mafuta ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuongeza uzalishaji wa kilimo cha miwa ili tuzalishe sukari yetu hapa hapa nchini. Hatuhitaji, nchi ndogo kama ya Uganda, siyo vizuri ikatushinda kuwa na utoshelevu wa sukari kuliko nchi ya Tanzania ambayo ni tajiri sana kwa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kujitosheleza kwa chakula lakini zaidi ya hapo tunahitaji mfuko wa kuchochea viwanda na ujenzi wa viwanda. Nilisema na nitaendelea kusema, bila kuwa na mfuko wa ujenzi wa viwanda, hapa tutaimba tu kujenga viwanda. Viwanda ndiyo vitatusaidia kupunguza tatizo la ajira, ndiyo tutazalisha bidhaa za kwetu za kwenda kushindana katika soko la dunia. Kwa hiyo, lazima tuwekeze, tujenge miundombinu, Serikali iweke fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuimarisha miundombinu mbalimbali kama ile ya bandari, TAZARA na SGR. Miundombinu hii ni msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu. Uwekezaji lazima uendeleo na ndiyo maana nimesema lazima tuendeleo kukopa lakini tunahitaji pia kuimarisha maslahi ya watumishi wa umma ili waweze kufanya kazi kwa weledi, tija, kujituma na waweze kuchangia na kuwa wabunifu zaidi kusudi nchi iweze kupiga hatua kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kukuza Sekta Binafsi. Sekta binafsi lazima iwe *supported*. Hii ndiyo msingi wa kulipa kodi, na hii ndiyo itakayokuwa mhimili wa kujenga uchumi wetu na Watanzania walio wengi walioko kwenye sekta binafsi. Hata kilimo tunachosema ni sekta binafsi, lazima kiwe *supported*, waweze kuchangia katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunahitaji kuanzisha Baraza la Tija. Baraza la Tija litatusaidia kuongeza tija kwenye kilimo, viwanda na maeneo mengine. Tuliliondoa siku nyingi, nami naendelea kulisema kwamba Baraza la Tija ni muhimu sana katika

19 JUNI, 2024

kuweza kuchochea maendeleo ya nchi yetu. Tunahitaji kuongeza jitihada katika kutangaza utalii na miundombinu yote iliyopo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya pamoja na mambo mengine yote, eneo kama la kule Songwe, Tunduma pale bandari kavu tunahitaji ile iimarishwe na uwekezaji uwe mkubwa. Nchi za SADC na nchi za huko kusini mwa Afrika zije kununua bidhaa mbalimbali pale. Pale Dar es Salaam tuimarishwe tuwe na maduka makubwa. Wale badala ya kwenda China, waje Tanzania wachukue, tufanye biashara na hapo ndipo nchi yetu itaweza kupiga hatua na tutaweza kukusanya kodi na tutaongeza wigo wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa nafasi. Naunga mkono hoja na ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, atafuata Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niseme kidogo kwenye hii Bajeti Kuu ya Serikali, niweke mchango wangu. Awali ya yote napenda kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza yeye mwenyewe kwa kazi kubwa anayoifanya, Serikali yake yote na wasaidizi wake wote kwa kuzidi kuboresha maslahi na ustawi wa Tanzania, nampa heko sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, leo ningependa kuzungumzia jinsi ambavyo nafikiria ni njia gani ambayo itasaidia nchi yetu kuongeza viwanda au kuwa nchi ya viwanda. Nimemsikia Mheshimiwa Hasunga hapa amesema kwamba uchumi wetu tukitaka uimarike, tuwe na viwanda vingi na tuongeze viwanda, ni sahihi kabisa. Kwa hiyo, mchango wangu unajikita hapo kuhusu jambo hili la kuongeza uchumi wa viwanda. *(Makofi)*



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia bajeti na mpango tunazungumzia maslahi ya Watanzania kuboresha ustawi na ufanisi wa maisha iweze kuwa himilivu na nzuri zaidi. Sasa ukiangalia kwa ujumla katika nchi yetu huduma zinazidi kuboreka; usafiri, mabasi yanakuwa mazuri. Juzi tumefungua reli ya kisasa imeanza kazi, huduma ya *petrol stations* (vituo vya mafuta ya magari na mafuta mengine maarufu sheli) kujenga hoteli na *guest houses*; huduma zinazidi kuimarika na kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 katikati nilifanya utundu kidogo, nilikuwa naelekea Dar es Salaam, nikahesabu *petrol stations* (hizi sheli) kuanzia Chalinze hadi Kibaha Maili Moja, nilipata sheli 68. Pale kuna kilomita 75, sheli 68 na leo nafikiri zimeshafika 100 na zaidi maana yake wanajenga kila siku. Ukipita unaangalia kushoto na kulia wanajenga, sheli zinazidi kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga sheli moja kwa makadirio yangu nafikiri inaweza kugharimu shilingi bilioni moja. Ununue ardhi ambayo iko barabarani siyo hela ndogo, upate kiwanja cha ekari moja au mbili ni pesa nyingi. Uweke matenki yale na *pumps* chini ya ardhi na juu yapande matenki na *pumps* ni hela nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenge nyumba zile, ofisi, wengine maduka ya vyakula, *restaurants*, huduma za magari, *service* na kadhalika; ni hela nyingi kujenga nyumba zile. Kuweka zege au *pavements* kusudi ardhi isiwe ya matope pale, kwa hiyo, ni gharama kubwa, ikiwa ndogo nafikiri ni shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa urefu ule wa kilomita 75, sheli 100 ni za nini? Wanagombania magari, magari yakija wale wahudumu wanakimbia, njoo huku! Njoo huku! Wanashindania magari kwa sababu hawana wateja wa kutosha. Zingejengwa 10 pale zingetosha kuanzia Chalinze mpaka Kibaha Maili Moja pale zingetosha kabisa na watu wangeuza wale wenye sheli zao zile, wasingeshindania magari, na biashara ingekuwa nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ya wageni moja, (*guest house*) kujenga ndogo kabisa labda ya vyumba 10, au vyumba

19 JUNI, 2024

20, unaongelea shilingi milioni 100 au shilingi milioni 150 kwa uchache; lakini unakuta kuna wageni wanaokuja pale kwa siku ni wawili tu, au mmoja, au sifuri, hatupati wateja kwa sababu zipo nyingi sana kuliko mahitaji ya wageni. Kwa hiyo, pale kwenye sheli, labda *guest house* 20, tano zingetoshwa, au nne, au mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikisema haya, naweka msingi wa kusema yafuatayo; kwamba, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Uwekezaji, tumemsikia juzi hapa akielezea hotuba yake, nafikiri kwenye Wizara yake, TIC kile Kituo cha Uwekezaji, kinafanya kazi nzuri, tunakipongeza. Kusajili miradi, lakini zaidi zaidi naona kama kinasaidia sana kuleta miradi ya nje, wawekezaji kutoka nje, kujenga viwanda vya *cement*, akina Dangote, akina Twiga wale, watu wa nje, na kampuni kubwa. Viwanda vya *tiles* Mkuranga kule na Chalinze, vya Wachina kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri TIC iwe na kitengo pale ndani cha kuhamasisha viwanda vya wazawa. Sasa, ichoronge kiwanda kwenye makaratasi, siyo kwenye kukijenga; kwenye makaratasi. landike mradi wa kiwanda, tuchukulie labda kiwanda cha matairi ya pikipiki ambazo ziko nyingi sana, hivyo soko lipo. Kiwanda cha matairi ya pikipiki, iainishe mahitaji ya mtaji, iainishe mahitaji ya malighafi (*raw materials*), iainishe mahitaji ya uendeshaji, Meneja, Wahasibu na Wanasheria na nani wa kuendesha kile kiwanda. Iainishe ardhi itapatikana wapi? Labda heka mbili, heka moja, heka tatu, yaani vyote vikamilishe kwenye maandishi, iwe mradi umebuniwa, umekamilika. Baada ya hapo, itangaze kwamba tumebuni mradi wa kiwanda cha matairi ya pikipiki chenye thamani labda ya shilingi bilioni 100. Shilingi bilioni 100 ni sheli 100 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hao hao ambao ungewaweka kwenye sheli, kwa sababu hawana pa kuwekeza hela yao; mtu ana hela yake ya mtaji, anaona bora aende kwenye sheli, awekeze apate hela kidogo kidogo kuliko kukaa nazo akazitumia. Kwa hiyo, watakapokuja kununua hisa kwenye kiwanda ambacho kimebuniwa na TIC, watanunua hisa,

19 JUNI, 2024

watawekeza. Hiyo TIC isimamie, wabainishe utawala, watangaze kazi. Vijana wapo wengi wenye uwezo waliosomea mambo ya utawala, biashara, uhasibu na fani nyingine, waainishwe, waonekane kwamba wapo. Watangaze wauze hisa. Watakuja watu watanunua hisa halafu waanzishe kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo na wa *guest house*, na wa bodaboda, na miradi mingine ya huduma watahamia kwenye viwanda, vitakuwa vingi na tutakuwa tumetatua tatizo la ajira kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema, kupunguza shida ya ajira kwa vijana wetu na kuongeza uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko yapo kama nilivyosema. Nchi hii ina pikipiki sijui milioni ngapi, matairi kwa siku yanakwenda sijui mia ngapi au elfu ngapi? Tukiwa na kiwanda cha matairi, watauza vizuri vijana, viwanda vitauza vizuri. Tukishindwa kuuza hapa, siyo kushindwa, hata nje kuna masoko, utauza Uganda, utauza Rwanda, utauza Malawi, na kadhalika. Masoko yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kiwanda cha samani (*furniture*), tutauza kote tunakotaka kuuza, *material* zipo, mbaao zipo nchini hapa, watu watapata tija kubwa sana ya fedha zao. Kiwanda cha Ngozi labda viatu au mabegi, ngozi zipo, *raw material* zipo nyingi na wataalamu wapo. Naomba sana kitengo cha kuhamasisha viwanda kwa wazawa chini ya TIC, kianzishwe na kiratibu utaratibu huu ambao utasaidia sana kuongeza uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uzima nami kuweza kutoa mchango wangu katika hii Bajeti Kuu ya Serikali. Pia namshukuru sana Mheshimiwa

19 JUNI, 2024

Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya katika nchi yetu hususan katika Jimbo la Kilolo, kwa mambo makubwa na miradi mingi ambayo tunaendelea kuipokea na Wanakilolo wanamshukuru sana, kazi yake wanaiona na wanaendelea kujiandaa kwa ajili ya kutoa malipo 2025. *Inshallah Mwenyezi Mungu ajaalie. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Manaiibu Mawaziri, Wizara ya Fedha na pia Wizara ya Mipango. Kwa upande wa Wizara ya Fedha, kwa ushirikiano mkubwa ambao tunaupata hasa katika utengaji wa fedha na utoaji wa fedha. Tumepokea fedha nyingi sana za miradi na tunajua hii ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake. Sisi Wanakilolo tunawashukuru na kuwapongeza sana, kazi yao tunaiona na Mwenyezi Mungu awajaalie waendeleo kufanya kazi hiyo kwa uaminifu na uadilifu kwa ajili ya wananchi wa Tanzania pia kwa ajili ya wananchi wa Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Naibu wake kwamba wameanza vizuri, na sisi tupo tunaendelea kuwaangalia na kuwashauri kwa mambo machache yale ambayo tunaamini yatatoa mchango katika ujenzi wa Taifa letu. Siku hii ya leo, pamoja na shukrani na pongezi hizi, ninayo michango michache ninayoweza kushauri katika Bajeti Kuu. Jambo la kwanza kwa Waheshimiwa Mawaziri, ni kuhusu utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwa mazao ya misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajulikana wazi kwamba Mkoa wa Iringa ndiyo unaotoa mazao ya misitu ya kupandwa hasa mbao nyingi kuliko mikoa mingine mingi hapa nchini na wananchi wa Wilaya kama ya Mufindi na Wilaya ya Kilolo, hawana shida na ulipaji kodi. Wanapenda kulipa kodi na wasingependa kuingia kwenye migogoro na Serikali kuhusu ulipaji wa kodi hasa za mazao ya misitu. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo haiwezekani hii nchi kila anayezalisha mbao kuwa na mashine ya *EFD*, haiwezekani. Wazalishaji wa mazao ya misitu ni wazalishaji wadogo wadogo; mtu anajichangachanga, ananunua mashine, anaenda msituni, anachana mbao, anaweza akajaza gari moja au magari mawili, anaanza kupeleka sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ili tusilete udanganyifu wa wale wakulima, wanapokuwa wameshajaza gari, kuanza kumtafuta mwenye risiti ili wanunue risiti, badala ya wao kutoa risiti halali, ni vizuri mikoa inayozalisha mazao ya misitu, wale Mameneja wa *TRA* wa Mikoa na wa Wilaya, wakakaa vizuri na kuelekezana namna bora ya ukusanyaji kodi kwa mazao ya misitu bila kusababisha biashara haramu ya risiti ambayo inaleta usumbufu mkubwa na kusababisha udanganyifu ambao hauna tija yoyote kwa mkulima, wala kwa Serikali, wala kwa mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana pia Waheshimiwa Mawaziri hawa waagize Wizara zao kufanyia kazi haraka kwa sababu inatakiwa kuondoa ile kero ya wale wafanyabiashara haraka iwezekanavyo. Hili linawezekana kufanya majadiliano kwa sababu hamna aliyekataa kulipa kodi. Kwa mfano, gari kumi zinakamatwa, maana yake mwenye gari amekamatwa na gari yake haifanyi kazi. Wakati huo huo mwenye biashara amekamatwa, biashara yake imesimama. Hatuendelezi biashara, lakini hapo tunakwamisha tu uchumi na wale wafanyabiashara wa mbao wanapata shida, wafanyabiashara wa magari wanapata shida na hao wote hakuna hata mmoja aliyekataa kulipa kodi, bali ni utaratibu ambao hautekelezeki uliowekwa kwamba kila anayepakia gari ya mbao, awe na mashine ya *EFD* kitu ambacho hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawakera sana wananchi wa Wilaya ya Kilolo, Mufindi, wananchi wa Mkoa wa Njombe ambao wanafanya biashara ya mbao. Hii ni kero ya muda mrefu na tumeshalizingumza sana hapa Bungeni. Tunaomba lifanyiwe kazi ili liondoke, na kama kuna suala na

19 JUNI, 2024

utaratibu mzuri wa kodi, uwekwe ili jambo hili liweze kuondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hili na ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango pale wamenisikia, sasa naenda kwenye suala lingine linalohusu uwekezaji kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa na kumekuwa na majadiliano mengi ya changamoto. Natoa mfano mmoja wa changamoto ya sukari na asubuhi hapa limejibiwa swali kwamba Wilaya ya Kilolo ina eneo la hekta 10,000 zinazoweza kupandwa miwa. Wakati huo huo, tunavyo vyombo au mashirika ya Serikali ambayo yameshajitolea kutengeneza mitambo midogo ya kuzalisha sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamka hapa TEMDO ambayo ipo Serikalini, sasa, kama tusipowekeza kwenye kuhakikisha kwamba TEMDO inawezeshwa ili kuzalisha ile mitambo ya kuchakata sukari ili wale wakulima wadogo wapate hii mitambo midogo midogo, maana yake tunaendelea kuvutia uingizaji mwingi wa sukari na kwenye uchumi tunaondoa ile dhana ya *balance of payment* kwa sababu sisi tutanunua sukari nyingi, lakini wakati huo huo tuna uwezo wa kuzalisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara ya Mipango, ni kuangalia hizi taasisi ambazo zinajihusisha na uzalishaji wa mitambo. Nimetoa mfano wa kiwanda cha sukari na mitambo yake, lakini, pale TEMDO pia wanazalisha vitanda. Vitanda vile ni kwa ajili ya hospitali. Sasa ukienda kwenye bajeti ya mwaka 2023, tumenunua vitanda vingi sana vya hospitalini kutoka nje ya nchi na TEMDO wanazalisha vitanda hapa hapa nchini ambapo tusingetoa dola kwenda nje, tungeweza kuwawezesha TEMDO wakazalisha vile vitanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TEMDO ni ya Serikali, Serikali hiyo hiyo ndiyo ambayo imenunua nje wakati TEMDO iko pale na pengine uzalishaji wao wa vitanda ni vichache kwa sababu hatukuweza kuwawezesha kiuchumi. (Makofi)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yetu, tuangalie hizi taasisi zinazojihusisha na ubunifu na uzalishaji wa mitambo ili ziwezeshe kupunguza uagizaji wa bidhaa nje, halafu sisi tuzalishe wenyewe ili tuweze kuimarisha uchumi wetu. Kwa hiyo, mimi nimetoa mfano mmoja wa *TEMDO*, lakini ziko *SIDO* na taasisi nyingine na hizi zinafanya kazi nzuri kama zitawezeshwa, lakini zisipowezeshwa, ndiyo wanaweza kuzalisha vitanda kumi au mashine moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo mashine kwa mfano ya kupeleka Kilolo kwa ajili ya kujaribu uzalishaji wa sukari, bado hadi leo haijakamilika. Ni moja hiyo kwa sababu ya uwezeshwaji wa kiuchumi. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aipe *TEMDO* fedha izalishe. Ule mtambo wa kuzalishia sukari, ukafungwe pale Kilolo ili tujaribu tuone kama unafanya kazi vizuri ili na maeneo mengine ambayo wanataka kutengeneza sukari kwa viwanda vidogo, waanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutoe mfano huo. Mimi sijajua wanahitaji kiasi gani, lakini wakimletea Mheshimiwa Waziri, basi atoe hiyo fedha tukajaribishe ule mtambo naye mwenyewe pia ataona kwamba kuna manufaa kwa sababu tukitoa dola nje, tunapata hasara zaidi kuliko tukiwa tunazalisha ndani na dola zinabaki kwa ajili ya manunuzi. Kwa hiyo, tunakuwa na urari wa malipo ambao ni mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hili, nazungumzia suala lingine kuhusu dharura. Hivi karibuni kuna mvua nyingi sana zimenyesha na sisi wote tumeathirika. Nina hakika hata Waheshimiwa Mawaziri wote waliokaa pale ni Wabunge wa Majimbo na huko kwao mvua zimenyesha, maana mvua hazikuchagua kwamba huku ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Mipango, wala huku ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mvua zilinyesha nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya zile mvua kwisha, tumepata madhara makubwa sana ya uharibifu wa barabara. Tunapozungumzia dharura, maana yake ni dharura. Madaraja yakivunjika, maana yake watu hawapati huduma.

19 JUNI, 2024

Tunapozungumzia dharura, maana yake ni kwamba mazao yanaoza. Kuna watu wana mazao yao, walikopa, wanataka wasafirisha wakalipe madeni yao benki. Hadi hivi tunavyozungumza, bado fedha za dharura kwenye maeneo mengi kwa ajili ya barabara, hazijaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapofanya hivi, wakati wa bajeti, inabidi tuangalie. Tunaweza tukamlaumu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini sisi hapa kama Wabunge, na kama Taifa, ni lazima tuwe na utaratibu na mfuko maalum wa majanga yanapotokea, ili tunapompigia simu Mheshimiwa Jenista kwamba huku kuna janga na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wajue hiyo hela wanatoa wapi ili sisi kule tuweze kukubaliana na madhara kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hilo hatujalifanyia kazi, basi maana yake ni kwamba, hizi barabara itabidi zisubiri bajeti ya kawaida ambapo maana ya maafa, wala maana ya majanga haitakuwepo. Kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na Serikali kwa ujumla, ni kwamba, sasa tuanze kuangalia fedha za dharura zinatoka wapi? Mabadiliko ya tabianchi yanaendelea, kwa hiyo, tutaendelea kupiga simu kwamba huku kuna dharura, lakini je, fedha hizo za maafa hayo tunazitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, bado kuna kata karibu nne mpaka leo barabara hazipitiki, wananchi hawawezi kusafiri kwa sababu fedha haijaenda. Nikienda *TARURA*, watasema hatujapokea fedha kutoka Serikalini ambazo nami nikikaa nikitafakari, naanza sasa kuangalia, je, Mheshimiwa Waziri anazo hizo fedha? Kwa hiyo, naomba sana, kwa hii dharura iliyotokea, tufanye lolote linalowezekana fedha zipatikane huku tukiendelea kujadili kwamba tutapata wapi fedha za dharura kwenye miaka ijayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kuweka mfuko wa dharura, mfuko huo uwekwe ili wakati mwingine tusipate shida tunapopata madhara kwenye maeneo yetu, kwa sababu hicho ni kitu ambacho tunaweza tukakitabiri. Ndiyo maana tumeweka



19 JUNI, 2024

utabiri wa hali ya hewa na watabiri wengine wanaoweza kutabiri madhara. Sasa, yanapotokea, lazima tujue kinachoitwa dharura ni dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha akipokea simu ya dharura, anakaa siku ya kwanza, ya pili, ya tatu, mwezi, yeye mwenyewe anajua ni dharura, huwa anajisikiaje? Lakini pengine hana cha kufanya kutokana na kutokuwepo kwa fedha. Kwa hiyo, lazima hili sisi kama nchi na kama Bunge, tulifanyie kazi ili yale maeneo ambayo yana changamoto yaweze kutatuliwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kidogo jambo moja ambalo Wizara ya Kilimo inaweza kulirekebisha, lakini na nyie mnaweza kuliangalia. Tunazungumzia sana kuhusu mazao mbalimbali na jinsi ambavyo tunatoa unafuu, na hapa nimpungeze sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya ruzuku ya mbolea. Ruzuku ya mbolea imesaidia sana kwenye hii nchi hasa kwenye sisi ambao ni wakulima, tunajua manufaa ya ruzuku ya mbolea ambayo kama bei yake ingekuwa bila ruzuku, wakulima wengi sana wasingemudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna jambo moja kwenye baadhi ya mazao, tunahitaji kuwa na tathmini ya kutosha. Mfano, mazao ya parachichi ambayo sasa hivi yanaendelea kulimwa kwenye mikoa ya Njombe, Iringa na maeneo mengine. Bado wakati tunatoa bure miche ya michikichi, miche ya kahawa na miche ya mazao mengine, bado miche ya parachichi inauzwa tena kwa bei kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mipango na TARI wameshaifanya kwa ajili ya ruzuku kwenye miche ya parachichi. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, suala hilo lifanyiwe kazi na kwenye bajeti hizi, kama zipo fedha zitakazowekwa kwa ajili ya ruzuku, basi ruzuku kwa ajili ya miche ya parachichi iweze kuangaliwa, na tutakapofanya hivyo, tutaona kile kilimo kinakua. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, huko tunakoenda, uvunaji wa parachichi unaendelea kwa kiwango kikubwa. Wizara na Idara mbalimbali za Serikali zimekuwa zikija hapa kuelezea mipango jinsi walivyojipanga kwa ajili ya masoko ya zao la parachichi. Ni wakati muafaka sasa kuhakikisha kwamba upo mpango maalum wa kuwa-link au kuwaunganisha wakulima na masoko ya parachichi ili kusiwe na mkulima anapoteza mazao ya parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuharakisha ujenzi wa viwanda vya parachichi. Kwa Mkoa wa Iringa, najua kwamba kuna bajeti wa ajili ya kujenga kiwanda cha parachichi pale Nyororo Mufindi. Kwa hiyo, hicho kingeweza kusaidia mkoa mzima wa Iringa lakini pia na mkoa mzima wa Njombe kwenye hayo maeneo. Hilo nalo liangaliwe kwa haraka ili tusipoteze mazao haya, lakini ili tuendeleo kuwatia moyo wakulima wa parachichi ambao wanaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, kuna jambo wakati tunaendelea, tuliliangalia na tuliona linaweza likawa ni fursa ambayo haitumiki vizuri. Ni suala la uelewa wa halmashauri zetu kuhusu CSR (*Cooperate Social Responsibility*). Mashirika mengi yalioko kwenye maeneo yetu, hayatoi CSR kwenye halmashauri zetu, au kama yanatoa, hayatoi kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo tunapoteza mapato mengi kwa sababu CSR siyo hisani. Baadhi ya Wakurugenzi au maeneo mengi wanafikiri ni hisani kwamba mtu anatakiwa atoe CSR kwa hiari. Kwa kuwa ile ni sheria na ilipitishwa hapa Bungeni, ni wakati muafaka sasa wa kuwahamasisha na kuwapa maelekezo Wakurugenzi wote na wale wote wanaosimamia, kuhakikisha kwamba kila taasisi ya kibiashara inatoa CSR kwenye halmashauri husika na hapo itakusaidia Mheshimiwa Waziri, kupunguza kupeleka fedha kwa sababu kama CSR itatumika kujenga shule, maana yake tayari hapo bajeti ya Serikali imeokolewa. Kama CSR itatumika kujenga zahanati, maana yake hapo bajeti ya Serikali imeokolewa.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ufuatiliaji wetu kwenye Kamati, tuliona jinsi ambavyo kuna fedha nyingi sana inapotea kwenye eneo la CSR. Ushauri wangu ni kwamba tuendeleo kuangalia hilo eneo kwa sababu ni chanzo kizuri cha mapato na tunaweza kujenga nchi yetu kupitia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo lingine la wageni; tunao wageni 41 wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Wakuu wa Shule kutoka Babati Vijijini Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Naomba kuwasoma wachangiaji wa kwanza watakaanza leo mchana. Tunaye Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, ndiye atakayenza, atafuatia Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate. Tunaomba wale ambao mmepangiwa kuchangia, basi muwahi mapema saa kumi na moja kamili tuweze kuanza.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana wale wote ambao wamepata fursa ya kuchangia asubuhi hii. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kuendelea kupokea na kunukuu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Naibu Mawaziri.

19 JUNI, 2024

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Kikao cha Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na  
Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa  
Fedha 2024/2025  
na  
Makadirio ya Mapato na  
Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa  
Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja za Serikali: Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Hoja ya Waziri wa Fedha. Tunaendelea na majadiliano, nilimtaja Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatia Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na Mheshimiwa Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunifanya niwe mchangiaji wa kwanza kwenye session hii ya jioni. Kwanza kabisa naunga mkono hoja, lakini kwa kuwa mimi ni mkulima na Jimbo la Mbinga Vijijini na wananchi wangu ni wakulima, naanza mchango wangu kwa kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi hiki chote kukifanya kilimo ni kipaumbele kikubwa sana. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona kipindi hiki ndipo tuliposhuhudia bajeti kubwa ya Serikali kutoka shilingi bilioni 294 mpaka kufikia bajeti hii ya shilingi trilioni moja na zaidi, lakini kipindi hiki ndicho tulipoona mbolea ya ruzuku inapatikana, kipindi hiki ndicho tulipoona wakulima wetu wanatumia mbegu bora na za kisasa karibu kwenye kila zao. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kujitoa kimasomaso kweli kweli kwenye sekta hii ya kilimo na kuonesha sasa tunaweza kuona matunda ya uwekezaji huu mkubwa yanaonekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inasema hapa kilimo kimetutoa kutoka shilingi bilioni 2.4 mpaka shilingi bilioni 4.3 na ukizipeleka hizi fedha kwenye fedha za Kitanzania ni matriloni ya fedha. Kwa hiyo, naishukuru na kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kukishikilia sana kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayaji hivi hivi, yanakuja kutokana na utashi wa Rais tuliyenaye madarakani, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kukitua kilimo kutoka kule kilikokuwa na kukifanya kiwe cha sasa na chenye tija kwa wakulima wake. Tunamshukuru sana, lakini hatuwezi kuwaacha wasaidizi wake, hapa kipekee nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, amesimama kidete kusimamia mipango yote inayopangwa katika Wizara yake kuhakikisha kwamba inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona sasa hivi hata kelele za wakulima wale ambao wanauza mazao yao zimepungua sana. Zipo, lakini zimepungua sana. Pia tunaweza kuona mazao yanayolimwa yanapata masoko. Binafsi, kwenye jimbo langu sisi ni wakulima wazuri wa mahindi. Mahindi katika miaka hii mitatu yameendelea kuuzwa vizuri, na kwa bei nzuri. Mwaka huu tumeahidiwa hapa na Serikali kwamba wakulima watulie, wasiuze mazao yao kwa bei ya kutupa kwa sababu, Serikali ina mipango mizuri, inaenda kununua mahindi haya kwa bei nzuri.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge hili niwatangazie wakulima wangu wa Jimbo la Mbinga Vijijini wasiwe na haraka ya kuuza mahindi yao, kwa sababu nimeambiwa sasa hivi mahindi yanauzwa kwa kilo shilingi 300, kilo shilingi 350, hiyo bei bado iko chini, lakini Serikali kupitia Waziri wa Kilimo, ameongea hapa na ninajua kwenye kuhitimisha atatamka hapa kuhusiana na mahindi yatauzwa kwa bei gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natumia nafasi hii kuwashukuru sana na kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Sita. Nisiishie hapo kwenye upande wa kahawa, pia sisi wakulima wa kahawa kipindi hiki tumeuza kahawa kwa bei nzuri. Hatujafikia kule kuzuri zaidi, lakini ni bei nzuri kulingana na miaka ya nyuma. Tumeuza kahawa kuanzia shilingi 3,500 mpaka shilingi 8,000 kwa kilo. Ni bei kubwa sana. Upo mwaka ambao tuliuzwa kahawa kwa shilingi 8,000; upo mwaka tumeuza kahawa kwa shilingi 6,000, lakini mwaka uliopita bei ilifika shilingi 4,000 ni bei nzuri kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwa mipango iliyopo na taratibu zilizowekwa tunaweza kwenda kuuza kahawa kwa bei nzuri zaidi. Ombi langu hapa kwa Serikali, nimeona Serikali imefanya vizuri upande wa korosho, wenzetu wale sasa hivi mambo yao yanakwenda vizuri sana. Pia Serikali imefanya vizuri kwa kahawa upande wa *robusta*. Wenzetu wale sasa hivi hawana malalamiko, lakini sisi wakulima wa Mbinga Vijijini bado tuna shida kidogo. Kahawa tunauza, lakini bado baadhi ya wakulima malipo yale hawayapati, na kama wanayapata, basi ni kwa kuchelewa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali vile ilivyofanya kwenye upande wa wakulima wa *robusta* mkoani Kagera, wakulima wale wakiuza kahawa hawachukui muda mrefu kupata malipo yao na wanapata malipo yao kwa mkupuo. Naomba vivyo hivyo utaratibu uliotumika kule Kagera basi uje utumike pia, kwa sisi wakulima wa *arabica* Wilayani Mbinga, kwa sababu, tunalima, tunauza, lakini tunapata dosari kidogo.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko baadhi ya AMCOS ambazo hazibalipi wakulima. Hivi ninavyoongea wako baadhi ya wakulima ambao bado wanadai malipo ya msimu uliopita na tayari msimu huu uko jirani sana kwenda kuanza. Kwa hiyo, naomba kupitia utaratibu huu ambao Mheshimiwa Waziri ameufanya, ameusimamia kwa Mkoa wa Kagera, basi vivyo hivyo ausimamie upande huu wa Mkoa wa Ruvuma, hususan Wilaya yetu ya Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo kwenye suala hili la viwanda, niliongea muda ule wa Bajeti ya Kilimo, niliongea pia muda wa Bajeti ya Viwanda kuomba viwanda kwenye Wilaya ya Mbinga. Sisi ni wazalishaji wazuri wa mahindi haya. Tuweke viwanda pale, hivi viwanda ambavyo kwenye mpango wetu wa awamu hii umeonesha. Mheshimiwa Prof. Kitila amesema hapa anaenda kuanzisha viwanda vidogo vidogo vikiwemo viwanda vya unga, ili mahindi yetu sasa sisi wakulima wa Mbinga, tusiyauze kama mahindi yenyewe, tuuze unga. Najua unga una thamani na unga utatupa fedha zaidi kuliko kuuza mahindi ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana jambo hili Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa sababu, tayari imejionyesha kuwasaidia wakulima basi, i-set viwanda kwenye maeneo haya ya uzalishaji, hasa Wilaya ya Mbinga, tunazalisha mahindi mengi. Watuwekee viwanda pale vya unga, watuwekee viwanda pale vya kahawa ili mwisho wa siku sasa malighafi yetu tuisage, tuuze sasa mali iliyo sahihi zaidi kuliko mazao yenyewe. Naomba sana suala hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niongelee suala la utekelezaji wa miradi. Naipongeza sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa utayari wa kupeleka miradi kwenye maeneo yetu. Ni miradi mingi sana; niitaje michache kwenye Wilaya yangu au kwenye Jimbo langu. Mimi nina Mradi wa Ujenzi wa Barabara kutoka Kitai – Amanimakoro – Ruanda mpaka Lituhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara kutoka Amanimakoro kuelekea Ruanda tayari mkandarasi yuko *site*, lakini kasi ya utekelezaji mradi huu iko nyuma sana. Mradi huu tulikuwa

19 JUNI, 2024

tukabidhiwe tarehe 18/12/2024, lakini mpaka ninavyoongea hapa bado mkandarasi hajaanza kuweka hata doti ya lami. Wananchi wangu wamenituma hili nilisitize hapa. Barabara hii ndiyo inayopitisha makaa ya mawe, ndipo mahali ambapo uzalishaji mkubwa wa makaa ya mawe unatokea. Kwa hiyo, ni barabara ya kiuchumi na ni barabara inayoiingizia fedha nyingi nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hii Serikali ya Awamu ya Sita ambayo iko tayari kujenga hii barabara iharakishe kupeleka fedha kwa mkandarasi yule ili barabara ijengwe na ikamilike. Nashukuru kipande cha pili kuanzia Ruanda kwenda Lituhi hadi Ndumbi ambako tumejenga bandari nzuri ya kisasa, tayari tumeingia mkataba na mkandarasi. Sasa naomba nako tupeleke fedha kwa haraka kwa mapema ili sasa kinapokamilika kipande hiki cha kilomita 35 basi na kile kipande cha pili cha kilomita 50 hadi 60 kikamilike ili barabara yote iweze kutumika kwa manufaa ya kukuza uchumi upande ule wa kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo tuna barabara inayotoka Songea hadi Makambako. Barabara hii ni muunganiko wa barabara inayotoka Ndumbi - Mbamba Bay kufika Songea, lakini ije sasa Makambako mpaka Dar es Salaam kupeleka malighafi hizi. Barabara hii na wewe utakumbuka kwa sababu inakugusa katika kipande pale, imetamkwa muda mrefu, mpaka leo hii hatuoni ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali yetu hii sikivu kwa sababu shida hapa ni fedha hazijaenda, itoe fedha barabara hii ianze kujengwa. Hali ya barabara hii sasa hivi ni mbaya sana, muda wowote tutahatarisha hali za watumiaji wa barabara hii. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali hii sikivu, naomba Mheshimiwa Waziri Nchemba, yuko vizuri, atulettee fedha kwenye hii miradi ili ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni mradi wa Umwagiliaji, Litumbandosyi ambao tumekuwanao na uko miongoni mwa miradi ile 19. Eneo hili tunazalisha sana mpunga, lakini tukipata huu mradi, ukikamilika, maana yake ni uwezo wetu



19 JUNI, 2024

wa kuzalisha utaongezeka na wananchi wetu watapata kipato kikubwa kwa sababu, watakuwa na uwezo sasa wa kuzalisha siyo kwa mwaka mara moja, bali wanaweza kuzalisha hata mara mbili kadiri mlivyotupangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tulikuwa tuanze kutumia ule mradi, lakini bado na wenyewe unakwenda kwa kasi ya chini sana. Naomba sana mradi huu upelekewe fedha na wenyewe tuanze kuutumia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha kipaza sauti. Nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya, ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai na Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu siku ya leo. Naanza kwa kusema naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, Hoja ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji, pamoja na Hoja ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa kwenye Jimbo langu la Maswa Magharibi kwenye mradi mmoja wa maji. Mheshimiwa Rais ametupatia fedha kwenye maeneo mengi; elimu, afya, kilimo na barabara, na vitu vingi tumepewa. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kipekee kabisa kwenye mradi huu wa maji kwenye jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mkoa wetu wa Simiyu tuna mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa Wilaya zote tano, lakini kwenye Wilaya ya Maswa upande mmoja ndiyo ulikuwa ule

19 JUNI, 2024

mradi wa maji unaishia. Kwa hiyo, ule upande wa pili ambao mimi niko, hatukuwa na chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria, lakini nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuwa juzi juzi mkataba wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyaleta kwenye Mji wa Malampaka na hatimaye Mji wa Malya na Vijiji vilivyo karibu umesainiwa, na mkandarasi yuko *site*. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, ameniondoa kwenye uyatima wa maji ya Ziwa Victoria kwenye Jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi mbili. Hawa mimi naweza kusema tuwaite *Singida Boys*. Kwa kweli, wamejitahidi, wameweka juhudi kubwa kwenye mpango na kwenye bajeti yenyewe. Juhudi mliyoweka ndani yake kwa kweli matunda yake tumeyaona na ni kazi nzuri. Pia nawapongeza Manaibu wao, Mheshimiwa Chande, Naibu Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Stanlaus Nyongo, mdogo wangu, Naibu Waziri wa Nchi kwenye Wizara ya Mipango na Uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mambo haya mliyoyapanga yakitekelezwa tunaweza kabisa kupiga hatua pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge watakaotoa. Naamini kabisa sisi kama nchi tutapiga hatua ya kimaendeleo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na kilimo kwa sababu na mimi ni mtu wa kilimo na jimbo langu lote kazi kubwa wanayofanya wananchi wangu ni kilimo. Naanza kwanza kwa kuishukuru Serikali kwa miradi ya umwagiliaji kwenye jimbo langu; Mradi wa Umwagiliaji wa Masela, Mradi wa Umwagiliaji wa Bukangilija, naambiwa unapata fedha kwenye bajeti hii tunayoijadili. Basi namshukuru sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, kwa kufikiria kupata miradi ya namna hiyo kwenye Jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu kwa sababu, mpaka leo Watanzania tulivyo tunapata chakula kutoka kwenye kilimo, mpaka leo tunapata malighafi za viwandani kutoka kwenye kilimo, pia tunapata fedha za kigeni

19 JUNI, 2024

kutoka kwenye kilimo, na tunapata ajira kubwa ya Watanzania kutoka kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sana ambacho kwenye taarifa za Waheshimiwa Mawaziri tunaojadili hoja zao wametaja mchango wa sekta ya kilimo kwenye ukuaji wa pato la Taifa kuwa ni mkubwa kuliko mchango mwingine wowote. 26.5% ni mchango mkubwa sana, lakini tujaribu kuangalia sasa kibajeti sekta hii kwa upana wake kwa maana ya kilimo cha mazao na mambo mengine, lakini ukaleta mifugo pia, na uvuvi. Bajeti iliyopangwa hapa ni ndogo sana. Nimejaribu kufanya hesabu, ni kama asilimia nne tu ya bajeti ambayo tunaijadili hapa ndiyo inaenda kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa nilidhani tungefikiria kukipa kilimo rasilimali fedha nyingi zaidi kuliko maeneo mengine kwa sababu mchango wake ni mkubwa. Kwa kuweka asilimia nne tuliyoweka sasa hivi na huku nyuma ilikuwa ipo chini asilimia tatu na kidogo, lakini bado mchango wake kwenye ukuaji wa Taifa ni asilimia kubwa zaidi, 26.5%. Sasa tungeongeza asilimia nne nyingine kwa mfano, nadhani mchango wa sekta hii ungekuwa ni mkubwa zaidi na hivyo sekta hii ingeweza kuchangia zaidi kwenye fedha za kigeni, kwenye ajira za Watanzania, kwenye chakula kwa ajili yetu kama Watanzania, pia kwenye viwanda kwa malighafi za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama Taifa tuanze kufikiria huko tunapoelekea mbele, tunafanyaje na sekta hii ambayo inatupatia maziwa mengi zaidi kwa kuipa majani kidogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya suala la bei za mazao. Mwenzangu Mheshimiwa Kapinga aliyemaliza kusema kabla yangu anashukuru kwa ajili ya bei za mazao anayolima kwenye eneo lake, lakini mimi bei ya zao la pamba kwenye eneo langu bado ni kidogo. Kusema kweli bei za mazao yetu ya kilimo tunabahatisha, kwa sababu tunategemea soko lile la nje. Sasa soko likiwa zuri bei zinapanda, soko likiwa chini, basi bei zinaanguka. Sasa ndivyo ilivyofanyika kwa zao la pamba. Mwaka

19 JUNI, 2024

huu bei ni shilingi 1,060 imepandapanda kidogo nimeambiwa ni shilingi 1,200 mpaka 1,300 sasa hivi kwa sababu ya ushindani bei, lakini bado ipo chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tunaloambiwa ni kwamba kwa sababu tunauza mazao yetu nje, tunategemea soko la nje. Sasa hii ni sababu kongwe mno kwa Taifa letu. Toka zamani tunaambiwa ni kwa sababu ya kuanguka kwa bei ya soko la dunia, basi mazao yetu pia yanaanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sasa Serikali ikaja na mpango wa namna ya kuwazawadia wakulima wa nchi hii ambao wanatusaidia katika mambo mengi. Kuna haja ya kuja na Mfuko wa Kilimo ambao ndani yake tutakuwa na Mfuko wa Fidia ya Bei za Mazao za Wakulima wa nchi hii. Kwa sababu tusipofanya hivyo, tutaendelea kuishi na soko la dunia. Sasa ili tuishi nalo vizuri, sisi kama nchi tufikirie namna ambavyo tunaweza kuwazawadia wakulima wetu kuliko kuiachia dunia ifikirie namna ya kuwazawadia wakati ndio hao wanatulisha, wanatupatia ajira na wanatupatia fedha za kigeni. Kwa mfano, tuna Mfuko wa Reli, REA, Maji, tumeshindwaje kuwa na Mfuko wa Sekta ya Kilimo? Mimi nadhani inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoke hapo kwenye kilimo niende kwenye suala la pili. Sekta isiyo rasmi katika nchi yetu sijaona imetajwa sana kwenye mpango, na hata kwenye bajeti. Sekta isiyo rasmi kwenye nchi yetu kwa mujibu wa utafiti wa Timu yetu ya Takwimu ya Taifa inachukua 46% ya shughuli zinazofanywa na Watanzania. Sasa hii ni kubwa mno na kwa Mkoa wa Dar es Salaam 58% ya kaya zilizopo Dar es Salaam zinajihusisha na sekta isiyo rasmi. Nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, hii sekta isiyo rasmi haijasajiliwa, hatujaitambua sana na pengine shughuli zake zinaweza kuwa zina mtaji mkubwa. Kwa mfano, utafiti uliofanyika Dar es Salaam mwaka 2019 unaonesha kwamba, mtaji uliowekezwa kwenye sekta isiyo rasmi kwa Dar es Salaam ni shilingi bilioni 901.7. Hizo ni pesa nyingi. Hii ni fedha ya kutosha kabisa. Sasa bado tunapokuwa na sekta isiyo rasmi kubwa namna hii, siyo

afya kwa uchumi wetu na kwa mapato ya Taifa letu kwa sababu kuna mapato ambayo hatuyapati kutoka kwenye mtaji mkubwa wa namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Serikali ije na sera zinazovutia sekta isiyo rasmi, iwe rasmi. Serikali ije na sheria na taratibu zilizo rahisi za usajili wa biashara hasa mpya ili kwamba sekta hii isiyo rasmi ambayo inahusisha gereji, bodaboda na vitu vingi mbalimbali ambavyo tunaona kama vina faida ndogo, lakini ni kubwa vikijumuishwa kwa pamoja. Sekta hii isiyo rasmi iwe rasmi na iweze kuchangia mapato ya Taifa letu kama ambavyo sisi wote tunatamani tuwe na kipato kikubwa kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mikakati ya kimsaada kwa ajili ya mafunzo na mikopo kwenye sekta hii. Mikakati mingine ni pamoja na motisha za kikodi. Motisha za kikodi zinaweza zikafanya hawa watu wanaokimbia kuwa rasmi wakaja wakawa rasmi. Sasa tofauti na ilivyo sasa hivi, mtu akionekana tu kidogo ana biashara yake ndogo tayari halmashauri na TRA wanaenda pale. Sasa tuje na motisha za kikodi ambazo zitasababisha hawa watu wapende kuwa rasmi badala ya hali walionayo ya kutokuwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la tatu juu ya ajira. Ajira bado ni tatizo kwenye nchi yetu. Watoto wetu wengi wanaomaliza vyo hawajaajiriwa na kwa hili kila mmoja hapa ni mwathirika kama familia na pia kama Taifa. Takwimu nilizonazo zinaonesha ajira za kudumu zimeajiri Watanzania 18% tu, ajira za muda wa kati zimeajiri Watanzania 10%, pia ajira za muda mfupi zimeajiri Watanzania wengi zaidi kama 72%. Sasa hizi ajira za muda mfupi ni ajira ambazo hazina uhakika kwa sababu ni miezi mitatu, sita au mwaka mmoja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni juu yetu kuhakikisha sekta zile zinazoajiri watu wengi zinapata rasilimali fedha ya kutosha ili ziweze kutengeneza ajira ya kutosha kwa ajili ya watu wetu. Naona Mwenyekiti umewasha

19 JUNI, 2024

*microphone* yako. Vinginevyo tutazungumza habari ya ajira, lakini kama tusipokuja na mkakati ambao ni sahihi kwa ajili ya kutibu tatizo la ajira, bado tutaendelea kulia na hili tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana kwa kunipa nafasi, nakushukuru sana na nirudie tena kusema naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, atafuatia Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili hasa ndugu zangu hawa wawili, mimi sitawaita *Singida Boys* ila nitawaita watani wangu kwa sababu *they are no longer boys*. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimepitia Hotuba ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha ameenda kwa jinsi ambavyo Waziri wa Mipango na Uwekezaji amefikiria. Kwa hiyo, naye amepanga kwa mikakati ya ushuru pamoja na kodi kwa sababu Waziri wa Mipango yeye anapanga nini kinachotakiwa, lakini Waziri wa Fedha anaenda kutuambia kwamba ni kwa namna gani tunapata fedha kwa ajili ya *ku-finance* Mipango ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025. Kwa hiyo, nawapongaza sana kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia mmetuonesha njia, lakini najaribu kuangalia kwamba katika dunia ya sasa hivi au Tanzania, hatujawahi kuwa na tatizo la mipango, kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Alexander Mkumbo. Tatizo letu ni katika utelelezaji wa mipango yetu kwa sababu kupanga na kutekeleza ni vitu viwili tofauti sana.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia Hotuba ya Waziri wa Mipango, amesema kwamba ni lazima tulinde viwanda vyetu vya ndani, lakini kwenye ushuru nimejaribu kupitia kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha ameondoa baadhi ya tozo na ushuru kwa baadhi ya bidhaa ambazo zinazalishwa nchini ambazo zinalinda viwanda vyetu. Kwa mfano, viwanda vya bati, nimeona pia nondo na vifaa vingine vya chuma, Waziri wa Fedha ameondoa ushuru pamoja na ushuru wa forodha na maeneo mengine kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu. Nawapongeza sana kwa hilo kwa sababu mmejithahidi. Hatuwezi kukusanya kodi kama hatuna watu ndani ya nchi yetu ambao wana uwezo wa kuzalisha pamoja na kupata fedha ambazo Serikali inaenda kupata kodi kutoka kwao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuendeleo kuwasaidia Watanzania wanaowekeza mitaji yao ndani ya nchi yetu ili Watanzania wanunue bidhaa zao pamoja na wao kupata fedha ambayo Serikali itapata kodi kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kauli moja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kuna kauli moja hapa ambayo alisema wakati anasoma hotuba yake, inahusiana na wafugaji. Kauli hiyo inasema kwamba, “Mtu mwenye ng’ombe 9,000 kutokulipa kodi na kutaka kujengewa joshu au bwawa kwa ajili ya mifugo yake kwa kodi ya mtu mwenye kipato cha shilingi 300,000 kwa mwezi, siyo sawa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa Tanzania au wafugaji wa Tanzania ninaowajua mimi nafikiri kama kuna mtu mwenye ng’ombe 9,000, labda kwa mfano nichukulie kwenye Jimbo la Ngorongoro ninapotokea, sijui mtu yeyote mwenye ng’ombe hata zaidi ya 1,000. Leo hii, kauli hii *is too general*, na akasema kwamba; “Napendekeza kila halmashauri zenye idadi kubwa ya mifugo kuratibu ushirika wa mifugo na kuanzisha mfuko wa kuendeleza huduma za ugani za mifugo na miundombinu ya mifugo kama majosho kwa kutumia mifuko hiyo na magari ya Serikali ya kuchimba mabwawa na visima yaliyopo mikoani mwetu. Vyama vya wafugaji wakubaliane kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa mifuko hiyo, kama inavyofanyika kwa vyama vya

ushirika kwenye mazao kwa mfano, korosho, tumbaku, pamba na kadhalika.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni wapi ruzuku inatolewa kwa wafugaji, lakini naamini kwa wakulima mnawapa ruzuku ya mbolea. Kwa mfano, leo sisi wafugaji tunapata wapi au sisi kuwa na mifugo imekuwa ni tatizo? Kwa sababu kwa nchi hii mfugaji naye ni mtu anayejitegemea, hutegemea mifugo yake kuanzia mwaka mmoja anapozaliwa mpaka anapofikisha miaka sita ndiyo ana uwezo wa kuuza ili apate mapato kutokana na ile mifugo. Unajua ni gharama kiasi gani kwa mfugaji kutunza mfugo mmoja kutoka mwaka wa kwanza mpaka mwaka wa sita? Anatumia siyo chini ya shilingi 300,000 halafu baadaye anauza shilingi 600,000 kwa ng'ombe mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha tusitumie hii *generalisation* kwa ajili ya kwenda kuwahukumu wafugaji wote wa Tanzania. Ni lazima tuangalie, tufanye *study* kwamba ni wafugaji wangapi ambao wana mifugo mingi? Hakuna mtu ambaye anakataa kwa sababu wafugaji nao wanalipa ushuru na kodi. Anapoenda dukani kununua dawa, analipa kodi. Hata anapoenda mnadani kuuza mfugo wake analipa ushuru. Kwa hiyo, tuangalie namna ambayo tutawatengenezea wafugaji wa Tanzania njia ambayo itatuletea manufaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imependekeza kwenye malipo ya *export permit* kwamba iwe kutoka shilingi 30,000 *which* kwa kawaida siyo shilingi 30,000, ni shilingi 25,000, ikaenda kwenye shilingi 31,000. Nadhani, kama tunataka ku-*discourage* watu kuuza nje mifugo, tutengeneze mazingira ya ndani ambayo tutahakikisha kwamba Serikali inakuja na bei elekezi ya mifugo na wauze kwa kilo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwenye mapendekezo yote ya ushuru pamoja na kufuta au kutoa unafuu, sijaona eneo lolote ambalo linatoa unafuu kwa vifaa vya viwanda vya uchakatji wa mazao ya mifugo ambayo ingesaidia pia wafugaji



19 JUNI, 2024

kuweza kuuza mifugo yao au kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naishauri Serikali ije na mpango ambao tutaanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo Tanzania ikiwepo nyama, maziwa pamoja na mazao mengine. Pia tuwe tunauza mifugo yetu kwa bei, badala ya kwenda sokoni na kukadiria bei ya mifugo, hiyo haitawanufaisha wafugaji wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa Mheshimiwa Waziri wa Mipango, kwa sasa kama Tanzania tunataka kwenda kwenye uchumi wa kidijiti, mawasiliano ni kitu cha muhimu, lakini kwa Tanzania maeneo mengi hayana mawasiliano ukitoka mkoa mmoja kwenda mwingine. Hakuna mkoa utasafiri Tanzania kukawa na mawasiliano, labda kilometa 100 mpaka 200. Ni lazima tuone ni namna gani ambapo kwa Tanzania hii tunawajengea watu uwezo kuwepo na mawasiliano na *internet* kwa kila mkoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunataka kuhamasisha wananchi wawe wanatumia lipa namba; kuna maeneo mengi Tanzania hapa hawana mawasiliano. Sasa ni lazima tufikirie ni namna gani ambayo Watanzania wanaweza kuwa na mawasiliano. Kwa mfano, kwenye Wilaya yangu ya Ngorongoro kwenye kata 28 kata ambazo zina mawasiliano ni kata 10 tu na siyo kote, ni *partially*; kijiji kimoja kinayo, kijiji kingine hakina. Kwa mfano, Kata ya Sale, Loswashi, Tinaga, Njoroi, Naan, Oloipiri, Karkamoru, Piyaya, Naiyobi, Ngoile, Kakesio, Meshil, Naiyobi, na maeneo mengine hakuna mawasiliano. Sasa hawa wananchi tutawezaje kuwashawishi waweze kwenda kwenye *digital economy*? Kama hawawezi kuwasiliana, hawawezi kufanya *transaction*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine kwenye Jimbo langu la Ngorongoro, tunataka barabara ya lami kutoka Sale mpaka Kigongoni. Kwenye wilaya yetu bado kuna tatizo kubwa la usafirishaji. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini anajua, walikuja na Naibu Waziri Mkuu aliacha *bumper* la gari yake

19 JUNI, 2024

Ngaresero. Nampongeza Naibu Waziri Mkuu kwa sababu alikuja kwa gari mpaka Loliondo, ameona changamoto iliyopo, lakini baadaye ilibidi waruke na ndege kwa sababu hawawezi kufika Arusha tena kwa magari yao. Sasa hawa wananchi wa Ngorongoro tuwasaidie nao wapate barabara ya lami waweze kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyenijaalia uzima kusimama tena kwenye Bunge lako Tukufu. Pia nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kwa ushirikiano ambao wanaendelea kunipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanza na Deni la Taifa. Kukopa siyo dhambi na nchi zote zinakopa hasa nchi zinazoendelea. Najua haki hiyo tunaipata kwenye Katiba yetu Ibara ya 141(i) – (ii) ambacho kinasema Deni la Taifa litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Ibara hii, Deni la Taifa maana yake ni deni lenyewe na pia faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni polepole na gharama zote zinazoambatana na usimamizi wa deni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie tu kwenye usimamizi. Kwa kuwa tuna haki ya kukopa, lakini kama Bunge tuna wajibu wa kushauri juu ya mikopo tunayokopa. Kama ambavyo nimeanza kuzungumza, kukopa siyo dhambi wala siyo kosa, lakini tunakopa fedha hizo kupeleka kwenye miradi gani?

19 JUNI, 2024

Kama Taifa tunanufaikaje na mikopo hiyo? Watanzania wananufaikaje na mikopo tunayokopa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Serikali kuona kwamba kuna umuhimu sasa pamoja na kwamba bado tunakopesheka, lakini tuangalie, lazima kama Taifa tuwe na mtazamo kwamba tunakopeleka fedha hizo kuna wakati kama Taifa tutahitaji kule ambako tumepeleka sasa fedha hizo tuweze kujiendesha kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikopa tukapeleka kwenye miradi ya uzalishaji siyo kosa, tunaenda kuzalisha ajira kule lakini miradi yenyewe ile itachangia baada ya kuzalisha kuendelea kujiendesha kama Taifa. Mimi siyo muumini sana, pamoja na kwamba tuna changamoto ya vyoo mashuleni, tunayo changamoto ya madarasa, siyo muumini wa kusema fedha tunazokopa kwa gharama kubwa tupeleke kujenga vyoo shuleni, isipokuwa tukikopa fedha tukapeleka kwenye miradi ya uzalishaji, miradi hiyo ambako tumepeleka, kama ni kwenye kilimo tunajua tukizalisha tutaenda kujenga vyoo, tutajenga madarasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna madarasa ambayo tulijenga kipindi cha COVID, yaani shule hazijamalizika yale madarasa wanayojenga yameshaweka ufa, lakini hayo madarasa lini yata-*mature* ili tulipe deni? Kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali na niko hapa kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia leo tumewekeza kwenye kilimo, ni jambo jema, nami naunga mkono kwa sababu tunaamini kwenye kilimo kuna uzalishaji. Leo tumeweka ruzuku kwenye mbolea, ni jambo jema kwa sababu tunataka Watanzania wengi wapate mbolea wazalishe na Taifa liendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri kidogo tu. Pamoja na ukuaji ambao kwa sasa sekta ya kilimo inachangia kwenye pato la Taifa, leo tuna Watanzania wengi ambao wanatamani kulima zaidi ya ekari 100 na kuendelea, lakini nini tunaweza tukafanya? Ni wajibu wa Serikali kuweka vizuri kwenye mipango

19 JUNI, 2024

sasa. Hapa tumeona Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Prof. Kitila, watu wangu wa Nkasi kule hawana shida na hizo taaluma zenu, wanataka wazione taaluma kwa kuenda angalau kubadilisha maisha yao ya sasa. Naamini Mheshimiwa Rais kuwateua hakufanya bahati mbaya, tunataka tuone ushauri utakaoendana na taaluma zao kwenda kusaidia maisha ya Watanzania kutoka kwenye ugumu wa maisha waliyonayo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kama mtu ana-trend ya miaka mitatu, ananunua mifuko 200 ya mbolea ambayo ina ruzuku, ni kwa nini mkulima huyo, kwa sababu mmeshaona trend yake, usitengenezwe utaratibu akapewa mbegu, akapewa na mbolea akaja kulipa baada ya mavuno? Kwa sababu tutakuwa tumemwongezea uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu natambua wapo wakulima ambao anatamani hata shilingi 70,000 hana, kwa sababu nchi yetu hatuna shida ya maeneo ya kulima, lakini watanzania hao wanahitaji kuwezesha ili nao watoke kwenye zile sekta wanazozita siyo rasmi. Kwa sababu, tunajua ni wajibu wa kila Mtanzania kulipa kodi, lakini tuchukue kodi ambazo ni halali. Kodi ambazo tumewatengenezea mazingira rafiki ya uzalishaji ili waweze kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo muumini wa zile kodi ambazo tunafikiri tunataka kujaza idadi, mimi ni muumini wa wananchi waliowezeshwa mazingira rafiki watimize wajibu wao wa kikatiba kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia kwenye kilimo tu, nitolee mfano tu wa Mkoa wa Rukwa. Tuna maeneo mazuri sana yanayofaa kwa kilimo. Sisi hata kwenye mabwawa, fedha ambazo zinatumiwa, sisi tuna Ziwa Tanganyika, tunahitaji fedha tukawawezeshe vijana wetu ambao hawana ajira waende kwenye kilimo cha umwagiliaji, tuachane na kilimo cha kutegemea mvua kwa mwaka mara moja. Hao Watanzania wapo. Nini ambacho hakijafanyika? Ni wajibu wetu sasa na yeye Mtanzania wa Nkasi aone mkopo uliokopwa safari hii, nami

19 JUNI, 2024

mwana-Nkasi nimenufaika na huo mkopo. Kitu ambacho nakiona kwenye nchi yetu, kwanza ni mipango. Hiyo mipango tunayopanga ni namna gani inaenda kuwanufaisha wananchi moja kwa moja kule chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitolee mfano tu. Nilizungumza jambo moja kwenye hoja ya dharura hapa ukaniambia nitazungumza leo, ninaenda kulisema sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi hatujawekeza sawasawa. Hapa ninapozungumza, eti mipango yetu tumejikita kupumzisha ziwa kwa miezi mitatu. Kwa sababu gani? Samaki wamepungua. Kwa hiyo, ukifunga miezi mitatu, samaki wanajaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miezi mitatu, ukifungua, uvuvi haramu utaendelea na wale wavuvi haramu ndiyo watanufaika na huo uvuvi, badala ya sisi kufikiri kuongeza pato kupitia uvuvi, tuwawezeshe hawa wananchi wetu. Tumeamua kuweka vizimba, sawa; vyakula ni bei ghali. Kwa nini msiwakopeshe hivyo vyakula? Vyakula vyenyewe vinatoka nje ya nchi! Ili tuone fedha tuliyowekeza kwenye uvuvi, tumeweza kuongeza pato la Taifa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufunga miezi mitatu ni mawazo mgando. Mimi sikubaliani hata siku moja, kwa sababu tutafungua, samaki wataonekana wamejaa. Wamejaa mwezi huu, anayenufaika ni yule ambaye anatumia uvuvi haramu. Atavua zaidi kuliko yule ambaye amelipa leseni, kalipa kodi zote za nchi hii, atapata mavuno ndani ya wiki moja, tunarudi kule kule samaki wamefanya nini? Wameisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na hayo mawazo, lazima tuwe na mpango endelevu wa namna gani tutatunza maziwa yetu makuu? Namna gani tutawainua wavuvi wetu? Aliyekuwa anapata angalau pato la shilingi milioni mbili kwa mwaka, tutegemee kwamba baada ya pale anaweza kupata shilingi milioni nne. Huyo tutamwambia unatakiwa utoke pale ulipokuwa unalipa kodi, uongeze kiwango cha kulipa kodi. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyozungumza hapa, hiyo miezi mitatu, Watanzania wenye haki ya kufanya shughuli halali ya uvuvi wa Ziwa Tanganyika wamefungiwa kwa sababu ya maamuzi ya mamlaka. Wamelipa leseni, hakuna siku tumetenga fedha ya kuwapa kwa kipindi cha mpito hawa Watanzania, ni kwa sababu hawana sehemu ya kusema. Kwa nini tunafanya mambo hayo? Bado tunasema alipe kodi; amelipa kodi. Ie kodi siyo halali, mmemnyonya huyu Mtanzania, tumempa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu ameenda kukopa fedha benki, lakini tulichokifanya ni kutumia nguvu yetu ambayo tunayo ya mamlaka kuhakikisha huyu Mtanzania anakosa haki yake halali. Narudia kusema tena, chanzo kikubwa cha nchi yetu pamoja na kukopa kwa nia njema, shida kubwa ya nchi yetu ni usimamizi wa fedha, nidhamu mbovu ya fedha kwenye Taifa letu, kuna upotevu mkubwa sana wa fedha. Kila ripoti ya CAG kuna upotevu wa fedha. Tujikite hapo tuweze kuzuia mianya ya upotevu wa fedha ili tuweze kuiona fedha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, pamoja na upotuvu wa fedha, hata vyanzo tulivyonavyo tunakusanya sahihi? Bado kuna shida kwenye nchi yetu. Ukusanyaji tu ni changamoto, lakini hata kile kinachokusanywa kinakwenda sehemu ambayo inatakiwa kwenda hiyo fedha? Bado kuna shida kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kushauri kwa nia njema, changamoto kubwa ya nchi yetu pamoja na kukopa fedha ni usimamizi mbovu wa fedha hiyo na mianya mingi ya upotevu wa fedha. Kama nia ni njema, lazima tuangalie, hatuwezi kukopa miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kushauri kwa nia njema, nchi ni yetu, tukope fedha tupeleke kwenye maeneo ya uzalishaji ili tuweze kulipa hayo madeni na baadaye kama Taifa tuweze kujiendesha. Tusikope kama *fashion*, tukope tukiamini siku moja kama Taifa hili tunaweza kujiendesha wenyewe. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, labda kwa vile Waziri wa Fedha upo hapa, uzoefu unaonesha huu mkakati wa kuwekeza kwenye vizimba hauwezi kufanikiwa kama hamta-address gharama ya chakula cha samaki. Kwa hiyo, ni vizuri mkafikiria kodi kwenye vyakula ambavyo vinaingizwa, kwa sababu asilimia kubwa ya gharama za uwekezaji huu upo kwenye chakula cha samaki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatia Mheshimiwa Sebastian Simoni Kapufi na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hii nafasi ya kuchangia kwenye bajeti ya Serikali yetu. Awali ya yote niwapongeze Mawaziri husika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Mipango; na Naibu Mawaziri wao, Mheshimiwa Chande na Mheshimiwa Nyongo kwa namna ambavyo mmewasilisha bajeti hii nzuri ambayo imegusa maeneo mengi katika maendeleo ya nchi yetu. Ninawapongeza kwa kazi hii na Wabunge kazi yetu sasa ni kushauri ambapo hamjaweka mambo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuwashauri, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa nchi yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri, njema na ya kizalendo anayoifanya kwenye nchi yetu. Nadhani sisi sote ni mashahidi, Rais wetu amekuwa muungwana, amekuwa mvumilivu, amekuwa mstahimilivu, amekuwa kiongozi mwema kabisa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Watanzania wanayaona yote anayoyafanya na mwaka 2025 watafanya kinachopaswa kwa kummwagia kura, nami kwa niaba ya watu wa Sumve niseme kwa yote aliyoyafanya Mama, Rais wetu tutampa kura nyingi sana. Kama zitatokea chache za kutokupata, basi itakuwa bahati mbaya. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ameonesha uvumilivu mkubwa sana, usikivu kwa kuruhusu mambo mengi ambayo yalikuwa yamezuiliwa hapo kabla. Naweza nikatoa mfano, Vyama vya Upinzani vililalamika kuhusu mikutano ya hadhara, kuhusu mambo ya demokrasia na kadhalika; amewaruhusu wameanza mikutano ya hadhara, wanasema wanavyosema, lakini kwa sababu ya kazi nzuri anayoifanya, sasa bahati mbaya sana zile sera za kusema, zimeisha kwa sababu kazi nzuri inafanywa, wameruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wamehamia kwenye matusi, kwenye kugawa nchi, kwenye udini na ukabila na hizo ni sifa za watu ambao wanakuwa wameishiwa sera. Kwa hiyo, hiyo ni moja ya mafanikio makubwa ya Mheshimiwa Rais, kufanya kazi nzuri mpaka wanaompinga wanaishiwa sera, hivyo, tunampongeza kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia amekuwa msikivu, hapa Wabunge tulisema tukashauri kuhusu kikokotoo, nadhani mmeona kupitia bajeti hii, kuna mwelekeo wa usikivu na mabadiliko kwenye kikokotoo. Kutoka ile 33% kwenda 40% ni hatua kubwa, lakini sisi kama Wabunge, mimi ninajua bado ninalo jukumu la kushauri Serikali yetu ya CCM iendelee kulitazama jambo hili kwa sababu chama chetu ni cha wakulima na wafanyakazi. Tufanye zaidi, ikiwezekana tufike ile 50% iliyokuwepo na ikiwezekana wale ambao tayari walishashughulikiwa na kikokotoo, hii nafuu iliyopatikana iwapate wakati huo tukijadili namna ya kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba sasa nijielekeze kwenye kuzungumza mambo yaliyoko kwenye Jimbo la Sumve. Watu wa Sumve tunayo shukrani kubwa ya kimaendeleo kwa Rais wetu. Tulikuwa tuna mambo machache nitayatolea mfano ambayo tulikuwa tunayalilia na ameyatekeleza. Wakati yeye anaingia madarakani na mimi nakuwa Mbunge, Sumve ilikuwa na vituo vya afya viwili tu, lakini leo tunazungumza viko vitano. Kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais na sisi watu wa Sumve tunashukuru kwa hilo. *(Makofi)*



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikuwa hatujawahi kuona mradi wowote wa kuleta maji ya Ziwa Victoria na hayakuwepo. Tuko kwenye Mkoa wa Mwanza, lakini ladha ya yale maji hatuijui, lakini kwenye uongozi wa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia, ametupatia mradi wa shilingi bilioni 39, unatoa maji Misungwi, Koromije, Sumve mpaka kwenye Jimbo zima la Sumve kupata maji ya Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa mradi mwingine wa maji ya Ziwa Victoria, unatoka Hungumalwa kupitia Jimbo la Mheshimiwa Mashimba Ndaki mpaka Malya kwenye Jimbo la Sumve. Hii ni heshima kubwa kwa watu wa Sumve na mambo mengi kwenye sekta za elimu na barabara za vijijini yamefanyika. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Serikali ya CCM ni Sikivu na mimi ni Mbunge wa CCM na ni Mbunge wa Jimbo la Sumve, sasa nami naomba yale ambayo hayajatekelezwa, nishauri namna ya kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa hapa nadhani kama huwa tunasikilizana vizuri, nimekuwa nikizungumza shida kubwa sana iliyoko kwenye Jimbo la Sumve. Siasa ya Sumve ni barabara, na nimekuwa nikizungumza kweli kuhusu siasa ya Sumve ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiwaambia kwamba, *historically*, labda leo unipe nafasi nitoe elimu kidogo. Jimbo la Sumve na Wilaya ya Kwimba ni moja ya maeneo ya kiutawala, makongwe na mama kwenye nchi hii. Wakati wa ukoloni tulikuwa na Mkoa wa *Nyanza Province*, ulikuwa na Wilaya za Mwanza, Musoma, Bukoba, Shinyanga na Wilaya ya Kwimba. Tulipopata Mkoa wa Mwanza, Wilaya za mwanzo ni Geita, Mwanza, Ukerewe, Kwimba yenyewe pamoja na Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ni Wilaya kongwe, imezaa Wilaya ya Magu, imezaa Wilaya ya Misungwi na ina mjukuu anaitwa Busega. Ni Wilaya kongwe kweli kweli, lakini ninavyozungumza hivi, mimi Mbunge ninayetoka Kwimba Jimbo

19 JUNI, 2024

la Sumve. Wilaya ya Kwimba ni Wilaya pekee kwenye Mkoa wa Mwanza ambayo haijaungwa na Makao Makuu ya Mkoa na barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sizungumzii leo, nimekuwa nikizungumza kila mara na kusesitiza, wakati mwingine ninakasirika na wakati mwingine nakuwa mpole nikiwaeleza ninyi ndugu zangu wa Serikalini kwamba, kule Sumve tunaomba mtujengee barabara ambayo hatujajihidi sisi, tuliahidiwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nami niliizuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inatoka Magu – Bukwimba – Ngudu – Hungumalwa, kwa kiwango cha lami na ni barabara ya kilometa 71 tu, siyo barabara ndefu sana. Kwa sababu yapo maeneo mengi yanajengewa hizi Barabara, tunaona na wengine mpaka zinabanduliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mwaka huu janga la mafuriko limezoa lami za watu, wakati wengine wanazolewa lami na bajeti inahamishiwa kwenye kuzirudishia zile lami, sisi hatuna. Jimbo la Sumve hata milimita. Yaani, hivi unaelewa nikisema milimita! Sentimeta ni kubwa kwa milimita, hatuna hata milimita moja ya lami Sumve na sisi ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nimelisema hapa kwa Mawaziri wote wakiwepo. Nilianza na Mzee Chamuraho akaniahidi ahadi haikutekelezwa. Kwa hiyo, kwa Kiswahili kizuri akanidanganya. Nikaja hapa Mheshimiwa Prof. Mbarawa nikamwomba akaniahidi ahadi haikutekelezwa, kwa hiyo lugha ya kistaarabu ni kwamba alinidanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina imani na Mheshimiwa Bashungwa, hujapata nafasi ya kunidanganya. Naomba usinidanganye. Naomba utujengee barabara na kule watu wetu kama walivyo watu wengine, nilikuwa naona kule Mtwara, umefanya kazi nzuri sana wakati wa haya mafuriko ya kuwafikia watu na kuwatia moyo na kurekebisha miundombinu, lakini hao uliokuwa unaona lami zao zimesombwa, sisi hatuna kabisa. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi haiwezekani wengine wanarudishiwa barabara zilizosombwa, wengine hawana. Hao waliosombewa lami zao wasubirie sisi ambao hatuna hata lami ya kusombwa na mafuriko tuwekewe ili walau na sisi ije isombwe tuone, kwamba lami huwa zikisombwa *this is what happens.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea hivi, sio sawa. Sasa hivi nimeona bajeti unarudishia kwa wale waliosombewa lami zao, sisi bado hatuna, tufanyeje? Turushe ngumi humu! Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, umewahi kuniahidi hapa mpaka ukaniambia unachukua mkopo kunijengea, hamna kitu, hujajenga *brother.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, naomba, naomba; mimi sasa hivi imani nitakayoamini hapa ni kuona magreda yako Sumve yanajenga lami, kwa sababu ahadi nimeshapewa, na Mheshimiwa Katimba leo wewe ndiyo Waziri Mkuu wetu. Nikwambie, si ndiyo anakaimu! Mimi ninakushtakia, watu wa Sumve tumedanganywa sana kuhusu Barabara, na Mbunge wao sasa niseme nini humu? Kama utaona uvivu kwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri Senior akina Mheshimiwa Jenista hapo, kuna Mheshimiwa Simbachawene hapo nyuma, wanisaidie. Sisi tumedanganywa sana. Tunaomba sasa na sisi tujengewe barabara yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani inafika wakati tunaona sasa sisi hapa...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamis, Taarifa.

### **TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Siku hiyo wakati anaahidiwa lami na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, mimi nilikuwepo. (Kicheko/Makofi)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuahidiwa lami, vikao vyote vilivyokuwa vinafanyika vya Marais wakati ule anagombea Mheshimiwa Mkapa, aliahidi lami ya kutokea Magu kwenda Hungumalwa, mimi nilikuwa Ngudu kwenye mkutano wa hadhara. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, akaja akaahidi Mheshimiwa Kikwete, nilikuwa tena Hungumalwa kwenye mkutano wa hadhara. Kaja kaahidi mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alikuja Kwimba niko kwenye mkutano wa hadhara. Sasa kama ahadi za viongozi wa Serikali hazitekelezwi, wasiwasi wangu ndiyo unakuwa mkubwa kwa sababu ni ahadi ya viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kasalali, unapokea Taarifa ya Mheshimiwa Hamis Tabasam?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa heshima kubwa sana taarifa ya Mheshimiwa Tabasam. Pia ninasisitiza, ndiyo maana nimetaja cheo cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu mimi wakati naomba kura pale Sumve aliyekuja kunishika mkono ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, naye akasisitiza kwenye ahadi iliyokuwa imetolewa na Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa Makamu wa Rais wakati ule alipokuja Sumve kuhusu kujenga barabara ile, akasisitiza itatekelezwa. Sasa tupo bado kwenye hatua za mwishoni mwishoni, hebu jamani tufanyeni hili tulimalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ya msingi sana kwenye uchumi na utalii wa Kanda ya Ziwa, barabara ambayo inatoka Bujingwa au Fulo inapita Nyambiti inaenda Malya na baadaye inaenda Maswa kwa Mheshimiwa Nyongo. Bahati nzuri Mheshimiwa Nyongo sasa yupo kwenye Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwenye kufungua Mbuga za Maswa na utalii wa Serengeti ya Kusini. Barabara hii imeahidiwa kwenye ukurasa wa 78 wa Ilani ya

19 JUNI, 2024

Chama Cha Mapinduzi na sote tunajua tupo hapa kumsaidia Mheshimiwa Rais. Naomba sana, sana, sana viongozi wangu Sumve ni barabara na siasa za Sumve ni barabara. Sasa na ninyi mpo hapo kutekeleza hilo. Wakati wa kitubio mtubu, kama mliwahi kutudanganya mwende mkatujengee barabara yote siyo kipande, yote na sisi tuanze kukanyaga lami maisha yaendele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naahidi kama nitathibitishiwa kwamba sidanganywi tena, nitaunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, atafuatia Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami pia nawashukuru Mawaziri wote wawili na wasaidizi wao na pia namshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya uchangiaji kwenye bajeti hii, naomba nianze na yale ya jimboni. Namshukuru Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, tulikuwa na shida kubwa ya chumba cha kusaidia mashine za uchujaji damu. Tumepeva takribani shilingi milioni 196, najua ujenzi mzima wa kile chumba unahitaji shilingi milioni 400. Ninaamini tumeanza huko mbele ya safari Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, umelisikia hilo utaona namna ya kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa kwa maana ya kuboresha uchumi wa Mkoa wa Katavi ni suala zima la Gridi ya Taifa (umeme wa msongo mkubwa). Sijaiona ikisomeka hapo, lakini naamini mpango mkubwa wa kuhakikisha Mpanda tunafikishiwa umeme wa Gridi ya Taifa utatusaidia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kuendelea kushauri, furaha ya kuwa na vitu vingi wakati mwingine inaweza

19 JUNI, 2024

ikakufikishia sehemu ukashindwa kujua uanze na kipi. Kama nchi, Mwenyezi Mungu ameturuzuku tuna vitu vingi sana, kuanzia madini, misitu, bahari, ardhi yenye rutuba, watu ambao pia hata suala la amani na utulivu ni kati ya vitu ambavyo Mwenyezi Mungu ameturuzuku. Hasa kutokana na hayo tunajikuta wakati mwingine tunapata shida, vitu ni vingi, hujui uanze na kipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kauli yangu ni nini? Ni vizuri tukaja na vipaumbele, tuwe na vipaumbele vichache. Tukianza na hivyo tutafika mahali. Sisemi kwamba mengine tuache, lakini tu-concentrate kwenye maeneo machache ambayo hayo yanaweza yakatusaidia kututoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuongea hapa ndani, bahati nzuri ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yupo hapa, kwamba tukizungumzia habari ya kuiunganisha nchi hii kwa mtandao wa maji (Gridi ya maji ya Taifa), tafsiri yake ni nini? Tunapozungumzia vyanzo vingine vya mapato kwa suala tu la kuunganisha nchi kwa mtandao wa maji, najua jitihada ya Serikali katika maeneo hayo, kuunganisha kwa kutokea Ziwa Victoria, tunazungumzia habari ya kuunganisha kutokea Ziwa Tanganyika, kuunganisha vyanzo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija na hiyo Gridi ya Taifa maana yake hapo kwa maana ya uchumi kilimo kitakua, kwa maana ya uchumi utalii utaongezeka na ufugaji halikadhalika. Kwa hiyo, hili suala la Gridi ya Taifa kati ya vipaumbele nilikuwa naomba sana tuisahau jambo hili. Pia, tuna maeneo mengine ambayo nashangaa Watanzania wenzangu Kiswahili kama Kiswahili ni bidhaa. Hebu tuipeleke huko duniani, kwani ni chanzo kikubwa cha mapato, na ni fursa ametupa Mwenyezi Mungu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa, ukifika mahali ambapo Kiswahili kinatoka Tanzania hapa, lakini ukienda baadhi ya nchi huko walimu wakuu katika vyo mbalimbali unakuta ni watu wa nchi nyingine. Kwa nini tusitumie fursa hii? Kwa nini nalisema hilo? Tukipeleka Kiswahili duniani, fedha watakayopata watu wetu huko wataturudishia nchini. Tukifanye Kiswahili kuwa bidhaa. (Makofi)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nilikuwa naongelea habari ya hiyo mipango, yaani kwa maana ya kuwa na vipaumbele. Nije kwenye suala la mipango fungamanishi. Kwanza siku zote mimi ni kinara wa masuala ya idadi ya watu kwa maana ya hapa Bungeni ni Mwenyekiti wa Chama cha Kibunge cha Idadi ya Watu. Naomba niendeleo kuisitiza kwa maana ya mipango. Sikatai idadi ya watu, lakini ukiwa na idadi ya watu ambao huwezi kuwadhhibiti, tatizo langu ndiyo linakuja hapo. Unapokuwa na midomo mingi ya kulisha kuliko wazalishaji, tatizo linakuja hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mipango yetu iende huko, kwa sababu sasa hivi ukijaribu kuangalia na huko duniani nimeshiriki makongamano mbalimbali, dunia inaogopa kutokana na suala la ongezeko la watu, na bahati mbaya zaidi wakiiangalia Afrika na ukiangalia Afrika utarudi hata Tanzania. Leo turudi kwenye idadi ya Watanzania tuliopo, wazalishaji ni wangapi? Unapokuwa na midomo mingi ya kulisha kuliko midomo mingi ya kuzalisha, tatizo lipo hapo. Kwa hiyo, nasema idadi ya watu siyo tatizo, ikitumika vizuri ni fursa, lakini isipotumika vizuri tatizo naliona linaanzia hapo. Kwa misingi hiyo, naomba suala la idadi ya watu tuliangalie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru suala la kuboresha nidhamu ya matumizi ya fedha, lakini pia kuboresha kitengo cha ufuatiliaji na tathmini na nilikuwa naomba watu hao wapatiwe rasilimali fedha na idadi ya watumishi iongezwe eneo hilo. Tunapozungumzia sekta za uzalishaji na huduma za jamii, usalama wa chakula, amani, usalama na umoja ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala lingine ambalo niliwahi kuongelea hapa suala la mapinduzi ya nne ya viwanda. Kwa maana leo hii sisi kama nchi bila kujikita huko ambako kunagusa akili bandia, wengine wanaita akili mnemba *(Artificial Intelligence)* shida ipo. Majuzi hapa mnaona kuna hiki kitu wanaita *optic fibre*, ilipata shida, tulipata tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo watu wetu katika suala zima la mipango, tusipojikita huko ambapo dunia ndiyo ipo

huko tutapata tabu. Nilipokuwa nikifuatilia tunaambiwa hakuna namna, tutafanya bila kubadilishana namna tunavyoweza kuishi, kwa maana ya mapinduzi ya nne ya viwanda. Pia, hapa tulipofika sasa hivi dunia tunaingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo bila ya kwenda huko sisi kama sisi hatuwezi tukabaki peke yetu. Narudia kutoa mfano, tulipata shida ya hiyo *optic fibre* na watu tuliparaganyika mahospitali, benki, viwanja vya ndege, wote tuliona. Kwa hiyo, wakati tukizungumzia tunatokaje hapa, tusiache na sisi kujikita huko kwa sababu hatupo peke yetu, lazima tuchanganyike na dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye eneo la madini. Madini kwa ujumla wake nilifurahi kusikia kwamba sekta ya madini iliongezeka kwa kiasi hiki, kutoka dola bilioni 3.12 mwaka 2021 hadi dola 3.55 mwaka 2023. Rai yangu ni kwamba, ili madini yaweze kututoa, tunatakiwa tuangalie hoja za msingi. Tatizo ni nini? Niliwahi kuzungumza hapa suala la tozo. Mbali ya tozo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, uende mbali zaidi. Ikiwa tunaambiwa leseni zilizopo... (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi, hiyo *figure* nadhani hujaitamka sawasawa, labda irejee vizuri, toka bilioni tatu *point* ngapi mpaka bilioni ngapi?

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni 3.12 kwa maana ya mwaka 2021 hadi dola bilioni 3.55 mwaka 2023. Kwa hiyo, *point* yangu hapa nilichokuwa naomba sana tusiache kwenda kwenye intelijensia ya uchumi. Kwenye eneo hilo la madini tukumbuke hatupo peke yetu, kuna watu wengine wanachimba pia, tusaidie kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna baadhi ya vitu hapa na inatakiwa watu wa mipango mtuambie, nimekuta huko kwenye vyombo vya habari tunaambiwa, kwa mfano eneo la matangazo tu na watu tunashindwa kuelewa matangazo yanaweza yakawa ni biashara. Leo baadhi ya nchi, ndege yao wameiandika



19 JUNI, 2024

*Ngorongoro Crater. Mtu unajiuliza, hivi wamefanya kwa kubahatisha au kuna kitu wana-aim at? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tunatakiwa kwa maana ya intelijensia ya uchumi twende huko. Yawezekana fedha ile ambayo ilitakiwa ije nchini kwa kuandika tu, watu wakatengeneza fedha. Sasa Watanzania tunasemaje katika maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapata shida baadhi ya nchi huko duniani wanaendelea kufikiri kwamba Mlima Kilimanjaro upo kwao, na Watanzania tunakalia hizo fursa. Tunatakiwa tutoke kwa maana ya dunia ya sasa hivi. Ndiyo maana nasema hatuwezi tukakwepa hii awamu ya nne ya maendeleo ya viwanda kwa maana, kama wenzetu wanafanya matangazo, wanajaribu kuishawishi dunia na sisi kwa maana ya uchumi mpana tufike huko, huko hakukwepeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa kumalizia, nilikuwa naomba mipango mizuri ambayo imefanyika na mama yetu kwa maana ya kuboresha sekta nzima ya afya, hivyo vifaatiba vilivyoongezeka tutoke kwenye eneo hilo, tufanye eneo la afya pia kuwa ni eneo ambalo tunaweza tukafanya utalii wa tiba na hiyo ikawa ni sehemu ya kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kapufi. Kuna matangazo kidogo kabla hatujaendelea.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni ndani ya ukumbi wetu wa Bunge; tunao wageni 65 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambao ni Makatibu wa Siasa na Uenezi wa Matawi yote kutoka Jimbo la Ubungo jijini Dar es Salaam, karibuni sana Wajumbe. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Tunao wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni wanafunzi 47 wanaosoma Shahada ya Pili ya Elimu kutoka *St. Augustine University of Tanzania* kwa maana ya SAUT, Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge ambao ni wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimbo la Kilolo Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge ambao ni walimu kutoka Nyamongo Jimbo la Tarime Vijijini Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, ambao ni wanafunzi 89 na walimu 20 kutoka Shule ya Msingi na Sekondari Masange Juu ya Lushoto Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma Taaluma ya Maendeleo ya Jamii, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, anafuata Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, baada ya Mheshimiwa Francis atafuata Mheshimiwa Anatropia Theonest kisha atafuata Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi.

Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza jioni ya leo. Kwanza

19 JUNI, 2024

nitangulie kuishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa namna ambavyo imetuunga mkono sisi wa Wilaya ya Kilwa baada ya kupatwa na janga la mafuriko yaliyosababishwa na mvua za *El-Nino* ambazo zilianza mwezi Oktoba hadi mwezi Mei na Kimbunga Hidaya ambacho kilitokea tarehe 3 hadi 5 mwezi Mei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kimbunga hiki na mafuriko haya yaliacha athari kubwa ambapo kaya takribani 2,096 ziliathirika, wakazi 8,397 waliathirika na kadhia hii, nyumba zaidi ya 1,160 zilizolewa na mafuriko na hekta 28,000 za mashamba ziliharibiwa na mafuriko. Kwa hiyo, napenda kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo aliweza kuidhinisha pesa nyingi zikaweza kutumika kwenda kutusaidia kupunguza athari na kuondoa athari za janga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kazi nzuri ambayo amefanya ya kurejesha mawasiliano ya barabara kuu na barabara za mikoa. Mheshimiwa Jenista Mhagama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Hussein Bashe, ambaye ametuahidi kutuletea miche 66,625 ya minazi na pia namshukuru Mheshimiwa RC wa Mkoa wa Lindi Mheshimiwa Zainab Telack kwa kutekeleza majukumu yake vizuri wakati wa janga hili, Mheshimiwa Mohamed Abdallah Nyundo DC wa Wilaya ya Kilwa, DED Wilaya ya Kilwa Bi. Hanan Bafagih, pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilwa Said Timami; sisi Wabunge kwa umoja wetu ambao tulishirikiana na mamlaka zote za Serikali, Mheshimiwa Rajabu Ngatanda, Diwani Kata ya Tingi, Mheshimiwa Said Manjonjo, Diwani Kata ya Somanga na Mzee wetu Shaweji Kimbwembwe au almaarufu Mzee wa Jogoo ambaye kwa hakika alikuwepo katika kila eneo ambapo mafuriko haya yalisababisha athari mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kuishukuru Taasisi ya AUWA (Asili ya Wamatumbi na Uzalendo Wao), Jeshi la Zimamoto na Uokozi, TANROADS, TAWA, Kanisa la AICC, Kanisa la EPCT, Taasisi ya Bin Shomari, Blue Springs ya Ujerumani, MSD, BAKWATA,

19 JUNI, 2024

Benki ya NMB, TRA, UNICEF pamoja na Umoja wa Wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo za dhati nawatakia kila la heri wale wote ambao walitusaidia na Mwenyezi Mungu awarejeshee pale ambapo walitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupongeza na kuunga mkono bajeti hii, nampongeza Mheshimiwa Waziri rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, ambaye alikuwa anasimamia utoaji wa mafungu. Nimemsikia katika hotuba yake ukurasa wa 155, amezungumzia suala la kutengeneza ule mfuko wa kusaidia athari za maafa mbalimbali, kwa kweli hapa amecheza kama Azizi Ki. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa hizo fedha zilizopangwa kukusanywa, zikusanywe kweli kweli ili linapotokea janga kama hili, basi tuweze kulishughulikia mara tu changamoto inapojitokeza. Hii itasaidia kurejesha mawasiliano na miundombinu mbalimbali kama ilivyotokea mwaka huu kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kushukuru na kupongeza hotuba ya bajeti kwa kuongeza malipo ya kikokotoo kwa wastaafu wetu, katika ukurasa wa 102 hadi 103. Kwa kweli hili ni jambo jema ambalo lilileta mgogoro mkubwa sana katika jamii na kwa kweli sasa tunaenda kupata mwarubaini katika jambo hili, isipokuwa nilikuwa nina angalizo eneo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kufanyika uhakiki wa Watumishi wetu waliostaafu, na mara zote uhakiki unafanyikia mikoani. Naomba jukumu hili sasa lipelekwe kwenye ngazi ya Tarafa kwa sababu tunafahamu hawa watumishi wanaokwenda kuhakiki hawa watumishi wastaafu wana vifaa, wana magari na kadhalika. Tofauti na hawa watumishi ambao wamekuwa wengi ni wazee, hawana nguvu ya kifedha ya kutosha ya kuweza kusafiri kwenda mikoani. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sitarajii Mwalimu wangu Swaleh Mweru anaishi Nandete leo umtembeze zaidi ya kilomita 300 kufuata haki zake au kufuata uhakiki. Kuna Mwalimu Said Ngomba yupo kule Mtende na kuna Mwalimu Emiliana Mandai yupo kule Kipatimu wanalazimika kutembea zaidi ya kilomita 300 kufuata haki zao au kufuata huo uhakiki. Kwa hiyo, naomba Serikali irekebishe hili ili kuboresha mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la mifumo. Mifumo yetu imekuwa sumbufu sana katika malipo. Licha ya bajeti ambayo tuliipitisha mwaka 2023 na mwaka 2022, utekelezaji wake umekuwa mgumu hasa kwenye kipengele cha malipo. Kwa mfano, kule kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kilwa, mpaka leo fedha za Mfuko wa Jimbo shilingi milioni 68 hazijaenda kwa walengwa. Tilitenga shilingi milioni 20 kati ya shilingi milioni 68 za Mfuko wa Jimbo ziende zikarekebishe huduma ya visima kule Kibata, imeshindikana mpaka wakati huu, mifumo inasumbua; Mfumo wa *MUSE* unasumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hela za *MSD* ambazo zilipangwa kununua madawa na vifaatiba, zimekwama, nazo ni shilingi milioni 780, lakini kuna fedha za mapato ya ndani cha kushangaza. Shilingi milioni 53 tulipanga zikaanze kujenga Zahanati ya Njinjo ambayo iliathiriwa na mafuriko ya mwaka 2020, zimeshindikana mpaka wakati huu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, basi afanye jitihada angalau inapofika wiki ijayo, tuone fedha hizo zimefika na siku zijazo katika utekelezaji wa bajeti ya shilingi bilioni 49 tuone fedha zikifika, zinaenda kutumika moja kwa moja ili kuongeza ufanisi na tija katika miradi ambayo tumelenga kuitekeleza kama ambavyo imepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, alitueleza hapa mwaka 2023, tungejengewa kilomita 72 kwa kiwango cha lami kati ya kilomita 230 za barabara za Nangurukuru -Liwale lakini sijasikia hata wakati akiwasilisha hoja za Wizara yake. Naomba atupe maelezo, watu kule tumeshawaambia lami inakuja (joka jeusi linakuja), lakini mpaka leo hatujaona juhudi zozote. Tunaomba maelezo huu mradi unatekelezwa lini na taratibu za zabuni zipoje na kadhalika. Pia,

19 JUNI, 2024

katika mradi wa barabara nne pale kutoka Mbagala Rangi Tatu kwenda Kongowe nao ningomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuipongeza Serikali, tumeshatekeleza miradi mingi na leo hii nimepata taarifa kuwa jumla ya shilingi milioni 560 zitaingia muda wowote kwenda kutekeleza Mradi wa Shule ya Sekondari Mt. Kimwaga, Kata ya Kipatimu. Naipongeza Serikali. VETA inaendelea kujengwa mwaka huu 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza Serikali imetenga bajeti kubwa kwa Taasisi ya TARURA pengine kuzidi hata ile ya TANROADS. Kwa hiyo, imeonesha namna gani kule vijijini ambako kuna uzalishaji mkubwa wa mazao kumewekewa mkazo wa kuboresha barabara zake ili mazao yaweze kusafirishwa kupelekwa sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada yakusema hayo, nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hii Bajeti Kuu ya Mipango. Cha kwanza, nawashukuru Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba; pili, nawashukuru Makatibu wote wa Wizara hizo na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Chande na Mheshimiwa Nyongo na viongozi wote wanaofanya kazi katika Wizara hii. Wanafanya vizuri sana kwenye maeneo yetu, tunawaona, tunawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kusoma hotuba ndefu kama hii niliyoisoma ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Nilivyoiangalia nikaona ni kama hawa jamaa walikuwa wamejikita kama maswali ya *questionnaire* fulani hivi. Tukijibu hivi itakuwaje? Tukijibu hivi itakuwaje? Kila kitu kibaya na kizuri kimeandikwa kwenye hii bajeti. Sijui mmeiona vizuri jamani! Kila

19 JUNI, 2024

kitu kimeandikwa. Kwa hiyo, nasi kwa kuiona bajeti hii, tunafanyaje kwenye hili jambo ambalo tunaweza kulizungumza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote hapa mimi nizungumze maombi maalumu. Bahati nzuri kuna Mipango na Fedha hapa. Jimbo la Bunda ambalo ni jimbo langu, limekatwa mwaka 2015 na limekatwa kwenye mazingira magumu sana. Wananchi wanasafiri kilomita 240 kwenda kutafuta halmashauri na kila siku humu ndani wapo watu wanaomba halmashauri, wanaomba na maeneo mengine kwa maana ya kuongezeka kwa mipaka ya maeneo na majibu ya Serikali yanasema kwamba, tumekuwa na utawala wa muda mrefu au tumekuwa na halmashauri nyingi tumeanzisha, tunazijenga upya ili mje kwenye hizi ambazo zina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, hivi kama Bunda majengo yaliyokuwa Halmashauri ya Bunda yapo wazi, yaani kuteua Mkurugenzi akae pale, wananchi waende kumwona, imekuwa kazi hiyo! Itakuwa na maana gani? Hivi tunasaidia nini? Kwa hiyo, naomba kwenye hili jimbo la Bunda kweli kabisa tuangaliane. Wakati fulani Mbunge akisimama humu ndani akitetea wananchi wake kwenye jambo nyeti huwa tunakuja na lugha kwamba, huyu anatafuta kura. Hivi wananchi gani wanateseka kwenye nchi hii? Watu waende kilomita 240 kutafuta halmashauri, majengo yao yapo pale Bunda. Kwa nini, msiteue Mkurugenzi akae pale? Kuna ubaya gani? Mkurugenzi tu akae pale Watumishi tugawane tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haiwezekani, kwa nini iwe Jimbo langu la Bunda? Tusiunganishe na Halmashauri ya Mji? Tukaenda. Kwa nini watu wasafiri muda mrefu hivyo? Wanateseka nini hasa? Tumeandika sera kwamba, tunapeleka huduma karibu na wananchi. Kwa hiyo, naomba hiyo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, na bahati nzuri yeye kule wale ni watu wake, na nikisema hivyo wanamsikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, Mheshimiwa Waziri amesema mwenyewe kwenye hotuba yake vizuri sana, sitaki

19 JUNI, 2024

kuisema zaidi. Amesema, *sometimes* tunakopa hizi fedha na fedha nyingine kwa kuangalia mikoa ambayo ipo nyuma kimaendeleo. Sasa nijulize, pale Bunda bahati nzuri Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia ametusaidia kuleta mradi wa Mgango – Kiabakari. Mradi ulikuwa umekwama, ametusaidia upo 99%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Butiama kuja Jimbo la Bunda; Nyamuswa pale ni kilomita tisa. Sisi hatuna maji ya Ziwa Victoria. Yaani leo maji yanasafiri kutoka Ziwa Victoria yanakuja Dodoma. Sisi ambao tuna kilomita 20 hatuna maji. Sasa *equal distribution* ipo wapi? Ipo wapi kugawana keki? Kwa hiyo, nawaomba kwenye haya maombi maalum wafanye hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya Sanzati – Nata. Sasa ni miaka 11, nimeona *certificate* za mkandarasi C 13 hazilipwi. Barabara imeshalimwa ipo, madaraja yamejengwa, haikamiliki. Kwa hiyo, naomba Halmashauri ya Wilaya, Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kwa vijiji 33 na barabara ya Sanzati iwekwe kwenye orodha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuwa anaongea rafiki yangu hapa Mheshimiwa Mwijage, nilikuwa nasoma bajeti yake yam waka 2017/2018, nikahesabu alivyokuwa amemsifia Marehemu Dkt. Magufuli kama mara 70 hivi, lakini nimeona bajeti hii pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ulivyomsifia Mama kama mara 100 hivi, nikasema haya mambo yanategemea na mapenzi ya kila mtu na kile anachokiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke *record*, leo mniandike vizuri hapa, kwamba Mungu akimsaidia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia akamaliza vipindi vyake viwili, atakuwa Rais bora katika nchi ya demokrasia. Haitatokea, atakuwa Rais anayevumilia watu, Rais anayejenga watu, haitatokea na atakuwa Rais bora zaidi. Mama ni mvumilivu kiasi. Watu hapa tupo tofauti sana. Wapo watu wana mambo mengi sana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imepatwa na ugonjwa wa kusema fulani anatafuta Urais, sijui kutafuta Urais ni dhambi?



19 JUNI, 2024

Yaani ni ugonjwa ambao umekua, lakini Mama amevumilia kwa kiasi chote. Kuna watu hapa wanamsema vibaya Mama na hao anawavumilia. Kuna watu wengine alienda hata kuwasalimia na kuwaona; Mama anavumilia, atakuwa Rais mwenye demokrasia kubwa hapa duniani kama alivyokuwa anafanya hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeona juzi watu wanauliza, CCM wajifunze kutoka *South Africa*. *South Africa* sisi ndio tunawapa dawa, sisi ndio waganga wao. Tuliwaambia msigeuke nyuma, wakageuka nyuma. Tunachosema, haya maneno yanayokuja hapa, mara mna vikaratasi, sijui vikaratasi mtu amefanya nini? Sijui amekodisha sukari, sijui amefanya nini? Mgawanyiko huu tunapoelekea kwenye uchaguzi ndiyo unaua chama. Huu mgawanyiko, watu wanatoa, kila mtu ana vikaratasi vyake, kila mtu anagombana, huo unaua chama. CCM miaka yote tumeheshimu Marais wote waliokuwepo, tumeheshimiana na watu wote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombea Mama, hii timu yake aliyonayo ya Mawaziri, Mawaziri hawa wanaochapa kazi usiku na mchana aende nayo na amalize nayo. Kwa hiyo, mgawanyiko wa Chama cha Mapinduzi kwa kuoneana wivu, kwa kutaka Madaraka, ndio unaua chama, na chama hiki kwa sasa kipo vizuri mno, na hao wanaotembeatembea huko barabarani mwasubiri waingie *king*. Wataingia tu haina shida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia *equal distribution* Mkoa wa Mara. Sasa nilikuwa nazungumza ya Jimbo la Bunda; sasa nije ya Mkoa wa Mara. Katika bajeti hizi, lazima mkumbuke Mkoa wa Mara. Leo watu wanazungumza reli iende mpaka Burundi iende wapi, lakini sisi reli inayotoka Tanga – Moshi – Arusha - Mara haijulikani hata ipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bandari iliyokuwepo Mkoa wa Mara - Musoma haipo, viwanda vya pamba havipo, viwanda vya Samaki havipo, *ginneries* za Kibara na Kosasi hazipo, hata kiwanja cha ndege tulichoanza kujenga juzi hela haiendi vizuri. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ina majengo mawili; jengo moja limekamilika, moja bado.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mama na vitita hivi kupeleka fedha, ajitahidi tumalize lile jengo angalau hata Hospitali ya Wilaya ionekane. Mkoa wa Mara umerudi nyuma sana. Tunaomba katika bajeti hii na mnapoenda mtufanyie vizuri ili mkoa wetu nao uonekane kwamba una maana kwenye nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni walipa kodi ya mifugo. nimeiona amezungumza Mbunge wa Ngorongoro, nami nikawa naangalia, hivi Mheshimiwa Dkt. Mwigulu huyu, mbona niliwahi kuona ka-statement kamesema ni mtoto wa mkulima na mfugaji. Hii lugha ya kuonekana kwamba wafugaji hawalipi kodi, hawakai vizuri inatoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaeleze, katika nchi kwenye *chemistry* kuna kitu kinaitwa *catalyst*, kama ukitengeneza soda, unaiweka inachochea. Katika watu wanaochochea maisha ya Watanzania hapa Tanzania ni wafugaji. Kilimo cha Tanzania 65% kinategemea Plau; ni ng'ombe hiyo hiyo; ni ngo'mbe ndio wanaolisha watu; mazao yanayozalishwa mnakata kodi, ni ng'ombe inazalisha. Leo vinywaji mnavyowekea kodi kubwa mtu anywe pombe vizuri lazima ale nyama inatoka wapi hiyo nyama? Anaitoa wapi? Leo minada yote mnayoenda kutafuta mbuzi na ng'ombe mnaitoa wapi? Maziwa yanatoa kwashakoo, Serikali haitoi hela; kwashakoo ni ngo'mbe. Mnaitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu leo mfugaji unasema ana ng'ombe 900, ana ng'ombe 9,000. Hata angekuwa nazo 10,000, eneo analoishi analipia kodi. Wafugaji wote wenye ngo'mbe 1,200 tunalipa kodi. Sisi kodi kubwa, kilometa moja unaweza kulipa shilingi 2,000,000 mpaka shilingi 3,000,000 halafu mnaenda kuongeza sijui iwe shilingi 31,000, sijui elfu ngapi? Hapana mzee, punguza hapo. Punguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujue hawa watu, ni watu wanaishi. Wanakaa katika maeneo ambayo yana changamoto za ufugaji; maeneo ya malisho na maji. Wafugaji hali yao sio nzuri. Kwa hiyo, tunawapa nafuu ili waendeleo kuwepo. Hivi mnaongeza kufanya

19 JUNI, 2024

nini? Kwa hiyo, nawaomba kwenye mambo ya mifugo, Mzee wewe nimekuona na *statement* yako ninayo, umetokana na hao watu. Angalia kwanza tabu zao ni kubwa, msiongeze tabu juu ya tabu. Watapata shida sana watu hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo leo ninalo ni mifumo. Nimesoma bajeti hii vizuri sana. Mifumo eti siku hizi kuna *robot* inaitwa mifumo. Sasa hivi unaweza kusema sekondari fulani imepata shilingi milioni 340; saa nne hesabu inasomeka zipo pale benki shilingi 340. Saa nane mfumo umetembea umerudi hela haipo. Siku hizi kuna mifumo kama *robot*. Sasa nchi hii unaweka hela kwenye akaunti za maendeleo, hela zipo ataiona asubuhi. Kuna Kituo kimoja cha Polisi, tunajenga, nimepewa shilingi milioni 50, RPC ananiambia hela iliingia jana, imetoka juzi. Imeingia sijui lini na imetoka, yaani kuna mifumo inatembea. Leo tunamaliza bajeti tarehe 26, tutaanza mwezi Julai, mifumo inaanza kufungwa mpaka mwezi wa Septemba. Hivi ni nini hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunatunga sheria ya kufanya bajeti itumike, lakini mifumo itafungwa, haifunguliwi. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, bahati nzuri wewe ni mzalendo unaishi na Bendera ya Taifa. Tazama vikwazo vinavyotokana na fedha. Ni bora fedha iwe haipo kuliko fedha ipo haifanyi kazi. Kwa hiyo, kwenye suala la mifumo, hiyo mifumo inayotembea kama *robot* uione uanze kuidhibiti. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaweza kuhitimisha, tafadhali.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Naam!

**MWENYEKITI:** Unaweza ukahitimisha, tafadhali.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya sawa. Nahitimisha kwa deni la Taifa, sasa huwa najjuliza, hivi deni la Taifa au ni wajinga, waliliwa? Hivi deni la Taifa linahusu Afrika tu au?

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda umeisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mimi nimeona madeni ya Taifa ya nchi zinazoendelea ni makubwa mno, makubwa, 240%, asilimia tatu, 160% na asilimia ngapi? Hivi Afrika ndio sisi wajinga, tunasema madeni, madeni! Madeni ya wapi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami kutoa mchango wangu katika Wizara hizi mbili ambazo zipo mbele yetu leo. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo kuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya kwenye nchi hii katika nyanja ya elimu, reli, barabara, umeme, maji na mambo mengi ambayo yalikuwa kero, na kwa kweli yameenda kutatulika kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita sana katika mipango yetu ya maendeleo ambayo inabidi iendane na Sensa ya Watu na Makazi. Maendeleo ambayo tunapanga ni vyema yakaendana na sensa ambayo tumetoka kutoa taarifa zake hivi karibuni. Taarifa za sensa zinaonesha idadi ya watu kuanzia kwenye mitaa mpaka Taifa, kwa hiyo, na maendeleo nayo yaendane na idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufike mahali tuone kwa idadi hii ya watu waliokuwepo katika kila Mkoa, je, miundombinu ya elimu iliyokuwepo inaendana na idadi ya watu? Kama haiendani na idadi ya watu, je, Serikali tunakuja na mpango gani? Hapa namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, kwa kiasi fulani amejitahidi sana iwe fedha za vyanzo au vyovyote, lakini tumeona namna ambavyo shule zimekuja nyingi katika maeneo

19 JUNI, 2024

yetu. Kwa hiyo, inaonesha ni jinsi gani Sensa ya Watu na Makazi imesababisha kupata maendeleo katika nyanja hii ya elimu msingi na sekondari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nataka nijikite sana kwenye barabara kwa sababu nafahamu tulikuwa na Wizara ya TAMISEMI, tumejadili barabara na Wizara ya Miundombinu kwa maana ya Ujenzi tumejadili mambo ya TANROADS. Haya yote tuliyoyajadili, anayefanya mambo yaende ni Wizara ya Fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia bajeti, Wizara hizi mbili zinaweka mipango yake katika maandishi, lakini ukweli tunahitaji fedha kutoka katika Wizara ya Fedha. Hoja yangu ya msingi ni kwamba, hebu tuangalie idadi ya watu waliokuwepo Mkoa wa Dar es Salaam, idadi ya watu waliopo katika Majimbo ya Mbagala na Ukonga na kiasi cha kilometa za barabara za TANROADS na TARURA tulizopangiwa, zipo sawa kulingana na ukubwa wa barabara zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha endapo hawataleta fedha kwa ajili ya kujenga kilometa tano mpaka sita, kwa kweli watakuwa hawajatutendea haki Mkoa wa Dar es Salaam, na majimbo haya niliyoyasema. Siasa ya Dar es Salaam kwa sasa ni barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua takwimu ya barabara za TANROADS zinazohitajika Dar es Salaam nzima haziwezi kufika kilometa 100. Sasa msipotupa barabara zote zilizowekwa kwenye bajeti za Dar es Salaam, mjue hamjatutendea haki. Tumepitisha bajeti kubwa ya Kilimo na mambo mengine, ni nzuri, lakini Dar es Salaam kilimo chetu sisi ni kwenye barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Kokoto mpaka Kongowe, Mheshimiwa Ndulane ameizungumzia, unaweza ukajiuliza, Mheshimiwa Ndulane sio Mbunge wa Dar es Salaam, kwa nini ameizungumza? Ni kwa sababu, ndiyo lango la kutokea kwao kuingia Dar es Salaam. Ukitaka kutoka Dar es Salaam kwenda Kusini, lazima upite barabara hiyo.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo imewekwa kwenye bajeti zaidi ya miaka mitano, lakini utekelezaji haupo. Wizara inayotoa fedha ni Wizara ya Fedha, hebu waoneeni huruma, chukueni takwimu, ni wananchi wangapi wamekufa katika barabara ile katika kipindi kifupi? Juzi tu wananchi watano wamekufa, gari limeshindwa kupanda, limerudi nyuma limeua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalieni kwa jicho la huruma. Barabara ile hai-save watu wa Dar es Salaam tu wala watu wa Mbagala, inawa-save watu wa Mikoa ya Kusini, Pwani na maeneo mengine. Hebu wekeni fedha safari hii. Wananchi wa pale wamethaminiwa nyumba zao zaidi ya miaka 10, hawajengi, hawaongezi kitu, na hatuwalipi fedha zao. Naomba sana Wizara ya Fedha tuwalipe fedha zao, tupanue ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Dar es Salaam sasa hivi ni Jimbo la Mbagala lenye foleni ya bodaboda. Mpaka bodaboda sasa hivi zinaenda kwa foleni kwa maana barabara zote zimejaa na zimefurika kwa msongamano. Wizara ya Fedha hizo kilometa chache za barabara tunazopangiwa, hebu toeni fedha ziende zikatengenezwe. Leo barabara inayotoka Rangi Tatu kwenda Mbande imekuwa ni changamoto kubwa, watu wanatembea kwa miguu, bodaboda zinakaa foleni, barabara zimezidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi. Mheshimiwa Kitila wewe upo katika Wizara ya Mipango, unapooni idadi ya watu ni kubwa elekeza mipango yako katika maeneo hayo. La sivyo, maeneo hayo hayataweza kupata maendeleo kwa kuwa kuna msongamano mkubwa wa watu na mipango iliyopangwa haiendani na wingi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunamshukuru sana Waziri wetu wa Ardhi, Mheshimiwa Jerry Silaa, ameenda kutatua migogoro ya ardhi, lakini nataka nimwambie kwa Dar es Salaam na kwa idadi ya sensa ya watu na makazi tunamwelewa, tunamheshimu na wananchi hatutavamia viwanja vya mtu, lakini

19 JUNI, 2024

kwa taasisi za Serikali ambazo wana viwanja na hawajengi, kwa *population* ile tukajenge wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa muda mrefu, Waziri wa Mipango upo, *NSSF* wana mipango yao ambayo haitekelezeki. Sisi hatuna maeneo ya kwenda, wananchi waende wapi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nakusikiliza, Taarifa. (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry Silaa, Waziri wa Ardhi.

#### TAARIFA

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Chaurembo kwa mchango wake mzuri, lakini naomba kumpa taarifa fupi kwamba, kwa namna yoyote uvamizi wa ardhi ni suala ambalo halikubaliki. Kwa hiyo, namwomba sana kama kiongozi na mwakilishi wa wananchi, pamoja na ongezeko la watu Dar es Salaam anaweza kuwasilisha na Serikali tumesikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatengeneza mpango mzuri wa matumizi ya ardhi, lakini ni vyema tukaheshimu maeneo yanayomilikiwa na watu binafsi, maeneo ya umma na maeneo ya Taasisi za Umma bila kuyavamia kwa sababu ni maeneo yetu sisi wote Watanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Abdallah Jafar Chaurembo unaipokea Taarifa?

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa nimeipokea, lakini hiyo hiyo Sheria ya Ardhi inaeleza, naye ni msomi mzuri, Mwanasheria, kwamba eneo lisipofanyiwa kazi kwa muda mrefu na mwananchi akaingia pale, tumia sheria

19 JUNI, 2024

hiyohiyo kumfanya mwananchi awepo. Hakuna Sheria isiyokuwa na mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* wana zaidi ya miaka 20 hawaendelezi maeneo. Wananchi wa Malela, Mwapemba wameendeleza. Tunao mpango, tulizungumza nao, tulikaa tukakubaliana kwamba kwa kuwa *NSSF* maeneo yale wanataka kuuza, wananchi wapo tayari, wawakatie, wayathamini, wawauzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi ametafuta hela kwa tabu, amejenga nyumba yake kwa tabu, leo hii nyumba imekamilika, *NSSF* wapo kazini wanavunja majumba ya watu. Sawa, tunakubali ni sheria, lakini wale watu wamekaa pale ndani ya muda gani? Kwa nini hatuwezi kukaa tukakubaliana kama kulipa mimi nikachukua kiinua mgongo changu nikawalipia wananchi wangu wakaendelea kukaa kuliko kuvunjiwa nyumba zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa hifadhi, wananchi wamevamia maeneo mengine, Serikali imekaa imeangalia namna bora ya matumizi ya ardhi, wameruhusiwa. Kwa nini isiwe Mbagala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali katika hili, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Jerry Silaa na Waziri wa Mipango, hao wamepanga mipango, wameshindwa kuitekeleza. Naomba tutengeneze utaratibu badala ya kuwavunja wananchi, basi wananchi wale warasimishwe. Tupo tayari kulipa kuliko kuvunja nyumba zao. Chonde chonde, siwezi kuruka sarakasi, lakini nitakachoweza kufanya, nitawasomea *Ahlul-Badr*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii nami nitoe mawili matatu kwenye



19 JUNI, 2024

hotuba ya Serikali. Mara nyingi huwa mnatuambia kwamba Serikali ni Sikivu, itasikia, pengine ngoja tuendelee kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea Bajeti ya 2024/2025. Kuongezeka kwa bajeti au kuongezeka kwa fedha, Taarifa ya Kamati inasema kwamba, ongezeko hilo linatokana na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, sehemu kubwa ya bajeti yetu itakwenda kwenye kulipa deni la Taifa, wote tumesoma na tumeona sehemu kubwa tena itaenda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, sehemu nyingie itaenda kwenye Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, hela nyingine itaenda kwenye ajira mpya na ulipaji wa hati za madai. Eneo lingine linaenda kugharamia Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050. Kwa hiyo, hiyo ni sura ndogo ya gharama ya bajeti tunayoiongelea hapa. Kwa nini nasema hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kubwa ambazo tumekuwa tukizipanga Bungeni zinaenda kwenye gharama za matumizi ya kawaida. Ukiangalia hata bajeti tuliyonayo ni kama iliyopita, fedha nyingi zinaenda kwenye *recurrent*. Zinaenda kwenye matumizi ya kununua hiki, kufanya hili, lakini siyo fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kuondoka tukawa na maendeleo bila kuwa tunapanga bajeti kwa ajili ya fedha za maendeleo? Hilo ni swali ambalo nataka niwaulize wanaomwakilisha Mheshimiwa Rais humu ndani; Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango na Wasaidizi wao, tunawezaje kufikia maendeleo kama kila bajeti tutakuwa tunaongelea *spending*? Kwa nini nasema hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na bajeti ambayo katika 100%, 68% inaenda kwenye matumizi ya kawaida na 32% inaenda kwenye matumizi ya maendeleo. Lazima tuangalie ni wapi tunaweza kwenda kujibana, ili 32% iwe ya matumizi ya kawaida na 68% ije kwenye matumizi ya maendeleo. Hapo ndiyo tunaweza ku-*archive* tunachokitaka, *otherwise* tutakuwa tunakuja

19 JUNI, 2024

kuongelea mikopo ya riba nafuu na mambo kadha wa kadha ambayo hayapendezi kwenye masikio ya walio wengi. Nikaanza kupitia nione ni kwa nini Serikali imekuwa inatumia fedha nyingi sana? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikachukuwa mfano wa kitu kidogo tu, ununuzi wa magari. Kumekuwa na ununuzi mkubwa sana wa magari kwenye halmashauri. Nikachukuwa bajeti kadha wa kadha, Serikali imekuwa inaongelea nini katika ununuzi wa magari? Nikachukuwa bajeti. Mfano, Hotuba ya Bajeti ya TAMISEMI ya mwaka 2019/2020 ilieleza, Serikali imepanga kununua magari 54 ya shilingi bilioni 4.48; hiyo ni 2019/2020. Tukaja mwaka 2020/2021, ikasema Serikali imetenga shilingi bilioni 29.83, kwa ajili ya magari 234 na hapa akataja magari 16 yataenda kwenye mikoa na magari 184 yataenda kwenye Halmashauri. Hiyo ni hotuba ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaitafuta Hotuba ya mwaka 2021/2022. Wakasema shilingi bilioni 2.8 zitaenda kununua magari nane, kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa na Tawala. Tukatoka hapo nikaingia kwenye bajeti iliyofuata mwaka 2022/2023, Hotuba ya Kamati ya Bajeti ikaongelea kwamba, Serikali ilitumia au ilipanga na kutumia zaidi ya shilingi bilioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa magari na wao kwenye ushauri wao wakaeleza kwamba, ni lazima Serikali iangalie haya matumizi ya magari. Nikachukuwa moja ya *script* ya Hotuba ya Wizara ya TAMISEMI juu ya gharama zenyewe za magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya viongozi kwa ngazi ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri kwa Mwaka 2020/2021; Mkoa wa Katavi gari moja la RAS shilingi milioni 300, Mlibwebwe DC gari moja shilingi milioni 220. Hotuba inaenda mpaka pale chini. Nataka niulize, tunaweza kwenda wapi na ununuzi wa magari ya namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine ni kwamba, kwa kiwango gani haya magari ambayo yamekuwa yananutuliwa kwenye halmashauri, halmashauri yenyewe ina mapato madogo, lakini unaipelekea gari la shilingi milioni 300; kuna gari la Mkuu wa

19 JUNI, 2024

Mkoa, kuna gari la Mkuu wa Wilaya, kuna gari la RAS, na uongozi mwingine mnaoujua. Ni kwa kiwango gani sasa tunaweza kuangalia *value for money* unapopeleka magari ya zaidi ya shilingi milioni 800 kwenye halmashauri moja? *Value for money* tunayoipata ni kiasi gani? Ni fedha kiasi gani halmashauri zina-*collect* ili kutuwezesha sisi kuona thamani ya kuwapelekea magari haya yote? Ni kwa nini tunapeleka hayo magari? Wananchi kwenye halmashauri husika, ukifanya sensa, wanatumia magari ya aina gani? Ni kwa nini wao watumie mashangingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate jibu la ni kwa nini tunatumia magari ya namna ile, tukikumbuka kwamba, hayo mashangingi tunayanunua kila siku *latest*, tunapeleka ajira Japan, tunapeleka fedha Japan, tunapeleka kila kitu Japan? Unapokuwa na nchi inayokuwa ina-*think of spending* zaidi ya kuwaza kutengeneza fedha na kutengeneza maendeleo ya watu wake *then* tujue kwamba, hapa kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri wetu, hebu tusaidieni namna tunavyoweza kubana matumizi katika matumizi ya fedha. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali imeeleza utaratibu mbovu ambao umekuwa ukitumika ku-*dispose* hayo magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari hata likipata ajali ndogo, likiegeshwa kwenye gereji, halitoki mpaka miaka minne na *value* yake inashuka. Gari mmenunua shilingi milioni 300, baada ya miaka miwili limepata ajali ya kawaida, anakuja kuuziwa mtumishi chini kwa chini zaidi ya shilingi milioni 10. Tumeona hayo na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali ameeleza hayo. Hiyo ndiyo namna tunayoweza kuisaidia hii Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuja hapa tunaongea mlolongo wa namna ya kutafuta fedha. Tunataka kutafuta fedha zipi kama hatuwezi kutunza hizi chache tulizonazo? Naomba hilo tuliangalie upya na utaratibu wa kwenye Halmashauri, tunapeleka gari baada ya muda gani?

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Bajeti na Wabunge wamewahi kushauri kwamba, tunapokwenda sasa tuwaze kuwakopesha hao watumishi magari badala ya kuwapa magari ya Serikali. Wamekuwa hawana *custodian* ya yale magari kwa sababu ya ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukaenda mbali zaidi, nataka hapa niongelee pendekezo ambalo analileta Mheshimiwa Waziri, nadhani ni Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Na. 220. Humu Bungeni tulikuwa tunajadili namna ambavyo tunaweza kusaidia magari ya Serikali badala ya kutumia *diesel* na *petrol* ambayo inakuwa *imported* na *it is very expensive*, twende kwenye gesi asilia tunayozalisha hapa nchini. Leo naona *trend* imebadilika na badala yake Wizara inakuja na tozo ya shilingi 382 kwenye kilo moja ya gesi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hiyo haikubaliki. Siyo tu kwa kuwa *friendly* kwa mazingira, lakini haikubaliki kwa mpango wa kuendelea kuchukua fedha, kuendelea kununua dola. Tunavyoendelea kuweka matumizi ya kuongeza kutumia dola tuna-*encourage* fedha kuzidi kuishiwa nguvu, kukosa fedha na kuendelea kuwa *dependant*. Kwa hiyo, hayo mambo siyaafiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, naongezea hapo. Mnakuja na Sheria ya Sukari, Sura Na. 251, kuwezesha *NFRA* kununua sukari ghafi. Hiyo haikubaliki kokote, na haiwezekani. Tunataka kuua viwanda vya sukari tulivyonavyo hapa! Tunataka kuhamisha ajira za Watanzania wenzetu! Tunataka mashamba makubwa ambayo yameanzishwa leo yafanye kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake hizi dola mnazotaka kuzipeleka nje, vikopesheni hivi viwanda viweze kuzalisha vya kutosha tutengeneze ajira za watu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, kama tunaweza kuwa na *thinking* ya namna ile, hii ni ya kuliumiza Taifa. Badala ya kuwaza kuhamisha fedha, tuanze kurudisha fedha hizi zivasaidie

19 JUNI, 2024

wananchi wetu, tuweze kurudisha fedha, ili tuweze kutengeneza uchumi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuangalie bajeti tuliyonayo leo. Hii bajeti yetu pamoja na mambo mengine, hapa Taarifa ya Kamati imeeleza hivi, kwanza ukopaji wa mikopo ya masharti, tunaita *concession loans*, umeongezeka kwa 48% kutoka kwenye ile tuliyokuwanayo. Ina maana mikopo imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, ukiangalia mapato tuliyonayo *TRA* inachoweza ku-*collect*, mapato yasiyokuwa ya kikodi, lakini pia na Halmashauri tunaweza kuitegemeza bajeti yetu kwa 70% tu. Kwa hiyo, unaona kwamba sisi ni *production for consumption with diversity*. Tunazalisha, tunatumia na tuna-*diversify*. Sasa hili ni Taifa la namna gani jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tunazoweza ku-*collect* hatuendi kulipa wakandarasi kwa wakati, tunaenda kulipa riba. Hapa Taarifa ya Kamati imeeleza vizuri sana, fedha mamilioni na mabilioni ambayo wakandarasi wanadai tunaenda kulipa riba kwenye miradi ya maji, tunaenda kulipa riba kwenye miradi ya barabara. Taarifa ya Kamati imeeleza vizuri ni kwa nini tunaingia kwenye *commitment* ya mikataba wakati hatujapata fedha? Kwamba, Maafisa Masuuli wana-*incur commitment za spending* wakati hawana fedha, ukifika wakati *certificate* zimefikia ku-*mature* wanapaswa kulipa, hawalipi. Ni kwa nini tunaenda hivi na ni kwa nini tunafanya hivi? Tunaiongezea Serikali mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunabanana hapa kwa ajili ya *spending*, kwa ajili ya kulipana mishahara, kwa ajili ya fedha kupotea na mambo mengine kama hayo. Mimi nashauri sana, lakini unaona tumekuwa tukiongea humu ndani kuwa na bajeti ambazo zinakuwa na mrengo wa kijinsia. Ni kwa kiwango gani bajeti zinakuwa zipo *sensitive* kwa wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nieleze wazi. Bajeti ya Wizara ya Maji imeshuka na inavyoshuka wanaoathirika kwa kiwango kikubwa ni wanawake ambao wao ndio wanachota maji wakati wanaume hawapo, wanabaki nyumbani wanahangaika.

19 JUNI, 2024

Naomba Mheshimiwa Waziri hili mliangalie upya na halikubaliki. Hiyo ndiyo namna pekee tunayoweza kuongelea bajeti ambazo zipo *sensitive*, lakini zinawagusa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache, naenda kwenye Jimbo la Kyerwa. Tuna changamoto kadha wa kadha. Changamoto ya kwanza ni barabara na hata asubuhi nimeeleza changamoto ya barabara. Sisi tuna barabara mbili tu; barabara ya kutoka Bugene – Nkwenda, unakuja Kaisho unakuja kutokea Murongo, lakini hiyo barabara unatoka Murongo unakuja Businde, unakuja kutokea Omgakorongo. Hizo ndizo barabara mbili tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi barabara zetu hazitengenezwi tangu mkoloni. Mmetuahidi kilometa 50 za Nkwenda, lakini imekuwa ni ngonjera kila siku. Ninachosikitika sasa wakati Mbunge mmoja amesema hapa kwamba, wengine barabara zilibanduka, sisi hata hiyo ya kubanduka, watoto hawajawahi kuiona lami. Siyo sahihi. Sisi ni walipa kodi, tunastahili lami. Serikali mmeahidi kilometa 50 za lami nami sina uhakika kama naweza kuunga mkono hii bajeti iwapo sisikii chochote kuhusu kuanza kwa hiyo lami. Siyo hiyo tu ya kilometa 50, lakini pia, kulipa fidia kwa wananchi wa Mgakorongo kuja kutokea mpaka Mrongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, nimeongelea changamoto ya vitambulisho vya *NIDA*. Naongea kwa uchungu sana, Wilaya zetu za mpakani ikiwemo Kyerwa, kumekuwa na changamoto ya kubambikiziana kwamba, wewe sio raia. Ukionekana unajitambua, unaweza kujisimamia, upo kwenye siasa, unaambiwa wewe sio raia. Wanakunyima kitambulisho, wanaanza kukubambika kwamba, sio raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uwepo mkakati maalum wa kuja kuandikisha vitambulisho, kama nilivyosema juzi na badala yake tuwe na Maafisa Uhamiaji wanaotufahamu. Mnatuletea watu kutoka wapi, wanaanza kusema huyu ana pua ndefu, huyu fupi na wale hawajui watu wa huko kwetu wanafananaje?

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, muda wangu siyo rafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani. Cha kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili wakafanye kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu wa Tanzania pamoja na wa Jimbo la Tunduru Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kwa namna ambavyo ameleta maendeleo katika Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru yetu kwa ujumla. Tunashukuru sana, wananchi wanaona na wanasubiri mwaka 2025 watakapopata kura nyinyi za ndiyo kwa ajili ya Rais wetu kwa ajili ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda nichangie katika maeneo matatu. Eneo la kwanza kabisa litakuwa ni eneo la kilimo. Jimbo la Tunduru Kusini karibu 98% ni wakulima wa korosho, ufuta, na choroko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kauli yake aliyoitoa wakati wa bajeti ya kuifanya TMX iweze kufanya kazi kwa ajili ya kufanya masoko kwa ajili ya mazao yetu wakianza na ufuta. Sisi ambao tunajua changamoto za wakulima zilivyo, tulifurahi sana na bahati nzuri mfumo ulianza vizuri sana. Kwa upande wa Tunduru wameanza na ufuta, ukaenda vizuri mnada wa kwanza. Kwenye mnada wa pili, wa tatu mpaka mnada wa nne, sasa shughuli imeanza kuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa ya Kamati ya Bajeti imesema changamoto mbalimbali inazokutana na sekta hii ya kilimo na hapa nitaenda moja kwa moja kwenye changamoto za mfumo wa kutumia TMX, ambao kwa sasa ndiyo tunautumia kwa ajili ya kufanya masoko ya mazao ya wakulima wetu

19 JUNI, 2024

ambapo umekwama na unaendelea kukwama kama Serikali haitachukua hatua za haraka kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kwenye bajeti ya kilimo nilizungumza sana kuhusu suala la maghala. Mfumo wa Stakabadhi Ghalani wa kutumia *TMX* unahitaji maghala kwenye ngazi ya vijiji, wilaya na kwenye ngazi ya Taifa. Maghala haya ni kwa ajili ya kuhifadhia haya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unataka *grading* ya mazao kulingana na *quality* ya hilo zao linalotakiwa na kulingana na mteja anayepeleka mazao ghalani, mnunuzi anayenunua hapaswi kufika *site*, anatumia mtandao kununua na *ku-bid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa *specification* zilizopo kwenye *bidding* azikute kwenye ghala kama zilivyo. Kwa isivyo bahati sasa, kwa sababu ya tatizo la maghala, utakuta mazao ya wakulima yanachanganywa tu. Mnunuzi amenunua kutoka kwenye chama X lakini anavyoenda kuchukua anapewa mazao ya chama Y. Ie ni changamoto kubwa kwa *TMX* inapokwenda mbele kama hatutachukua tahadhari mapema kuhakikisha kwamba maghala makuu yanajengwa ili kuhakikisha kila mkulima anaweka mazao yake kulingana na chama chake. Jambo hili linaweza kukwama na likatuletea matatizo makubwa mbele ya safari, kushitakiana kati ya wanunuzi na vyama vyetu vya ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili jambo tusilifanyie mzaha, tutafute fedha za dharura ili mfumo huu uende vizuri na kuwasaidia wakulima. Ni lazima tuwe na maghala ya kuhifadhia korosho na mazao yote ili mfumo uende sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimezungumzia changamoto nyingine ya *TMX* ambayo mpaka sasa bado tunakumbana nayo, ni suala la mfumo wenyewe wa *TMX* kutokufanya minada zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja. Vyama



19 JUNI, 2024

viko vingi na mazao yako mengi, wanahitaji kufanya mnada kila siku lakini TMX wanachokifanya, wanaweka muda, wanapanga saa fulani mpaka saa fulani tutanadi kahawa. Saa fulani mpaka saa fulani tutanadi ufuta Tunduru, saa fulani mpaka saa fulani tutanadi ufuta Kibaha, jambo ambalo kidogo linaleta mkanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tabia za wafanyabiashara wetu, mnada mmoja unachukua zaidi ya masaa matatu hadi manne. Kwa hiyo, wanaahirisha minada mara kwa mara. Jambo hili lina sababisha usumbufu kwa wakulima ambao wanaenda maeneo ya mnada na hata wafanyabiashara wanaotaka kushuhudia kinachoendelea kwenye ule mnada. Tuliangalie hili, Mfumo wa TMX uwe na uwezo wa kufanya mnada zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja ili kuruhusu minada mingi ifanyike kwa wakati mmoja. Matokeo yake tunasababisha madhara ya kibiashara ambayo yanafanya wakulima wetu wakose tija kutokana na hii minada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine iliyojitokeza kwa sasa hivi ambayo tunatakiwa tuifanyie kazi kwa haraka sana ni suala la upungufu wa wateja wanaoingia kwenye minada hii. Natoa mfano, mnada wa kwanza wa Tunduru ulikuwa na wateja watatu tu ambao walinunua kwa shilingi 3,629 bei ya jumla, ndiyo bei ya average, kulikuwa na tani 701.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada wa pili ulikuwa na tani 1,064 wakaongezeka wakawa watano tu. Mnada wa tatu kulikuwa na tani 1,884 wakawa wateja sita tu na hapa ndiyo mtihani ulipoanza kujitokeza. Mnada wa leo tumepeleka sokoni tani 1,502 lakini wateja wameshuka na bei zinaendelea kushuka kutoka shilingi 3,629 ya mnada wa kwanza, leo tumeuza kwa shilingi 3,152. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto, ndani ya wiki tatu tumepunguza shilingi 477 kwa mkulima wetu lakini kwa kadiri ya mazao yanavyokuwa mengi ghalani, wanunuzi wanapungua na bei zinapungua. Tunaomba sana Serikali kupitia TMX...

19 JUNI, 2024

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpakate, kuna Taarifa. Mheshimiwa Kungu, tafadhali Taarifa.

### **TAARIFA**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji kaka yangu Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, kwamba mnada wa tatu Tunduru pamoja na kushuka bei kwa Mfumo huu wa TMX lakini mnada wa tatu tani 278 zilikosa mnunuzi maana yake zilibaki. Kwa hiyo, mfumo huu unakwenda kubakisha hata mazao ya wakulima badala ya kumaliza mazao yote, kuyanunua kama ilivyokuwa kwenye mfumo ule uliopita. Kwa hiyo, Serikali iangalie kwa umakini na ukiendelea namna hii, tunakwenda kuwagombanisha wakulima pamoja na Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate, unaipokea Taarifa ya Mheshimiwa Kungu?

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili. Ndiyo nilikuwa naelekea huko. Ni moja ya changamoto ambayo imeanza kujitokeza kwenye minada hii inayotumia TMX. Hata wenzetu wa Pwani juzi wamebakisha zaidi ya tani 1,000 kwenye mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inatakiwa Serikali ichukue hatua mara moja, kuhakikisha kwamba wanaona sababu zinazosababisha nini kinachofanya; moja, wanunuzi waendeleo kupungua; pili, kwa nini bei ziendeleo kupungua? Tatu, ni kwa nini mazao yabakie ghalani? Hii ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hizi tunazoziona, wakiona tatizo limekuwa kubwa, wasione dhambi kurudi tulikotoka kwa sababu lengo la mkulima ni kutaka kupata fedha. Sasa tunapopeleka korosho na mazao yetu ghalani halafu wanunuzi hawapo na bei inashuka, matokeo yake ni kwamba

19 JUNI, 2024

mkulima anachelewa kupata malipo yake ya haki ambayo alitakiwa kuyapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili lazima tufanye juu chini utafiti ufanyike kwa haraka sana kabla hatujafika hata msimu wa korosho. Maana yake tabia hii imeanza kwenye mazao madogo, ikifika kwenye korosho huko Waheshimiwa Wabunge wa Kusini tunakuwa na shida sana. Kama jambo hili halitatafutwa muafaka na kufanyiwa utafiti kupata majibu, hili jambo litaharibu mfumo mzima wa ununuzi wa korosho na mazao mengine kutumia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo la pili niongelee kuhusu suala la barabara. Kila nikisimama hapa kwenye Bajeti Kuu hata Wizara ya Ujenzi, nilizungumzia sana suala la ujenzi wa reli yetu ya Kusini kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unafahamu Mkoa wa Ruvuma tumepata neema kubwa sana ya kuwa na makaa ya mawe. Magari yanayopita kwenye barabara ya kutoka Songea kwenda Njombe, Songea kwenda Mtwara, Songea kwenda Dar es Salaam, neema hii imekuwa balaa kwetu kwa sababu barabara zile sasa zina hali mbaya. Tunahitaji fedha nyingi kila wakati kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu wa Kusini akisimama hapa anaongelea Barabara ya Mtwara – Lindi mpaka Dar es Salaam na ushahidi upo kwamba sasa hivi iko hoi *bin* taabani. Barabara ya kutoka Songea – Tunduru mpaka Mtwara, kutokana na malori yale makubwa iko hoi *bin* taabani; mashimo ni mengi na haina zaidi ya miaka kumi tangu imekamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Songea mpaka Njombe, hali ni mbaya zaidi, barabara hii wakati imekamilika mwaka 1984 mimi nilikuwa kidato cha tatu. Kwa kweli tunaomba Serikali kwenye suala la kujenga reli ya Kusini waipe kipaumbele kuokoa barabara hizi za Kusini ili ziweze kupona. Pia, naomba sana Barabara ya Mtwara – Pachani – Nalasi mpaka Tunduru, barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu akiwa Makamu

19 JUNI, 2024

wa Rais 2015, akiwa mgombea 2020. Tunaomba tumpe heshima yake barabara ile itengenezwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matengenezo hayo, tuna bahati katika Kata ya Mbesa, tuna machimbo, pale kuna mwekezaji wa copper anataka kuwekeza zaidi ya dola 15,000 kwa kutumia barabara ile. Copper ni kama makaa ya mawe na chuma, huwezi kubeba mfukoni, utabeba na malori makubwa. Kwa hiyo, ujenzi wa reli hii utaokoa Tunduru kwa maana ya copper, utaokoa Songea na utaokoa mpaka barabara ya kutoka Songea kwenda Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama reli hii itaweka kipaumbele, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji aone umuhimu wa kujenga reli hii pamoja na kufufua ule Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Nyimbo hizi tumezichoka kila mwaka kusema, Liganga na Mchuchuma, Liganga na Mchuchuma, tunatafuta fedha za kigeni, lakini tunatumia fedha nyingi kutafuta chuma kutoka nje wakati chuma kimekaa hapo Liganga, ni cha kutosha ambacho kingeweza kutusaidia sisi kufanya mambo yetu kwa maana ya... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, hitimisha tafadhali.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. Nina maana ya kwamba hiki chuma kingechimbwa tusingekuwa na matumizi ya dola kwenda kufuata chuma nje. Tungeweza kuwekeza hapa ndani. Nondo, *square pipe* na biashara zote za chuma zingeweza kufanywa kutokana na chuma chetu ambacho kipo kimelala hakina matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali aangalie suala la Liganga na Mchuchuma na kupewa kipaumbele aweze kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika, atafuatia Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema mawili matatu kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Amekuwa ni Rais ambaye amewatazama Watanzania katika hali zao na kuwahudumia kama ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nachukua nafasi hii kumshukuru na kuwashukuru wasaidizi wake, Makamu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan katika kulitumikia Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba ifahamike mpaka dakika ya sasa kwamba, tunaposimama kama Wabunge wa Mkoa wa Kigoma bado mahitaji yetu hayajatekelezwa na ndiyo maana tunasimama kwanza, kukumbusha; na pili, kueleza Serikali yetu sikivu ili iweze kufahamu namna gani watu wa Kigoma tuna uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mikoa yote ya Tanzania mpaka dakika hii tunayozungumza mikoa yote imeshaunganishwa kwa lami, imebaki Kigoma peke yake na sehemu iliyobaki ni ndogo sana ambayo nasimama leo kumwomba sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kuona namna ambavyo atatutoa katika hii dhahama Watu wa Kigoma ili nasi tuweze kuingia kwenye *record* ya kuweza kuwa miongoni mwa mikoa iliyounganishwa kwa lami kama ilivyo mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

19 JUNI, 2024

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mekanika, kuna Taarifa.

### **TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa mchangiaji, anachangia vizuri sana, lakini siyo kweli kwamba nchi yote imeunganishwa, ila bado Mkoa wa Kigoma tu. Sisi wa Lindi na Morogoro bado hatujaunganishwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mekanika.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea na hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kigoma tuna barabara hii ya Uvinza ambayo barabara hii ilikuwa inatokea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mekanika, Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 77 inakutaka useme au unaipokea au hupokei taarifa.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali nayo iweze kumwona. Nimesikia taarifa yake na nimeipokea. Serikali iweze kuona umuhimu wa kumwezesha naye pia ili na mkoa wake uweze kuunganishwa kwa lami ikiwa ni mahitaji ya Watanzania wa maeneo mbalimbali, lakini ni sisi Kigoma na maeneo aliyotaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Barabara hii ya Uvinza ambayo imeanzia Tabora. Barabara hii kipande cha Tabora sasa kimekamilika kwa lami lakini ukija kipande kinachoiunganisha Kigoma kutokea Tabora bado kilometa 51 mpaka sasa. Kwa kweli tunaiomba Serikali ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kuona namna bora ambayo itatuwezesha sisi watu wa Kigoma tuingie kwenye uchaguzi kipande hiki kikiwa kimekamilika. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba, ukiangalia barabara hii na mkandarasi aliyepo, bado anasuasua na tunaomba kwa kweli Serikali iweze kutia mkazo sana fedha zipelekwe na mkandarasi yule aweze kulipwa ili kipande hiki kiweze kuendelea kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tuna barabara ambayo tumeishaijeleza Serikali, kutokea Mwandiga inakwenda mpaka Kata ya Mwamgongo na baadaye inaelekea kwenye Soko la Kimataifa la kule Kagunga. Barabara hii imekuwa ni changamoto sana, ambapo toka nimeingia Bungeni nimeipigia kelele sana ya kwamba watu wa Ukanda wa Ziwa na wao. Ni wakati mwafaka sasa Serikali iweze kuona namna bora ipeleke miundombinu hii ya barabara ili iweze kufika katika kata hizo zaidi ya nne ambazo bado hazijafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa sana na Mheshimiwa Waziri Bashungwa. Tumekwenda Wizarani kwake, tumezungumza naye sana kama Wabunge wa Mkoa wa Kigoma, naomba sana mtani wangu aweze kuangalia namna bora ambayo ataweza kuzifungua hizi kata nne ili ziweze kupata miundombinu hii ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba niseme juu ya hali ya biashara katika Mkoa wetu wa Kigoma na nchi ya jirani ambayo sisi watu wa Kigoma tunategemea biashara hii kuweza kukua kwa haraka kwa sababu ndiyo uchumi mkubwa wa Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2009 zinaonesha bidhaa ambazo zimepita katika mpaka wa Kigoma zenye thamani ya dola bilioni 600 zimepita katika mpaka wetu wa Kigoma lakini ukichukulia mipaka hii mingine, mpaka wa Tanga, Arusha, Holili na kwenda mpaka Namanga, thamani ya fedha zilizopita pale ni thamani ya dola bilioni 500. Ukiangalia mpaka wa Kigoma peke yake umeweza kuipiku hii mipaka yote mingine kutoka mwaka 2019. *(Makofi)*

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hali ya Bandari ile ya Kigoma imekuwa ni kavu sana. Ukiangalia, ni meli moja tu ndiyo utaikuta pale inashusha, lakini ukienda upande wa pili utakuta meli nyingi zinachanganya kupakia na kushusha mizigo kwa ajili ya kuelekea katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha wafanyabiashara wa huko Karema, Lubumbashi hata Kabwe nchini Congo, hivi sasa wanakwenda kupita nchi ya Burundi kwenda kufanya biashara zao nchi ya Burundi na wengine sasa wanaingia nchini Uganda na sababu kubwa peke yake ni urasimu ambao unaendelea katika Bandari yetu ya pale Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaweza akalitazama hili. Hawa wafanyabiashara wanaokimbilia Mombasa wanakwenda Burundi, wanakwenda mpaka nchini Rwanda walikuwa wanapitisha mizigo mingi katika Bandari ya Kigoma, lakini hivi sasa wamekimbia. Jambo ni dogo tu; zipo Sheria ya Vipimo ambayo imeweza kuumiza uchumi wa Mkoa wetu wa Kigoma kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo sheria ya vipimo inaitwa Sheria ya Vipimo vya Habatani inaweza ikatazamwa kwa umakini zaidi kwa sababu inachepusha biashara nyingi ambazo zinakwenda kwenye hizo nchi ambazo nimezitaja na Sheria hii ya Habatani inachukua tu sura mbili; sura ya kwanza ni Sheria ya Kipimo ambayo inapima kwa uzito na kwa ukubwa. Hii kwa ukubwa, kitaalam ndiyo CBM ambayo hivi sasa, hii sheria imeweka *mandatory* ya sheria au kiwango cha kodi yoyote inayotozwa inaamuliwa na Afisa wa pale bandari, jambo ambalo linatoa mianya mikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wa hizi nchi wanakimbia bandari yetu kwa sababu kumekuwa na urasimu mkubwa. Kwa hiyo, na hilo Mheshimiwa Waziri na Bunge tuweze kuona namna hii sheria itaweza kubadilishwa hatimaye tuweze kukomboa uchumi huu wa Kigoma na Bandari yetu ya Kigoma.



19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja kwa sababu ni bajeti ambayo inabeba mambo yote yanayohusu wananchi. Tumeweza kuzungumza juu ya jambo la Ziwa. Kwa kweli hali ya kufunga Ziwa tunaona kwamba imeweza kuumiza uchumi mkubwa wa wavuvi wengi katika Mkoa wetu wa Kigoma. Sasa hii imesababisha hali ambayo uchumi wa watu wetu umezorota kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano tu mdogo, hivi sasa kumekuwa na vizimba ambavyo vimeletwa huko Kigoma, lakini vizimba 29 vimejengwa katika Jimbo la Kigoma Mjini na kwenda kule ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Jimbo la Kigoma Kaskazini hakuna hata kizimba kimoja, na hali hii ambayo imeweza kuwaingiza wananchi wengi kwenye hali ya dimbwi la umaskini kwa sababu ziwa limefungwa, lakini ukilinganisha mkataba ule wa kufunga ziwa ulikuwa ni wa zaidi ya nchi tatu mpaka nne. Hali hii tunaomba sana Serikali iweze kutazama namna bora ili tuweze kuangalia kwa sababu wananchi waliumizwa. Wananchi walikuwa na mikopo ambao wametoa kwenye mabenki lakini ziwa limefungwa na hali ya uchumi wao umezorota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya machache hayo, nakushukuru na ninaunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makanika. Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo yeye pamoja na Serikali wameteteleza katika Jimbo la Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka hii mitatu iliyopita, Jimbo la Serengeti limepata miradi mikubwa sana ya maji, barabara, elimu, afya na kadhalika. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa pamoja na Serikali yote.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia kwa kuiongoza vizuri nchi yetu katika kuelekea kujenga uchumi mkubwa pamoja na kuondoa umaskini. Katika kuzingatia dhana kubwa kabisa ya ushindani wa uchumi katika mataifa mbalimbali yanayotuzunguka na mataifa mengine pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Wizara hii ya Fedha pamoja na Wizara ya Mipango kwa kazi ya uwasilishaji wa Mpango ule wa Taifa wa Maendeleo pamoja na bajeti ambayo kwa kiasi kikubwa imeonesha kulipeleka Taifa katika kujenga uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ninazishauri Wizara hizi mbili kwamba ni vema zikazingatia pia mambo haya makubwa manne tunapoendelea ku-focus kuipeleka nchi yetu katika kujenga uchumi na kuondoa umaskini, kwa sababu Taifa lolote lile ukiangalia wachumi wakubwa duniani wakiwemo akina John Keynes, akina Adam Smith wanasema, Taifa lolote duniani ambalo linataka kukua katika uchumi lazima lizingatie mambo manne. Jambo la kwanza ni lazima lijenge uchumi ambao unategemea sana kilimo pamoja na viwanda, kwa maana ya kwamba lazima tujenge uwezo mkubwa wa uzalishaji katika kilimo na katika viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima Taifa hilo lihakikishe linajenga kwa kiasi kikubwa miundombinu bora na ya kisasa ambayo inagusa maeneo ya mawasiliano na usafirishaji hasa kuelekea katika maeneo yote yenye uzalishaji wa mali. Jambo la tatu ni lazima Taifa lijielekeze katika kujenga uwezo mkubwa wa kiteknolojia na jambo la nne ni lazima Taifa hilo lijielekeze sana katika kujenga rasilimali watu wenye ujuzi mkubwa na ambayo ina nidhamu ya kazi na inayojituma katika kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii pamoja na mpango wetu wa maendeleo, naomba kugusa maeneo mawili tu katika hayo manne, nikianza na eneo hili la ujenzi wa miundombinu bora ya kisasa na inayogusa maeneo ya

19 JUNI, 2024

mawasiliano na usafirishaji katika maeneo yetu tunayoyategemea katika uchumi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu maeneo yetu tunayoyategemea sana katika uchumi hayajafikiwa vizuri na miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano. Tumejaribu kwa kiasi fulani, naipongeza Serikali imefanya, lakini bado yapo maeneo ambayo ni vema yaweze kuzingatiwa kwa haraka kwa sababu tunajipotezea wenyewe uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa mazingira ya ushindani uliopo duniani unapotaka kujenga uchumi ni lazima uchukue mali kutoka kwa mataifa mengine, lazima uchukue fedha kutoka kwa mataifa mengine. Ili uchukue fedha zao na mali zao lazima yale maeneo ya muhimu katika uzalishaji yafikike, lazima mawasiliano yawepo. Huko nyuma kipaumbele chetu katika ujenzi wa miundombinu kilikuwa zaidi katika kuhakikisha kwamba tunaunganisha maeneo ya kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona haja ya uwepo wa Tume ya Mipango. Leo maeneo yetu yenye uzalishaji mkubwa yapo mengi, lakini nitaje moja ambalo nalifahamu zaidi. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni jambo ambalo lipo wazi, imeendelea kutuingizia pesa nyingi sana. Sasa mataifa ili waje na kuleta pesa, lazima eneo hili lifikike, lakini mpaka leo barabara ile ya kutoka kule Musoma Makutano ambayo inatuunganisha kutoka Kenya inafika Makutano, inapita Butiama – Sanzate – Nata mpaka kule Mugumu na kuunganisha na Hifadhi ya Serengeti haijawahi kukamilika kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naiomba Serikali, jinsi tunavyochelewa kuiunganisha hifadhi hii, watalii wanavyopata shida kufika eneo hili, tunaendelea kujichelewesha katika kujenga uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Barabara, imekuwepo ajenda ya muda mrefu ya kujenga uwanja wa ndege mkubwa katika eneo hili, lengo kubwa ilikuwa kuona kwamba

19 JUNI, 2024

watalii wanafika eneo hili kwa urahisi na kwa muda mfupi ili tuweze kukusanya pesa hizi za mataifa. Kwa muda mrefu zimeundwa timu nyingi sana huko nyuma. Imewahi kuundwa timu ya kwanza miaka kati ya mwaka 2010 – 2015 haikufika mahali popote. Ikaja timu nyingine ya pili 2017 – 2019, wakaja Maliasili nao wakaunda timu lakini hakuna kilichoendelea, wakaenda watu mpaka nje ya nchi wakazunguka hakuna kitu kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeundwa tena timu nyingine ya nne tarehe 16 Mei, 2024 ipo barua inayoonesha tena timu nyingine ya nne, barua yenye Kumbukumbu Na. CAD.26/3180/1C/117. Barua hii ime-circulate kenye ma-group mengi sana ya mitandao hii ya kijamii, sasa tumejuliza kwa nini timu nyingi ziundwe? Lazima kuwepo *commitment* ya fedha. Mimi niishauri sana Wizara, tunahitaji kuingia kwenye kufanya *commitment* na siyo kutengeneza mipango mingi, siyo kutengeneza timu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotaka kujenga viwanja, kujenga barabara mbalimbali ndani ya nchi yetu, hatukuunda timu nyingi hivi. Tena tumefanya miradi mikubwa sana bila uwepo wa timu nyingi hizi. Pia ukiangalia wenzetu katika mambo tofauti tofauti hawakuwa na mikakati na mipango mingi ya namna hii. Nitolee mfano tu nchi ya Malawi. Malawi wana eneo dogo kuliko sisi kama kilomita za mraba 200,000 hivi. Sisi ni zaidi ya 940, lakini wana *export* chai mara 10 zaidi yetu. Sisi tumekuwa na mipango mingi, mikakati mingi ya kitaifa kuhusu kilimo, lakini hatukuwahi kuwazidi watu hawa. Kwa nini? Ni kwa sababu tumekosa *commitment* ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Wizara hii ya Fedha pamoja na Wizara ya Mipango waone sasa umuhimu wa ku-*prioritize* maeneo ambayo yanaweza kutuletea uchumi mkubwa ambayo mataifa yanaweza kuja na kuleta fedha. Tujenge miundombinu ikamilike na tukusanye fedha tuweze kuondoa umaskini. Tusipofanya kazi hii tunaendelea kujichelewesha, tunaendelea kufanya Taifa hili kubaki kwenye makusanyo madogo na kutojipatia maendeleo ambayo Watanzania wanakusudia. (Makofi)

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami nichangie hotuba ya Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazoendelea kufanya kwenye Taifa letu. Tumejiridhisha na kuona namna ambavyo Mheshimiwa Rais anavyoendelea kufanya kazi kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili na Waheshimiwa Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanazofanya na kwa bajeti ambazo wameleta hapa nzuri na ambazo zinaleta taswira kwa nchi yetu katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu ambayo nataka nichangie. Jambo la kwanza ni kukubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kurudisha *wharfage* kukusanywa na TPA. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuliona hili. Suala hili lilichangiwa sana katika Wizara ya Uchukuzi, kwa kweli linaenda kuleta tija. Kama bandari watafanya ukarabati inavyotakiwa kwa kupitia fedha hizi za *wharfage*, zitaenda kusaidia sana katika suala zima la ukusanyaji wa kodi zitokanazo na bandari kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, TRA ilikusanya kodi zitokanazo na bandari kwa maana ya kodi za forodha kiasi cha shilingi trilioni tisa. Tuna imani kwamba sasa zinaenda kuongezeka kwa sababu miundombinu ya bandari itaenda kuimarika. Napongeza sana kwa hatua hii, ni hatua njema ambayo inaleta taswira ya makusanyo mazuri katika nchi yetu.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili ambalo nataka kuchangia ni eneo hili ambalo limelizungumzia matumizi ya mfumo wa malipo kidigitali. Mfumo huu ni mzuri sana. Mfumo wa *TIPS* ambao umetengenezwa na watu wetu wa *BoT* ni mfumo ambao utatusaidia sana nchi yetu katika ukusanyaji wa mapato ya *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze kidogo nini faida ya mfumo huu? Mfumo huu utaenda kutusaidia hasa katika kujua miamala ya kibiashara iliyofanyika kwa mfanyabiashara, pia inaenda kuleta uwazi mkubwa wa miamala yote inayofanyika kwa wafanyabiashara na watumiaji wa mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme jambo moja ambalo sasa inatakiwa tujielekeze kwa matumizi ya mfumo huu ili kupunguza matumizi ya malipo kwa kutumia *cash*. Nchi zilizoendelea ni zile ambazo nimeondokana na mfumo wa kulipa kwa kutumia *cash*, kwa sababu mfumo huu kwa kulipa kwa kutumia *cash* una mambo mengi hasa katika ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanakwepa kodi kwa kutumia mfumo huu wa malipo kwa kutumia *cash* kwa sababu mtu anapewa *cash*, harekodi popote biashara imemalizika, amepata chake, hamna sehemu alipolipa; lakini kwa mfumo huu ambao Mheshimiwa Waziri amekuja nao wa kupunguza malipo yoyoye kwa kutumia *cash*, kwa kweli itaenda kusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwa takwimu kwamba kwa sasa hivi malipo kwa kutumia mfumo huu ni 20% tu malipo yanayofanyika. Bado tuna safari ndefu, naomba sana Mheshimiwa Waziri asimamie hili, tuwasaidie wafanyabiashara kupata mashine za *PoS* kwa ajili ya malipo ya kutumia mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wafanyabiashara wajiunge na mfumo huu ili kusudi waweze kusaidiwa na kufanya malipo yatokanayo na mfumo huu yaende vizuri. Mfumo huu unaweza ku-*discourage* watumiaji kama hatutaweka misingi mizuri ya makato ya miamala. Mfano, nikupe jambo moja hapa na ungenisikiliza ingekuwa vizuri sana.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano wa jambo moja hapa. Ukitoa fedha kutoka kwenye mabenki, kwa benki zetu za kibiashara ukatoa kuja kuleta kwenye mtandao wa simu, mfano M-PESA kiasi cha shilingi 100,000 ukileta kwenye mtandao wa simu, kwa maana ya laini, benki inakukata shilingi 6,000 kwa shilingi 100,000 lakini ukienda kulipa kwa mfanyabiashara kwa matumizi ya manunuzi ya bidhaa kwa kutumia Lipa Namba kwa kiasi cha shilingi 100,000 utakatwa shilingi 2,000. Unaiona laki moja umekatwa shilingi 8,000. Sasa kwa wananchi wetu wa kawaida, shilingi 8,000 ni kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza wananchi wa Busega leo kwenda kufanya *transaction* ya shilingi 100,000 kwa kununua bidhaa alipe shilingi 8,000 hatakubali. Ataona ni bora achukue bodaboda alipe shilingi 1,000 akachukue Shilingi 100,000 kwenye ATM halafu akaenda akafanya manunuzi. Hapo tutakuwa bado hatujasaidia nchi katika suala zima la kutumia mfumo huu. Ili mfumo huu utumike vizuri, anza kwanza na haya matatizo ambayo yanaweza kuwasababisha wananchi kuwa *demoralized* kwenye suala zima la kutumia mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekupa mfano hapa wa shilingi 100,000 namna inavyokatwa kwenda kwa mlaji wa mwisho huyu uliyemlipa kwa kutumia Lipa Namba, kama angekatwa makato ya kawaida mfano Shilingi 100,000 nikitoa hapa kuja kwangu kwenye M-PESA wakakata shilingi 2,000 badala ya shilingi 6,000 mimi inani-*encourage* kutumia mitandao ya simu kufanya manunuzi lakini kama tukifanya hivyo maana yake haya manunuzi ambayo tunasema tunaenda kununua kwa *cash* kodi yake haitafahamika.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon kuna taarifa.

### **TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana kwa asilimia mia moja na anachokizungumza Mheshimiwa Simon.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *incentives* tu zinaweza zikaisaidia Serikali kutoka kwenye huu mfumo wa kutumia *cash* kwenda kwenye *cashless*. Hata kwenye *EFD* Mheshimiwa Waziri tungeshauri shusheni *VAT* kwa mtu ambaye analipa kwa *cashless economy* kwa maana kwa mfumo kuliko mtu anayelipa kwa *cash* hii itasaidia Watanzania wengi kushawishika kutumia fedha au kulipa fedha kupitia kwenye mfumo na hatimaye Serikali ikaiona fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shusheni *VAT* angalau mfikishe kutoka 18% kwenda 16% ili iweze kusaidia Watanzania wengi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Simon unapokea taarifa ya Mheshimiwa Festo Sanga?

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa kutoka kwa mtu bingwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yake, mfano sasa hivi nikitoka hapa niende *ATM* nikachukue shilingi 100,000 wanakata shilingi 2,000, lakini nikitoa shilingi 100,000 hiyo hiyo kuja kwenye *M-PESA* nakatwa shilingi 6,000. Huoni hili ni tatizo kubwa. Sasa tutamshawishi vipi Mtanzania atumie miamala kupitia simu badala ya kutumia *cash*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikata kumsaidia Mtanzania ni lazima kwanza tuanze na benki za kibiashara waweze kupata faida kidogo ambazo amezungumzia *incentives* zile ili tuweze kwenda kwenye mfumo. Huu mfumo unasaidia eneo lipi? Hata wale ambao tunapiga kelele wanakwepa kutoa *EFD*, mfumo utamwonesha kwamba wewe mfumo unasema *sales* zako ni shilingi bilioni 200, mbona *EFD* zinaonyesha shilingi bilioni 100? Hukutoa risiti huku kwa sababu mfumo hauwezi kudanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tulione hili tuweze kuwasaidia Watanzania na tuisaidie nchi. Tunapoteza kodi na walipakodi wameshajua muda mwingine mnaziangalia *account* zao. Kwa hiyo, kuna wafanyabiashara wengine wanakuwa na



19 JUNI, 2024

*account* ya kampuni na *account* ya *personal* zote zinapokea fedha za biashara. Akikusanya pale amekusanya shilingi milioni 200, shilingi milioni 100 anapeleka kwenye kampuni; shilingi milioni 100 anapeleka kwenye *account* yake ya kawaida ili mkienda kuangalia *account* mjue mauzo yake hamtayapata yote, lakini tukitumia mfumo ambao huu umekuja nao wa *TIPS* ni mfumo mzuri, nauunga mkono, lakini lazima tuone vitu ambavyo vinaweza kuleta changamoto ikiwepo na gharama za miamala kama nilivyosema na kama alivyosema rafiki yangu Mheshimiwa Sanga hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, barabara ya kutoka Mwanza – Tarime kipange ya kutoa Nyanguge kwenda Lamadi, hiki kipande ni kibovu, ni kibovu sijawahi kuona. Barabara hii ni barabara ya kiuchumi, ni barabara ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani atakavyokuja kuzungumza wakati wa bajeti yake, aseme hili, lakini tunatamani kuona barabara inatengenezwa, tunatamani kuona barabara hii inakarabatiwa kwa sababu ni barabara kuu. Tunaomba aitembelee barabara hii ili aweze kuona namna ilivyoharibika kutoka pale Nyanguge kuelekea Lamadi Jimboni kwangu tuweze kuitengeneza iweze kuleta uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais, tumetengeneza Daraja la Msisi, sasa ili litumike vizuri ni lazima barabara nyingine na zenyewe ziwe na ushirikiano. Kama barabara hizi hazina ushirikiano, sasa mizigo kutoka kule Tarime tunapitisha wapi kwenda Geita? Barabara hizi lazima ziwe na ushirikiano ili ziwe na matokeo chanya kwa Watanzania na tuweze kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimeona kwenye bajeti yako ukurasa wa 20, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amewapa *MSD* mtaji wa shilingi bilioni 100 kitu ambacho ni kizuri. Nilitamani atuambie atakapokuja hapa aseme, hizi fedha shilingi bilioni 100 alizowapa *MSD* ni sehemu ya deni wanalodai? Kwa sababu *MSD* ukisoma taarifa zao za fedha wanamdai shilingi bilioni 260. Sasa

19 JUNI, 2024

huu mtaji aliowapa, ni nje ya deni? Kama amewapa kama mtaji nitashangaa kwa sababu *it was very simple*. Awalipe tu deni lao shilingi bilioni 260, achane nao, basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mheshimiwa Waziri alitazame vizuri hapa. Kama amewapa mtaji wa shilingi bilioni 100, *it is better offset* kwenye deni shilingi bilioni 260, wabakiwe na deni la shilingi bilioni 160, wamalizane. Hakuna sababu za kuendelea kusema tumewapa shilingi bilioni 100 kama mtaji halafu wao huku kwenye vitabu vyao wanaendelea kudai shilingi bilioni 260. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali ichukue shilingi bilioni 260 isiwe na madeni makubwa, amalizane nao. Awape fedha zao zile shilingi bilioni 100, wakubaliane kwamba bado shilingi bilioni 160 wanawadai wamalizane ili vitabu vya Serikali, vitabu vya MSD visomane na kuleta tija na kutokuwa na madeni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja hapa tunazungumzia madeni, madeni, ili tuweze kufanya vizuri zaidi, nilikuwa nafikiri Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu, basi nitashawishika aniambie hizi fedha shilingi bilioni 100 na hili deni la Shilingi bilioni 260 zimekaaje? Kama aliwapa mtaji, pia atupe mkakati ni kwa namna gani hili deni la shilingi bilioni la 260 ambalo zinadaiswa na MSD anaenda kulilipa ili wananchi wetu waendeleo kupata huduma, kwa sababu fedha hizi ukienda MSD wanakwambia tunaidai Serikali, bado haijatulipa na mwisho wa siku dawa zinakosekana kwenye taasisi zetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Simon, muda umeisha.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri umefanya mambo mazuri kwenye bajeti, haya ambayo nimeyazungumza natamani siku ya kuhitimisha utupe majibu yake.

19 JUNI, 2024

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmepata fursa ya kuchangia kwa niaba yetu. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri mliopata nafasi ya kufafanua, zaidi Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara husika hizi mbili pamoja na Naibu Mawaziri ambao mmetumia muda wenu kupokea ushauri na maoni ya Wabunge kuhusiana na mapendelezo ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho. Ninaahirisha kikao chetu cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.04 Jioni, Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis,  
Tarehe 20 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*